KCSE 2025 FINAL PREDICTION

KISWAHILI

(JARIBIO LA KCSE 1-10)

Mkusanyiko huu una maswali yaliyopangwa vyema, ya kina, na ya kina ya ubashiri yanayolenga KCSE 2025. Imeundwa ili kuakisi miundo halisi ya mitihani, inashughulikia mada kuu, na kuimarisha utayari wa wanafunzi. Inatoa maswali ya utambuzi, yanayolenga mtihani ili kujenga kujiamini, kuboresha utendaji kazi na kuhakikisha mafanikio ya kitaaluma.

MASWALI YA KUTARAJIA MITIHANI YA KCSE 2025!

CONFIDENTIAL!

Kwa Mipango ya Kuashiria, Pigia
Bw. Isaboke 0746 222 000 / 0742 999 000

SIRI YA MAFANIKIO KCSE

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA KWANZA)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika insha* ***mbil****i. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***

b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

c) *Kila insha isipungue maneno* ***400.***

d) *Kila insha ni alama* ***20.***

e) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Swali la lazima.

Wewe ni mtaalamu aliyebobea katika uwanja wa ushauri nasaha. Umealikwa na mwalimu mkuu ili mzungumze kuhusu mambo yanayoweza kutatua msongo wa mawazo miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari. Andika dayolojia kati yenu.

2. Matumizi ya kompyuta yana faida na hasara kwa vijana. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: **Baada ya dhiki faraja**.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo:

Wingu la moshi lilitanda jioni hiyo tulipokuwa tukitoka shuleni. Hatukuamini macho yetu. Tulichanja mbuga**…**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA KWANZA)

KISWAHILI

102/2

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

- *Andika **jina lako** na **namba yako** katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Weka **sahihi yako** na **tarehe** ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa*
- *Jibu maswali yote.*
- *Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	

UFAHAMU **(ALAMA 15)**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuta.

Ufisadi ni jinamizi ambalo limekuwapo ulimwenguni kote kwa miaka na mikaka. Madhara ya utoaji na ulaji rushwa kwa nia ya kujitajirisha au kupata upendeleo fulani haliwezi kupuuzwa. Ni jambo ambalo li kinyume na maadili au kaida za kijamii. Mojawapo ya madhara ya ufisadi ni kuwepo kwa maendeleo duni nchini. Kudorora kwa maendeleo nchini kumesababishwa na athari hasi mbalimbali za ufisadi. Kutolewa kiasi fulani cha darahima kama hongo ni kiini mojawapo cha kuwapo kwa maendeleo finyu nchini. Hii ni kutokana na ukweli kuwa chirimiri husababisha kupunguzwa kwa kiasi cha fedha za kutekeleza miradi mbalimbali. Si ajabu wafanyakazi wa kutekeleza miradi kukosa kulipwa au kupunjwa kwa kupewa mshahara wa kijingujiko, kukosa kulipwa au hata kulipwa nusu ya mshahara.

Visa vya ubadhirifu wa pesa zilizotengewa miradi mbalimbali vimeripotiwa katika maeneo tofauti tofauti nchini. Aghalabu, jambo hili hutendwa na wasimamizi wa hazina ya maendeleo. Mathalani, inasikitisha kuwa baadhi ya watumishi wa umma hutumia fedha za maendeleo katika safari humu nchini na hata ughaibuni zisizo na manufaa kwa taifa. Wao hukosa uaminifu na huongozwa na tamaa na ubinafsi uliopita mipaka. Watu hawa hupuuza ukweli kuwa tamaa huja kabla ya mauti. Jambo hili huifanya miradi lengwa kunyimwa pesa zinazohitajika.

Kutokana na ufisadi, kumekuwa na miradi ya kiwango cha chini. Hii ni kutokana na kununuliwa kwa malighafi ghushi ya kutumiwa viwandani au hata katika ujenzi wa miundombinu. Ukweli ni kuwa miradi inayotekelezwa hudumu katika hali nzuri kwa mwia mfupi tu. Hatimaye ukarabati wa miradi iliyofanywa huanza ; hali inayosababisha matumizi mabaya zaidi ya pesa za umma.

Aidha, kudinda kwa wafadhili wa miradi mbalimbali kuipa nchi pesa kuanzisha na kuendeleza miradi fulani hutokana na ufisadi. Wahisani hawa huhofia matumizi mabaya ya **ghawazi**. Matokeo yake huwa kutotekelezwa kwa miradi mikubwa ambayo huweza kuwa kitega-uchumi kwa watu wengi nchini. Kwingineko miradi mingi hukosa pesa za kutosha na kuifanya kutokamilika ipasavyo.

Isitoshe, **kupakwa mafuta viganjani** kwa wanaostahili kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa imefikia kiwango kinachohitajika ni sababu nyingine ya maendeleo duni. Ni kutokana na hongo wao huidhinisha kazi duni. Kwa mfano, kuporomoka kwa majengo ambako tumeshuhudia mara kadha na kusababisha vifo kunatokana na utepetevu huu. Watu wengi hupoteza mali huku mchango wa kuleta maendeleo kwa waliolemaa ukiadimika.

Ni wazi kabisa kuwa kiasi kikubwa cha miradi dhaifu hutokana na chauchau. Serikali pamoja na wananchi wana jukumu kubwa la kuliangamiza janga hili.

Maswali

(a) Fafanua vikwazo **vitano** vya maendeleo ya nchi na jamii **(alama 5)**

(b) Taja na ueleze mbinu **nne** za kimtindo ambazo zimetumika katika kifungu **(alama 4)**

(a) Eleza jinsi washikadau mbalimbali wanavyoonyesha uwajibikaji kwa mujibu wa kifungu hiki. **(alama4)**

(g) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kulingana na muktadha wa matumizi yake kifunguni. **(alama 2)**

(i)ghawazi**……**

(ii) kupakwa mafuta viganjani**……..**

UFUPISHO (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kiswahili tunasema ni lugha yetu kwa sababu ndiyo lugha ya Kiafrika inayoongewa katika nchi nyingi Barani Afrika. Ni lugha yetu kwa sababu ni lugha asilia mojawapo za Afrika. Siyo lugha iliyoletwa na watu wa nchi za nje kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Uzuri wa Kiswahili sasa ni kuwa kimeenea kote Afrika Mashariki na Kati.

Wenyeji asilia waliokuwa wakiongea lugha hii tangu awali ni Waswahili. Waswahili hawa hata leo wako na wanaendelea kuitumia lugha hii kama lugha yao ya mama, kama vile Wakikuyu watumiavyo Kikikuyu, Wakamba, Kikamba na Wadigo lugha ya Kidigo. Makao yao Waswahili tangu jadi yanapatikana kaunti za Pwani. Makao yao yameanzia upande wa Kaskazini Mashariki mwa Kenya , na wanapakana na nchi ya Somalia huko. Wameenea katika upwa huo wa Pwani, ikiwemo Lamu, Malindi, Mombasa, Pemba, Unguja, Visiwa vya Ngazija na kuendelea.

Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi kulingana na sehemu wanamoishi. Kwa mfano, Waswahili wa Lamu huongea lahaja ya Kiswahili inayoitwa Kiamu. Waswahili wa Mombasa huongea lahaja ya Kimvita. Pemba wanaongea Kipemba, Ngazija lahaja ya Kingazija, Unguja lahaja ya Kiunguja na kadhalika. Kutokana na lahaja hizi na nyinginezo za Kiswahili ambazo hazikutajwa hapo, wataalamu wa lugha walitokea na Kiswahili sanifu. Hiki Kiswahili sanifu ndicho kitumiwacho katika mafunzo ya shule, uandishi wa vitabu na mawasiliano ya kiserikali na kibiashara.

Nchini Kenya, kwa muda mrefu Kiswahili hakikuthaminiwa kama Lugha ya Kiingereza. Sababu mojawapo ni kuwa Kiswahili hakikufanywa somo la lazima katika rasimu za shule, wala kutahiniwa katika shule za msingi. Hata katika shule za upili, katika kufunzwa na kutahiniwa hakikupewa umuhimu wowote. Kwa ajili hii wanafunzi wengi waliacha kujifunza Kiswahili kama somo. Hali hiyo ilifanya Kiswahili kuonekana kama lugha inayoongewa na wale watu wasio na kisomo ama elimu nyingi. Kwa ajili ya fikira hizi, watu wengi wamekuwa wakikichukia, kukidunisha na kujaribu kuongea Kiingereza kila nafasi inapojitokeza.

Miaka michache iliyopita, Kiswahili kilianza kutiliwa mkazo katika shughuli zote nchini Kenya. Kwa upande wa msimamo wa nchi lugha hii ilionekana yenye manufaa katika kuleta

umoja na kuwaunganisha wananchi wote. Jambo hili ni muhimu kwa maendeleo ya nchi iwayo yote. Umoja huleta maelewano na undugu. Hali hizi mbili zinapokuwapo, amani husambaa nchini mote.

Tukitazama mfumo wa elimu wa 8-4-4, Kiswahili kimepewa nafasi sawa katika ratiba za shule kama lugha ya Kiingereza. Kiswahili kinatahiniwa kama somo muhimu kuanzia shule ya msingi hadi shule ya upili. Kinyume na enzi za zamani, siku hizi mwanafunzi anayesoma Kiswahili, hata asipofaulu vizuri katika lugha ya Kingereza ana nafasi sawa ya kupata kazi kama wengine.

Maswali

a) Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno 80. (alama 6, utiririko 1)

Matayarisho

Jibu

b) Fupisha aya ya nne kwa maneno 40 **(alama 5, utiririko 1)**

Matayarisho

Jibu

c) Onyesha jinsi mtazamo kuhusu lugha ya Kiswahili ulivyobadilika (**maneno 50) (alama 4)**

Matayarisho

Jibu

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA **(Alama 40)**

(a) i) Unda neno lenye muundo ufuatao: **(alama 2)**

Irabu ya juu, nyuma + nazali ya ufizi, ghuna + kipasuo cha ufizi, ghuna + irabu ya chini, kati

ii) Kiyeyusho cha mdomo+ irabu ya juu tandazwa + kipua cha midomoni +irabu ya chini

b) Onyesha muundo wa silabi katika neno lifuatalo: **(alama 1)**

mchwa

(c) Tia shadda katika meneno yafuatayo kuonyesha dhana katika mabano: **(alama 2)**

i) Ala (kifaa)

ii) Ala! (kihisishi)

(d) Tunga sentensi katika wakati ujao hali ya mazoea. **(alama 2)**

(e) Andika sentensi ifuatayo katika udogo wingi **(alama 2)**

Nyundo za wazee wale zimevunjwa na mwana wake.

(f) Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha pekee chenye dhana ya **"badala ya"** katika ngeli ya U-**ZI.** **(alama 2)**

(g) Akifisha ili kuonyesha usemi halisi **(alama 2)**

tanya ondoka hapa mara moja

(h) Tunga sentensi ukitumia nomino dhahania inayotokana na kitenzi '**silimu**' **(alama 2)**

(i) Eleza matumizi ya mofimu **'ji'** katika sentensi zifuatazo: **(alama 2)**

(i) Sauti hiyo inajirudia.

(ii) Aliliua jitu hilo kwa mshale dhaifu.

(j) Bainisha sehemu za kiuamilifu za sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Aliwanunulia watoto mkate jana asubuhi.

(k) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Mwalimu aliniambia wataenda kwake kesho.

(l) Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya LI –YA **(alama2)**

(m) Chanaganua sentensi ifuatayo kwa kutumia mchoro wa matawi. **(alama 4)**

Huyu ndiye mwizi aliyewaibia watu pesa na atafikishwa mahakamani baadaye

(n) Tunga sentensi ukitumia kishazi tegemezi chenye dhana ya kielezi cha mahali. **(alama 2)**

(o) Kanusha **(alama 2)**

Mwamu wangu alinilea na kunielimisha.

(p) Andika sentensi ukitumia kitenzi **– cha** katika kauli ya kutendewa. **(alama 1)**

(q) Onyesha mofimu katika neno **(alama 3)**

Aliowapa

(r) Andika kitenzi kifuatacho katika hali iliyopo mabanoni **(alama 1)**

-ja (nafsi ya pili wingi)

(s) i) Kiri ni kwa kukana na _____ ni kwa nafuu. Na sifu ni kwa_____**(alama 1)**

ii) _____ ni kwa kukubaliana na jambo , simile ni kutaka kitu kinusurike na hongera ni _____. **(alama 1)**

(t) Tunga sentensi mojakuonyesha maana tofauti za neno **'ua'** **(alama 2)**

4. ISIMU JAMII

" Maafisa 3 wakana kusaidia mshukiwa wa mauwaji ya watoto kutoroka kituoni.

Maafisa watatu wa polisi jana walikana mashtaka ya kumsaidia mshukiwa wa mauaji ya watoto 13 kutoroka kutoka kituo cha polisi…**"**

(a) Huku ukitoa sababu mbili, tambua sajili hii. **(alama 3)**

(b) Fafanua sifa zozote saba za sajili hii. **(alama 7)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA KWANZA)

KISWAHILI

102/3

KARATASI YA 3

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Andika jina lako na nambari yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

b) *Tia sahihi kisha uandike tarehe*

c) *Jibu maswali **manne** pekee*

d) *Swali la kwanza ni la lazima*

e) *Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Tamthilia, Riwaya, Ushairi na Hadithi Fupi*

f) *Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja*

g) *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU A: TAMTHILIA ;P. Kea: *Bembea ya Maisha*

1. LAZIMA

Maji yangekuwa yamewafika shingo basi wangeshindwa kuishi pamoja, Ndoa ni bembea,kuna wakati itakuwa juu na wakati itakuwa chini. Hizo juu-chini chini-juu ndizo utamu wake. Ni kama maisha kwa jumla. Yana pandashuka ndiyo lakini pandashuka hizo ndizo hutupa kuridhika hatimaye tunapozishinda. Maisha yangekuwaje bila hali kubadilika?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Tambua mbinu **nne** za kimtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

c) Kwa kurejelea tamthilia nzima fafanua pandashuka walizopitia wahusika mbalimbali**.(alama 7)**

d) Kwa hoja tano, jadili umuhimu wa mbinu rejeshi kama ilivyotumiwa katika tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama 5)**

SEHEMU B: RIWAYA;Clara Momanyi: *Nguu za Jadi*

Jibu swali la 2 au la 3

2. … alijitoma kwenye mabanda hayo yaliyosaki walevi nyakati hizi za jioni. Kelele zilizokuwa humo zingeweza kumtia mtu kichaa. Wengine waliimba ilhali wengine walipaaza sauti hata hungesikia walichosema. Baadhi yao nishai za ulevi ziliwapanda. Wakawa wanacheza kwa miondoko mbalimbali isiyoenda sambamba na nyimbo za santuri. Kuna baadhi ambao walikuwa wakilia na kutiririkwa na machozi bila kujua kilichowaliza. Hapa na pale kuna waliomkonyezea… na kumpigia mbinja… Alijifanya hawaoni ilmradi akamilishe usakaji wake. Alihisi kinyaa, akatamani apakimbie pahali pale. Lakini hakuwa ametimiza lililompeleka huko. Alihiari kuyapitia yote bora ampate aliyemtafuta.

a) Changanua mtindo kwenye kifungu hiki. **(alama 5)**

b) Ukirejelea dondoo hili, dondoa sifa zozote tano na mrejelewa. **(alama 5)**

c) "Maisha ya mrejelewa yalijaa kinyaa na mateso." Jazili mikakati aliyotumia kukabiliana na hali hii. **(alama 10)**

au

3. a) "Ukosefu wa malezi bora una athari kwa jamii." Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya Nguu za Jadi. **(alama 8)**

b) "Ai! **Faragha ya nyani imeishia ngokoni**. Sasa wanafanya nini hawa hapa saa hizi?" Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari ukirejelea riwaya nzima. **(alama 12)**

SEHEMU C: HADITHI FUPI

D.W. Lutomia na P. Muthama (wah.): *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

Jibu swali la 4 au las 5

4. R. Wangari: Fadhila za Punda

"Nia yangu ni nyeupe kama pamba. Mimi si miongoni mwa wale wanaume wenye nia ya kuharibu watoto wa watu. Kusudi langu halali."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

b) Bainisha mbinu mbili zinazoweza kutumiwa kutambua sifa za msemaji wa dondoo hili.**(alama4)**
c) Fafanua kinyume kinachojitokeza katika dondoo hili kwa kurejelea hadithi "Fadhila za Punda."
(alama12)

5. a) Fafanua matarajio ya jamii kuhusu 'mke mwema' kwa mujibu wa hadithi "Nipe Nafasi."
(alama12)

b) "… Alikuwa kashaonja mrututu wa maisha na kugundua kuwa dunia haina huruma…"
Kwa hoja nane thibitisha kuwa dunia haina huruma kwa kurejelea hadithi "Kifo cha Suluhu."
(alama8)

SEHEMU YA D: USHAIRI
JIBU SWALI 6 au 7

6. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.*

Mwalimu ndiye kiwanda, binadamu malighafi
Kikipewa kinaunda, hakipigiwi makofi
Siku zote za kalenda, chaondowa ukorofi
Nakushukuru mwalimu, kunifanya niwe mtu

Hizi bondo safisafi, ndiyo kazi yake nani?
Waja wenye roho safi, wasochoka kuauni
Ni kaziye mtu safi, ya mwalimu darasani
Nakushukuru mwalimu, kunifanya niwe mtu

Watu wote mashuhuri,ni mikono ya mwalimu
Kwa ofisi nzurinzuri,waloiva tarakimu
Aleaye kwa uzuri,namba wani ni mwalimu
Nakushukuru mwalimu, kunifanya niwe mtu
Lugha unatufundisha, kwa kunena hutokwama
Masayansi afundisha, maabara tunapima
Maadili kifundisha, watu wengi wawa wema
Nakushukuru mwalimu, kunifanya niwe mtu

Asubuhi wanamsha, akili kunizindua
Kwa maswali nakuchosha, we huchoki kubukua
Kwa tabia nakuchosha, mwalimu wanikosoa
Nakushukuru mwalimu, kunifanya niwe mtu

Sipokuwa darasani, ni mawazo unapanga
Uwapo kule nyumbani, mikakati unapanga
Barabara na shambani, unasema na kupanga
Nakushukuru mwalimu, kunifanya niwe mtu

Cha kulipwa ki kidogo, hujalipwa vya kutosha
Hustahiki kidogo, kazi yako inatosha
Walipwaje ndogondogo, na kaziyo inachosha?
Nakushukuru mwalimu, kunifanya niwe mtu

U kiumbe wa ajabu, mfanowe sijapata
Na busara za kibabu,'toka kwako nazipata
Wenye vinywa na mabubu, ya mwalimu wanadata
Nakushukuru mwalimu, kunifanya niwe mtu

Maswali

a) Tambua aina ya shairi hili.Toa sababu yako. **(alama2)**
b) Kwa kutoa idhibati tambua nafsineni katika shairi hili. **(alama 2)**
c) Eleza sifa **tatu** za nafsi nenewa katika shairi. **(alama 3)**
d) Thibitisha kuwa nafsinenewa amefaulu katika jukumu lake. **(alama 1)**
e) Kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo tambua bahari za shairi hili. **(alama 2)**
i)Vipande
ii)vina
f) Fafanua aina **mbili** za toni katika shairi hili. **(alama2)**
g) Kwa kutolea mifano ,fafanua mbinu mshairi alizotumia ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. **(alama2)**
h) Fafanua mbinu **mbili** za kimtindo zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama2)**
i) Andika ubeti wa **saba** kwa lugha nathari. **(alama 4)**

au

7. Nitafakaripo kwa tuo
Moyo hunitweta na mtetemo kunivaa
Wanijiapo na tabasamu
Ambazo hulinyonga tumaini langu
Ninahuzunika.

Wanisalimiapo kwa mikono miwili
Na chini kuniinamia
Wakiyakoleza yao matamshi
"mzee…ndugu…salama!salama!"

Nachukia zao nyendo
Wanadai kwa muhemko
'lazima tungo kutetea wanyonge'
Lakini nitazamapo,wenyewe hawasiti
Mnyonge mkononi kumtia.

Na kwa maguvu kumfikicha
Haki yake kumhini
Mtetezi kumhini
Mtetezi kufaidi
Wote hawa sioni tofauti
Wote hawa sawa
Na mwanasiasa mwehu
Ni moto wa jicho
Wanapotabasamu nachelea kuridhia
Hutabasamu wadhamiriapo vingine
Tabasamu zao ni ishara ya maangamizi.

Wanipangiayo kimoyomoyo,kimyakimya
Wakafurahia kutatarika kwangu
Kwenye tanuri hii ya maisha.

Maswali

a) Thibitisha shairi hili la kimapinduzi kwa kutumia hoja mbili. **(alama 2)**

b) Fafanua aina nne za taswira katika shairi hili. **(alama 4)**

c) Tambua aina tatu za urudiaji katika shairi hili . **(alama 3)**

d) Onyesha matumizi ya mbinu zifuatazo za kimtindo; **(alama 4)**

i) Usambamba

ii) Sitiari

iii) Kinaya

iv) Uhuishi

e) Fafanua mbinu zilizotumiwa na mshairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi **(alama3)**

f) Onyesha matumizi mawili ya mishororo mishata katika shairi hili. **(alama 2)**

g) Thibitisha kuwepo kwa usaliti katika shairi hili. **(alama2)**

SEHEMU YA E-FASIHI SIMULIZI

8. *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Bembo,Bembo…
Mtoto yu matatani
Anataka mama yake
Na mama kaondoka kutafuta mayai
Naye kuku katoroka
Asijikute chunguni

Bembo, Bembo
Mtafute mwenye mtama
Mwenye mtama hapatikani
Naye amevunja kijiti
Nacho kinatakikana
Ili kumponda nyoka

Bembo,Bembo…
Utamwuaje nyoka
Ili naye mwenye mtama
Akaingia kwenye pori
Akatafute hicho kijiti
Na kumwondokea kuku

Bembo ,Bembo
Ukishamwua nyoka
Mwenye mtama kwenye pori
Akakitafute kijiti
Naye akiwa porini
Kuku wetu atarudi

Bembo,Bembo
Kuku wetu akirudi
Kuku atataga yai
Naye mama atarudi
Achukue na mayai
Akampe mtoto wake.

Maswali

a) Tambua aina ya wimbo huu. **(alama 1)**

b) Eleza sifa **mbili** za kipera ulichokitambua. **(alama 2)**

c) Eleza mikakati ambayo mwasilishaji wa utungo huu angetumia ili kufanikisha uwasilishaji wake. **(alama 5)**

e) Eleza sifa nne zitakazopotea wimbo huu ukiandikwa badala ya kuimbwa. **(alama4)**

e) Unatazamia kufanya utafiti wa aina hii ya nyimbo kwa njia ya kushiriki,fafanua udhaifu wa mbinu hii. **(alama 4)**

f) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika ulimwengu wa sasa. Pendekeza njia **nne** za kuhakikisha hazipotei. **(alama4)**

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA PILI)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani.*
b) *Tia sahihi yako kasha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Andika insha mbili*
d) *Swali la kwanza ni la lazima*
e) *Kasha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizoakia.*
f) *Kila insha isipungue maneno 400.*
g) *Kila insha ina alama 20*
h) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
JUMLA	40	

1. **LAZIMA**

Wewe ni mhariri wa gazeti la Angaza. Andika tahariri kuhusu umuhimu wa wanafunzi kushiriki katika michezo na masomo mengine yasiyokuwa ya kiakademia.

2. Maovu ya kijamii yamekithiri sana miongoni mwa vijana. Eleza chanzo na upendekeze hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kusitisha maovu haya.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha matumizi methali ifuatayo:

Jifya moja haliinjiki chungu

4. Andika kisa kinachoanza kwa maneno haya.

"Umeletwa hapa na wasamaria wema." Sauti ikanieleza. Nikavuta kumbukizi**i……**

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO KUPIGWA CHAPA!

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA PILI)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) Andika *jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) Tia *sahihi yako na kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali yote.*

d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

e) *Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya* ***Kiswahili.***

Kwa matumizi ya Mtahini Pekee :

SWALI	UPEO	ALAMA
1. Ufahamu	15	
2. Muhtasari	15	
3. Matumizi ya Lugha	40	
4. Isimu Jamii	10	
JUMLA	80	

1. Ufahamu **(Alama 15)**

Soma makala halafu ujibu maswali yanayofuatia.

Leo Mwalimu Bidii amerauka kama ada yake kwa ajili ya kutekeleza wajibu wake kwa wanafunzi wake Shuleni Mwera. Anaelewa barabara kwamba mchapuko wa ghafla wa gonjwa la korona kule Uchina, ulitikisa na kuvuruga dunia nzima katika nyanja zote za maisha ya binadamu. Miongoni mwa nyanja zilizoathiriwa zaidi ni elimu ambayo huongoza nyanja zingine za maisha. Awali, taasisi zote za elimu zilifungwa kama hatua muhimu ya kudhibiti msambao wa uwele huu. Baadaye afueni ilipodhihiri, na ushauri kutolewa na wataalamu wa afya, mataifa mbalimbali yalibuni taratibu za kurejelewa kwa shughuli za masomo katika taasisi zote. Labda marejeleo haya hayakuwa na ugumu kama ilivyokuwa namna ya kufidia na kurejelewa kwa mfumo wa kawaida shuleni. Naam, mwiba uchomeapo ndipo utolewapo na tiba mjarabu ni ile itokayo kwa mwele mwenyewe. Wizara ya elimu nchini iliratibu mihula upya na kuvuruga mazoea. Hii ni hatua iliyowasababishia **bughudha** washikadau wote; sio walimu, wazazi, wauzaji na wanafunzi. Sijui mizani gani iliyotumiwa kupima, lakini watu wengi walihisi kwamba ni walimu waliokumbwa na usumbufu mkubwa zaidi.

Iliwabidi walimu wafaragueue na kuongeza ubunifu wao ili kukamilisha mitaala ya masomo katika muda mfupi kuliko ule ulioratibiwa na wakuzaji mitaala. Mathalani, vipindi vilianza mapema kuliko kawaida yake na kuendelea hadi kupita saa kumi jioni na kuzima michezo ya baada ya madarasa. Mwalimu Bidii hakuwa na budi ila kujitoma ndani ya kinyang'anyiro hiki kwa vile hakupenda kuachwa nyuma. Hii ndiyo sababu ilimfanya kurauka kila siku. Lakini leo matarajio yake ya kuwahi kipindi cha saa kumi na mbili alfajiri yanaelekea kuyeyuka na kutokomea mithili ya theluji inavyoyeyuka na kugeuka kuwa maji yanayateremka kutoka milimani kufaidi walio mabondeni na kuviacha vileleta vya milima na kiu. Usiku uliopita ilikunya kidindia ungedhani ilikuwa mashindanoni. Barabara iliyotamani kutiwa sakafu tangu nchi ijinyakulie uhuru hadi sasa ikanyonya, ikameza na kutapika maji yakaloa kote. Wajuao chuku ya lugha walisema kilichozaliwa barabarani kilikuwa mama ya tope wala sio tope tu. Tazamo hili lilikejeli ile pikipiki aina ya 'Honda' aliyokuwa ameitumia Mwalimu Bidii kwa miongo miwili u nusu sasa – pikipiki aliyonunua baada ya kuomba mkopo kutoka kwenye chama cha ushirika cha akiba na mikopo baada ya miaka mitatu ya ajira. Ilimchukua miaka mitano kulipia mkopo wake.

Ilikuwa dhahiri tangu aiguse barabara hii kwamba alikuwa anajenga nyumba ya karata. Utelezi wa barabarani uliongezwa na magurudumu yaliyolika meno na kubwagwa chini halikuwa tukio lililokuwa ng'ambo ya utendekaji kamwe. Mara mojamoja ilimbidi Mwalimu Bidii kusalimu amri. Si hoja kwamba hakupiga hatua za maana kupunguza kitalifa cha kilomita kumi baina ya shule na nyumba yake ya kukodisha. Muda huu wote manyunyu ya mvua yalikuwa yanaendelea kudondoka ni kama yalikuwa na kinyongo na mzalendo huyu **aliyejitolea sabili** kuhudumia nchi yake. Alizidi kupambana akihema kama punda aliyebandikwa mzigo uliozidi uwezo wake akijaribu kuelekeza chombo chake **kisiende pewa** topeni. Kwa kweli hakuenda popote heri ule mfano wa simulizi ya Sofokile kumhusu mbingirisha mwamba kuupandisha kwenye mlima ulioteleza. Ingawa alishindwa kuukwea mlima, angaa angerudi nyuma sio kama mwalimu. Mwalimu alisakamwa kabisa; mbele na nyuma hakukuendeka!

Mbele yake kidogo alimwona mtu aliyemjua akiwa amevua viatu na kuvishika mikononi ili alikabili tope barabarani. Huyu alikuwa afisa wa maabara kwenye Zahanati ya Nafuu iliyokuwa karibu na Shule ya Mwera. Muala Mutia alipambana na hali yake bila kutazama nyuma aone dhiki alizokuwa anapitia mwalimu. Aliogopa kuchelewa kupokezwa zamu na mwenzake aliyehudumu usiku huo. Hakupenda nuksani za asubuhi ambazo Kechi angemzulia lau angechelewa hata kwa dakika chache tu. Kechi alikuwa mbali sana na ungwana na wenzake kazini waliepuka kumkorofisha kwani hakuna neno ambalo ulimi wake haungelitaja faraghani na hadharani. **Hakuwa na kaba ya ulimi**. Kama alikuwa na marafiki, achana na wandani, hawakujulikana pale zahanatini. Mutia aliambaa shari ili imwambae. Lakini leo ilikuwa muhali kwani hangeweza kukamilisha umbali wa kilomita tisa kwa miguu katika nusu saa iliyosalia kabla ya muda wa kupokezwa zamu. Na hakika lisilo budi mja muungwana hupatana nalo wala hapingani nalo.

Hatua kadhaa mbele yake alimpata yule mchuuzi anayewasambazia maziwa zahanatini amebwagwa chini na pikipiki yake na mitungi ikafunguka na kurembesha barabara kwa maziwa yaliyokuwamo. Kiplimo, jamaa aliyestawisha kilimo cha ufugaji katika Kijiji cha Kaplel, leo ameambulia hasara. Atarejea nyumbani mikono mitupu. Alisakama pale matopeni hadi Mutia alipomfikia na kuinua pikipiki iliyokuwa imeumbana mguu wake wa kulia asitoke.

"Hawa viongozi wetu wanahujumu maendeleo yetu kabisa! Mbona miaka hii yote barabara hii haijabandikwa lami?" Kiplimo akamaka baada ya kusimama.

Mutia akamkumbusha, "Lakini si ni nyinyi mna mazoea ya kukubali visenti vichache wakati wa uchaguzi ili kuwachagua wanafiki hawa? Kisha kuna wengine ambao husema 'Tunachagua mtu wetu', 'mtu wetu' ambaye sasa hana mwao kuhusu kero tunazopitia! Na wengine kama yule jirani yetu upande wa kusini haendi kupiga kura akidai kuwa kura yake moja haiwezi kuleta tofauti yoyote. Ni janga tumelichuma wakati wa uchaguzi sasa tuvumilie kulila. Wajua tangu kale, mwiba wa kujidunga huambiwi pole."

Mwalimu Bidii naye, baada ya kughairi nia, alikuwa ameegesha 'Honda' yake kando ya kigingi cha ua uliozingira shamba la yule mkwasi ambaye wengi hawakumjua ila walimsikia tu, akawa anamfuata Mutia akitumainia usaidizi wake. Alipowakaribia na kusikia malumbano yao, akatupa nukuu aliyowahi kuisikia kwa mtu asiyemkumbuka, "*Choices have consequences*!" Wale wawili wakaitikia kama ngonjera, "Ni kweli mwalimu!"

MASWALI

a) Mikakati ya kukamilisha mitaala ya masomo iliwaathiri washikadau kwa namna mbalimbali. Taja athari **tatu** kwa wanafunzi**.** **(alama 3)**

b) Orodhesha changamoto **nne** zinazowatanza wahusika katika kutekeleza shughuli zao katika makala haya. **(alama 4)**

c) Thibitisha ukweli wa kauli kwamba 'uamuzi una athari zake' kwa kurejelea matukio **matatu** kuwahusu wananchi kama inavyosimuliwa katika kifungu hiki**.** **(alama 3)**

d) Nakili kisawe cha '**bughudha**' kutoka kifunguni**.** **(alama 1)**

e) Andika visawe vya nahau zifuatazo**:** **(alama 2)**

(i) aliyejitolea sabili **……**

(ii) kisiende pewa **……**

f) (i) Bila kukanusha, eleza maana ya '**Hakuwa na kaba ya ulimi.'** **(alama 1)**

g) Andika methali moja inayoasa kuhusu ulimi**.** **(alama 1)**

2. Ufupisho **(Alama 15)**

Fupisha kifungu hiki kulingana maagizo yanayotolewa mwishoni mwake.

Katika karne ya kumi na tisa bara la Afrika lilivamiwa na nchi za Ulaya kama vile Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Ubelgiji, Italia, Ureno na kadhalika na kutwaliwa. Uingiliaji huu haukuhusu Afrika pekee bali mataifa mengine katika ule ulioitwa ulimwengu usiostaarabika kama India. Kwa mujibu wa wanahistoria, Uingereza ndilo taifa lililojitwalia idadi kubwa ya nchi za ulimwengu chini ya mfumo wa kiutawala ulioitwa ukoloni labda kwa sababu kwamba Uingereza ni taifa lililokuwa limefikia ustawi mkubwa katika Ulaya nzima wakati huo. Bila shaka huu ulikuwa muktadha uliostahili matumizi ya usemi kuwa mwenye nguvu hupishwa na mataifa mengine ya Ulaya hayakuwa na budi ila kuipisha Uingereza ijilimbikizie mataifa ya ulimwengu na kuyaweka chini ya kwapa zake. Jambo lingine lililoiwezesha Uingereza kuyapiku mataifa mengine ya Ulaya katika kujipakulia koloni ulimwenguni ni kwamba Waingereza walitakadamu katika uvumbuzi wa vyombo vya usafiri wa majini na kwa hivyo waliweza kuzuru nchi za ulimwengu kwa wepesi zaidi na katika kipindi kifupi. Licha ya Uingereza kuwa katika nafasi bora ya kutwaa koloni ulimwenguni, mataifa mengine ya Ulaya hayakusubiri kugawiwa bali hayo pia yaling'ang'ania kumega sehemu fulani ya koloni. Huu mng'ang'anio ulikuwa kinyang'anyiro halisi ambacho kilimithilishwa na watu wanaogawana kipande cha mkate au nyama; kila mmoja akijikatia kadiri ya uwezo wake na makali ya kisu chake.

Uvamizi huu ulidhihirika kupitia utwaliwaji wa mamlaka ya kiutawala katika mataifa yaliyoathiriwa na kuwekwa chini ya himaya ya taifa husika kutoka Ulaya. Mtindo huu ulikinzana na tawala asilia za jamii mbalimbali za Kiafrika zilizokuwa na falme zao ambazo zilisambaratishwa baada ya kuangikwa kwa bendera ya taifa husika kutoka Ulaya. Hakukuwa na fursa ya kutathmini namna kila jamii katika kila eneo ilivyoendesha serikali yake chini ya viongozi wao mbalimbali. Usishangae kusikia kwamba Wazungu wengi waliipuuzilia mbali hii mifumo ya kiutawala au hata kudai kwamba wenyeji hawakuwa na mfumo wowote wa kujitawala. Uhasama uliokuwepo baina ya jamii tofauti pamoja na upekee wa mila na tamaduni zao zingine, ni mambo yaliyoangaziwa kwa kurunzi kali zaidi na kupuuza ukweli kwamba Waafrika walikuwa na mifumo mbalimbali ya kujiongoza.

Bara la Afrika lilikatwakatwa katika vipande mbalimbali na kugawiwa mataifa tofautitofauti ya Ulaya. Walibuni mipaka kiholela na kuwatenganisha watu wa jamii moja wakajipata kwenye nchi mbili tofauti. Si ajabu kwamba hata katika visa vya kidhalimu watu wa familia moja walitenganishwa kwa kuwekwa katika nchi mbili tofauti. Aidha, hata watu wa ukoo mmoja walitawanywa kimakusudi na kupelekwa katika maeneo mengine ya kijiografia yaliyoitwa nchi. Kadhalika, hata kuna maboma ambayo yalipigwa mpaka katikati na kumega sehemu moja kuitupa katika nchi

tofauti na nyingine. Na kwa kweli asiyekujua hakudhamini. Watu walioathirika na tendo hili la kiholela waliona ugumu mkubwa kutii mipaka ya aina hii na kunao waliokaidi mipaka na kuendelea kutagusana na kutangamana na jamaa zao kokote walikopelekwa.

Tahakiki za wanahistoria hudai kwamba uvamizi wa Wazungu katika bara la Afrika, kwa kiwango cha juu zaidi uliletwa na msukumo wa kutaka kunyakua maliasili kochokocho iliyojaa katika maeneo mengi. Madini kama chuma, makaa, shaba, almasi, dhahabu na mengine mengi yalijaa tele na viwanda vilivyokuwa vimestawishwa kutokana na Mageuzi ya Kiwanda ya Karne ya 19 vilihitaji malighafi na madini kwa wingi. Afrika illikuwa na hazina ya hiyo malighafi na ilifaa kutwaliwa bila pingamizi. Njia ya pekee ya kujihakikishia kuwepo mfululizo kwa bidhaa hii ilikuwa kuziweka nchi hizi chini ya himaya za serikali zao za Ulaya. Sina shaka walielewa msemo kwamba pavumapo palilie nao wageni wavamizi iliwabidi walilie bara lenye maliasili nyingi sana.

Licha ya majilio ya Wazungu barani Afrika kuangaziwa kwa uhasi, ni kweli kwamba kuna mambo mengi mazuri ambayo hayangetokea lau hawangalikuja. Ustawishaji wa miundomsingi, hasa njia, uliwezesha maeneo ya ndani kufikiwa bila bughudha nyingi. Ikumbukwe kwamba njia ya reli ya Kenya – Uganda, iliyojengwa mwanzoni mwa karne ya ishirini ilirahisisha kufanywa kwa shughuli katika maeneo ya ndani ya nchi. Kuna taasisi za matibabu, shule na vyuo vya mafunzo anuai katika taaluma mbalimbali vilivyojengwa na wakoloni. Hata viongozi wa kwanza baada ya nchi hizi kurejeshewa utawala wao, walisomea kwenye taasisi hizi. Mgala muue na haki yake mpe kwani ni stahili yake.

Maswali

a) Kwa maneno kati ya 80 – 90, andika hoja muhimu katika **aya mbili za kwanza**. **(alama 8)**

Matayarisho

Nakala safi

b) Fupisha aya za **tatu, nne** na **tano** ukizingatia athari hasi za ukoloni, kichocheo cha chake na manufaa ya ukoloni barani Afrika. (maneno 50**)** **(alama 6)**

Matayarisho

Nakala safi

3. Matumizi ya Lugha **(Alama 40)**

a) Andika maneno yenye vitamkwa vya sifa zifuatazo**:** **(alama 2)**

(i) kikwamizwa sighuna cha kaakaa gumu, irabu ya nyuma juu, kikwamizwa ghuna cha kaakaa laini, irabu ya nyuma juu, kilainisho na irabu ya mbele juu

(ii) nazali ya midomoni, irabu ya mbele kati, nazali ya ufizini na irabu ya nyuma wastani

b) Taja sifa zinazoonyesha usawa baina ya kila jozi ya sauti hizi**.** **(alama 1)**

(i) /m/ na /w/ ……

(ii) /t/ na /ch/ ……

c) Eleza maana **mbili** zilizo katika sentensi**:** **(alama 2)**

Usijadili mtihani unaoendelea wakati huu.

d) Tumia wingi kuandika sentensi zifuatazo.

(i) Mkulima alilima ucheu ili kujiandaa kwa msimu wa upanzi wa nafaka**.** **(alama 1)**

(ii) Shauri lake liliniepusha na janga la uwele hatari unaosambaa haraka**.** **(alama 1)**

e) Onyesha katika sentensi **moja** matumizi **mawili** ya ritifaa (‘) katika lugha. **(alama 2)**

f) Zingatia maagizo katika mabano mwishoni mwa kila sentensi kuziandika upya.

(i) Wangia alipata mafunzo murua chuoni. Wangia ni stadi katika Kifaransa.

(Unganisha ukianzia: Mafunzo…) **(alama 2)**

(ii) Sherehe nyingi zilifanywa ili kuadhimisha ushindi wa Pute. (Tumia vitenzijina badala ya maneno yaliyopigiwa mistari**.)** **(alama 2)**

(iii) Mari alinunua simutamba mpya kwa shilingi elfu kumi na kumtunza mwanafunzi bora.

(Anza na shamirisho ala**.)** **(alama 2)**

g) Ainisha mofimu katika maneno yafuatayo:

(i) katika (kitenzi) **…….. (alama 1)**

(ii) achaguliwaye **…… (alama 2)**

h) Tunga mfano **mojamoja** wa sentensi kwa kila muundo.

(i) S - KN (Ɵ)+KT(Ts+T+H+N**)** **(alama 1)**

(ii) S - KN (W+V)+KT(t+N+V) **(alama 2)**

i) Bainisha kiima, kiarifu na chagizo katika sentensi hii. **(alama 3)**

Mhandisi shupavu atakagua ujenzi wa ghorofa hatua kwa hatua.

j) Eleza matumizi ya kiambishi **-o** katika sentensi ifuatayo**:** **(alama 1)**

Waliofanikiwa walifanya makadirio mazuri.

k) Ainisha nomino katika sentensi hii: **(alama 2)**

Mashabiki wengi walipiga vigelegele Kocha Manoa alipowapa maji.

l) Vishazi tegemezi vina dhima za kivumishi na kielezi. Tunga sentensi **mojamoja** kuonyesha kila dhima**.** **(alama 2)**

(i) kivumishi: **……..**

(ii) kielezi: **……..**

m) Onyesha maana **mbili** za neno ‘**bunda**’ kwa kutungia sentensi **mbili** tofauti. (**alama 2)**

n) Kwa kutumia sentensi **moja**, onyesha miundo **miwili** ya virai husishi**.** **(alama 2)**

o) Akifisha.

siku ya kiswahili duniani iliadhimishwa na wengi ilifana **(alama 2)**

p) Jaza mapengo kwa maneno yanayostahili. **(alama 2)**

Kinza ni kwa pinga na tambua ni kwa …….. ilhali nata ni kwa ……

r) Onyesha katika sentensi maana ya nahau: '**shika shokoa**'**.** **(alama 1)**

s) Kasura aligundua kwamba Ogina alikuwa na uwezo mwingi wa kukabili Somo la Hisabati na akaamua kwenda mara kwa mara kupewa ushauri na Ogina hata akaimarika. Taja methali inayoweza kutumiwa kuafiki muktadha wa Kasura**.** **(alama 1)**

t) Kwa kuzingatia dhamira, sentensi ifuatayo inaweza kuwa katika **aina mbili**. Zitaje. **(alama 1)**

Mkiondoka wawiliwawili, mtafika haraka.

4. Isimujamii **(Alama 10)**

a) Eleza sifa **tano** za lugha ambayo wewe kama mnyapara wa kiwanda cha kusaga miwa cha Kimatuni utatumia ukiwahutubia wafanyakazi walio chini yako**.** **(alama 5)**

b) *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.* **(alama 5)**

"Polepole, Mama Mercy! Unajua si kupenda kwangu. Tena si hali itakayodumu milele. Baada ya siku chache tu, tutakuwa tumekamilisha mradi huo wenye dharura. Kisha tutakuwa na muda wa kila kitu. Hili, Mama Mercy, ni kile tunaita *bad coincidence*… nimebanwa na kazi. Unanielewa **…?**

"Dadii…njaa…sana!"

Fafanua sifa **tano** za lugha inayotumika katika huu muktadha wa familia**.** **(alama 5)**

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO KUPIGWA CHAPA!

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA PILI)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika jina lako, nambari ya usajili, mkondo, sahihi na tarehe katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*

c) *Swali la kwanza ni la* ***lazima****.*

d) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.*

e) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

f) ***Maswali yote ni sharti yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	80	

SEHEMU YA 'A' - FASIHI SIMULIZI.

Swali la lazima

1. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.

Ndimi kisoa,dume wa ukoo mtukufu
Uliojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hatari wa ngoma
Ndimi dume lililoingia nyanjani
Makoo yakatetemka
Yakang'ang'ania ,gozi kusakata nami

Kijiji kizima kilinijua
Wazee walinienzi
Wakamiminika kiamboni
Mabuti kunikabidhi

Maswali

a. Bainisha kipera hiki. **{alama2]**

b. Eleza sifa zozote tano zinazotambulisha kipera hiki**.** **[alama5]**

c. Fafanua shughuli mbili za kijamii wanayoshiriki jamii hii. **[alama4]**

d. Tambua toni inayojitokeza katika utungo huu. **[alama2]**

e. Eleza namna wanajamii wanavyoweza kutunza utungo huu miongoni mwa tungo nyingine za fasihi hii zisififie. **[alama7]**

SEHEMU YA 'B' – RIWAYA.

Nguu Za Jadi – Clara Momanyi

Jibu ama swali la 2 au la 3

2. "Mimi ni mwanamume .Ninaweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake. Mwanamke akishaolewa, basi yake yamekwisha hapo. Azae na kuitumikia jamaa yake bila kuulizauliza maswali.

Maswali

a. Weka dondoo hili katika muktadha wake**.** **[alama 4]**

b. Eleza sifa nne za msemewa wa maneno haya**.** **[alama 4]**

c. Eleza jinsi mnenewa alivyoitumikia jamii yake. **[alama 6]**

d. Jadili maudhui matatu yanayojitokeza kwenye dondoo hili. **[alama 6]**

3. (a) **Changanua mitindo katika kifungu hiki.** **[alama10]**

Toka mbele yangu. Kwenda! Waketwa ni watu wasio na akili hata ya kuchagua wachumba. Ndivyo maana daima mnabaki nyuma kama makoti.Hata sijui kwa nini nilikuajiri. Umenivunjia heshima kumkataa rafiki yangu. Toka! Chifu Mshabaha alimfukuza Mngwasha kutoka afisini mwake. Kwa muda, Mangwasha hakujua kwa nini chifu mshabaha alimkaripia kiasi hicho. Alifululiza hadi kwake nyumbani. Alijifungia chumbani akalia kwa kwikwi. Alidhani chifu yule

tayari alikwisha kumpiga kalamu. Hangeweza kumfukuza vile kisha amtake kurudi kazini. Alihisi kwamba Maisha ya uchochole sasa yanamkodolea macho. Aende wapi kwingine? Kazi hiyo ilimkidhia lishe na mavazi. Sasa angeshika mti gani?

(b) Wakati jamii inapojitahidi na kupiga hatua,kuna watu ambao huwaendea wenzao kinyume. Jadili kwa hoja kumi ukerejelea riwaya nguu za jadi. **{alama 10]**

SEHEMU YA 'C' - TAMTHILIA

Bembea ya maisha – Arege Timothy.

Jibu ama swali la 4 au la 5

4. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi. Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi ya kutisha. Maisha yetu ni mfano wa mbegu iliyopandwa. Mbegu hiyo haina budi kuoza kwanza ndipo ioteshe mche upendezao. Mche huo wa asili ya mbegu iliyooza, hatimaye hutoa zao la mbegu nyingi ajabu. Ukitazama vizuri, mbegu ile haifi bali huchukua mkondo mwingine wa Maisha.Huchukua umbo jipya lipendelezalo hasa ikiwa itakuwa imeangukia ardhi nzuri.Hapa kijijini japo yapo mawili matatu ya kusinya, ardhi yake si mbaya.

Maswali

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **[alama 4]**

(b) Fafanua ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kurejelea hoja kumi kwenye tamthilia nzima**.** **[alama10]**

(c) Bainisha mbinu za kimtindo zinazojitokeza katika kifungu hiki. **[alama 6]**

5. Jadili namna maudhui ya usaliti yanavyojitokeza katika tamthilia bembea ya Maisha. **[alama20]**

SEHEMU YA 'D' - HADITHI FUPI

Jibu ama swali la 6 au la 7.

6. "Nitafanyaje nifike shuleni kabla ya saa mbili asubuhi? Kitafanyika nini nikifika katika ukumbi huu baada ya mtihani kuanza?

(a) Fafanua muktadha wa dondoo. **[alama 4]**

(b) Fafanua sifa za msemaji wa maneno haya. **[alama 4]**

(c) Bainisha toni inayojitokeza katika dondoo hili. **[alama 2]**

(d) Eleza maudhui ya elimu yalivyoshughulikiwa katika hadithi hii. **[alama10]**

7. "Wafanya nini hapa wewe?"

"Sikujua nilihitaji miadi kumwona mume wangu"

Maswali

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **[alama 4]**

(b) Bainisha umuhimu wa anayeulizwa swali katika dondoo hili. **[alama 6]**

(c) Taja toni inayojitokeza katika dondoo hili. **[alama 2]**

(d) Jadili namna 'uvundo"unavyojitokeza katika jamii ukirejelea hadithi hii. **[alama 8]**

SEHEMU YA 'D' – USHAIRI

8. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

Pana jambo inatukiya, kwangu hilo ni muhali
Kitenda naona haya, kujishusha yangu hali
Sipendi unupe hidaya, sipendi kutenda hili
Sipendi mimi kucheka

Sipendi mimi kucheka, kucheka mawi
Sipendi na ya dhihaka, kwangu nyemi hiwi
Sipendi kwa hakika, mwovu kistawika

Halufaye ninacheka!
Maskini akiteswa
Yatima akinyanyaswa
Mnyonge naye akinyonywa
Sipendi hata ikiwa
Unazo nguvu ikiwa
Unazo nguvu najuwa
Na hili sitatekezwa

Mbona lakini nicheke,kwayo furaha?
Na wewe ukajiweke, uli na siha?
Na yatima ali pweke, uli na siha?
Amenywima haki yake, hanayo raha!
Na moyo wangu ucheke, kwa ha. ha, ha, ha!
Kucheka kwa kucheka
Mimi katu sitacheka

Maswali

a) Taja na ueleze shairi hili ni la aina gani? **[alama2]**
b) Taja sababu zozote tano zinazomfanya mwandishi wa shairi hili asitake kucheka. **[alama5]**
c) Chambua shairi hili kimtindo. **[alama4]**
d) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **[alama4]**
e) Tambua nafsineni katika shairi. **[alama2]**
f) Bainisha mbinu tatu za kimtindo zinazojitokeza kwenye shairi hili. **[alama3]**

Mwisho

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TATU)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika insha* ***mbil****i. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima.***
b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
c) *Kila insha isipungue maneno* ***400.***
d) *Kila insha ni alama* ***20.***
e) *Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

1. **Lazima**

Umeteuliwa kama mwenyekiti wa tume inayoshughulikia mambo yanayochangia visa vya wanajamii kuwa na msongo wa mawazo. Umewaalika wanatume wengine wawili ili kujadili chanzo cha swala hili. Andika mazungumzo baina yenu.

2. Jadili namna mshikamano baina ya walimu na wanafunzi shuleni unavyoweza kuboreshwa.

3. Andika kisa kinachounga mkono methali;

Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu.

4. Tunga kisa kitakachoanza kwa maneno haya;

Sauti za watu, wengine wakinishangilia na wengine wakinikashifu, zilichanganyika hewani na kuwa kelele zisizoeleweka**…**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TATU)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Andika mkondo wa kidato chako ,tarehe kisha utie sahihi yako katika nafasi ulizoachiwa*

c) *Jibu maswali **yote.***

d) *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

e) *Majibu yote **sharti** yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

f) *Usitoe ukurasa wowote katika kijitabu hiki,*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

1. UFAHAMU: (Alama 15)

<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.</u>

Ulikuwa wakati wa jioni jua limepunguza udhia wake na upepo mwanana ulikuwa ukipita na kuzipapasa Ngozi zetu mfano wa pamba. Kama ilivyokuwa desturi yetu pale chuoni, siku hiyo tuliketi karibu na lango kuu la chuo ili kutafiti kazi mradi tuliyokuwa tumepewa darasani. Sehemu hii tuliipenda sana kwa kuwa kuuchakura mtandao ilikuwa ni bure bora tu ufahamu nywila ya mtandao huo. Mandhari ya sehemu hii pia yaliwavutia wanafuzi wengi katika sehemu hii.

Tulipotia fahamu, tulipata mazoea haya yamekita mizizi nasi tukawa hatuna budi kuyakumbatia. Hatukuyakumbatia tu, bali tuliyakumbatia kwa dhati ya moyo. Vikao hivi havikuwa tu hazina kubwa kwetu bali pia vilikuwa vya thamani isiyomithilika. Hapa ndipo tulinoleana bongo kwa kupashana habari. Leo hii tumo katika mjadala kuhusu kuhusu mfumo mpya wa elimu CBC tuliopewa darasani kama kazi mradi. Nahodha wa kikundi hiki anampa msemaji wa kwanza nafasi naye hakusita kushika usukani.

"Nionavyo mimi, mfumo wa CBC unafaa kufutiliwa mbali. Serikali haijajiandaa vilivyo ili kuufanikisha mfumo huu wa elimu. Kwanza, mafunzo waliyopewa walimu ili kuufanikisha mfumo huu kamwe hayatoshi. Nionavyo mimi ni kwamba walimu waliopo ambao idadi yao haitoshi, wanatumia elimu ya mfumo wa 8-4-4 kuufunza ule wa CBC. Itawezekanaje mwalimu apate mafunzo ya wiki moja kisha akawa amefuzu kumwelekeza mwanafunzi? Isitoshe mfumo huu unamhitaji sana mwalimu kutumia teknolojia ya kisasa katika ufunzaji. Usishangae nikikwambia kuwa walimu wengi hawana mafunzo ya kisasa ya kompyuta. Zaidi ya hayo shule nyingi vilevile hazina tarakilishi. Baadhi yazo pia umeme haupo. Baada ya serikali ya uhuru kuahidi kuwapa Watoto vipakatalishi, je jiulize, ni wanafunzi wangapi hivi sasa ambao walipata vipakatalishi hivyo? Kando na hayo, wazazi wengi washalalamika kuhusu gharama kubwa ya vifaa ambavyo walimu huwatuma wanafunzi kuvileta shuleni. Huenda ikawa sababu ya wao kusema kuwa ni heri mfumo huo wa CBC ukaachiwa shule za kibinafsi.

Muda huo wote kila mtu pale tulipoketi alikuwa ametulia. Wapo waliotikisa vichwa kukubaliana naye Sumaku na wapo waliotikisa kukataa. Mara kijana mmoja tuliyemwita Sudi alisimama na kuzungumza. mawazo yake sudi ni kama yalikuwa ya kumpinga sumaku.

"Mtazamo wangu mimi ni kuwa mfumo wa CBC haufai kufutiliwa mbali. Itakuwa hasara kubwa kwa washika dau mbali mbali ambao wameekeza katika mfumo huu. Ikumbukwe kwamba imeigharimu serikali ya Uhuru pesa nyingi katika kujenga madarasa, kuwafunza walimu pamoja kuchapisha vitabu vya mfumo huu. Isitoshe kuutupilia mbali mfumo huu itakuwa sawa nakuwapotezea muda wanafunzi wa darasa la sita ambao kwa miaka sita wamekuwa wakisoma mfumo huu"

"Nakuunga mkono sumaku, alianza Dida. Kwanza sudi awazie tena udhaifu wa mfumo 8-4-4 ndipo awazie hayo. Kila mwanafunzi katika mfumo huu wa CBC ni mshindi. Hakuna kuwagawa wanafunzi katika makundi ya wajinga na werevu. Isitoshe, katika mtaala huu mpya, hakuna kurudia rudia madarasa kama ilivyo katika mfumo huo wa awali. Vile vile, mtaala wa CBC utawapa wanafunzi wa Kenya matumaini na fursa ya kuimarisha vipawa na uwezo wao. Ikumbukwe kwamba mtaala huu unasisitiza ukuzaji wa talanta za wanafunzi nchini tofauti na ule

wa 8-4-4. Pia, CBC humfunza mwanafunzi masomo ambayo tu yatamfaa maishani mwake. Lugha asili za wanafunzi pia zitakuzwa katika mfumo huu mpya. Hivyo basi serikali yake Ruto na Riggy G haina budi kuufanikisha mtaala huu.

Maneno yake Dida yalifunikwa ghafla na kelele za kumshangilia na kumsifu kijana huyu. Alipoona bado wanashangilia, aliinua mkono wake wa kushoto juu na kusema, "Basi ! basi wanafunzi wenzangu, sina shaka ujumbe umeshafika.

a) Ni mambo yepi yanayoleta utangamano baina ya vijana katika kundi hili chuoni**?(alama 3)**

b) Eleza udhaifu wa mfumo wa 8-4-4 kulingana na kifungu hiki. **(alama 5)**

c) Jadili manufaa ya mfumo mpya wa elimu kulingana na Makala haya**. (alama 5)**

d) Kauli "upepo mwanana ulikuwa ukipita na kuzipapasa Ngozi zetu, " imetumia tamathali gani ya usemi? **(alama 1)**

e) Eleza maana ya "tulinoleana bongo" kwa mujibu wa taarifa**. (alama 1)**

2. UFUPISHO (Alama 15)

<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.</u>

Bei ghali ya vyakula ni jambo linalowaathiri wakenya wengi kwa hivi sasa. Inasikitisha kupata kwamba bei ya unga wa ugali imepanda hadi sh. 200. Ni wazi kwamba familia nyingi nchini hukosa lishe lao kutokana na kufumka kwa bei ya bidhaa muhimu. Hata hivyo ibainike kwamba nchi isiyowakimu raia wake kwa chakula ni sawa ng"ombe aliyeshindwa kumnyonyesha ndama wake.

Kwa muda mrefu, viongozi wamekuwa wakipambana na tatizo la ukosefu wa chakula. Msimu wa kiangazi unapobisha hodi, watu wengi hasa wale wahitaji hupukutika kutokana na mngato wa njaa. Japo serikali na wafadhili hutuma vyakula vya msaada kwa jamii zilizoathirika, chakula hiki huwa kama nguo ya kuazima, na bila shaka ya kuazima haikidhi haja.

Mojawapo ya vyanzo vikuu vya uhaba wa chakula ni kiwango cha chini cha uzalishaji na uhifadhi wa chakula chenyewe. Zipo seheu nyingi ambazo ni kame nchini.sehemu hizi hukabiliwa na ukosefu wa maji kwani, ama mvua hainyeshi au inaponyesha haitoshelezi mahitaji ya mimea. Mimea mingi hujikaukia ikiwa michanga na kudhihaki juhudi za wapanzi. Zipo sehemu katika nchi hii ambazo huenda kwa misimu hata mitano bila kupata zao lolote kutoka mashambani. Hali ikiwa hivi makali ya uhitaji huzidi na wakazi wa sehemu hizi hulazimika kuwa wategemezi kwa majirani na serikali. Wengine wanapokosa chakula kabisa huazimia kula visivyoliwa. Wanaamwa la mbwa baada ya kukosa la mama.

Hali kadhalika japo zipo sehemu zingine ambazo hazina tatizo la ukame, mbinu hasi za kilimo husababisha utoaji wa mavuno haba, hivyo kutojitosheleza kwa chakula. Bilas haka wanapopanda ovyo wanavuna ovyo. Kuna wakulima ambao hupalilia mmomonyoka wa udongo kwa kulima kando kando ya mito, kupanda zao lile lile katika sehemu ile ile ya ardhi miaka nenda miaka rudi, na kutopanda mimea ambayo hukinga tabaka la juu la udongo dhidi ya kumomonyolewa na maji

au upepo. Matokeo ya haya yanaweza kutabiriwa; udongo wenye rutuba huoshwa na mashamba kutwaa utasa ambao huzidisha kuzalisha kwa chakula haba. Wakulima wengine hukaidi wito wa kupanda mimea ambayo hustahimili ukame kama vile mbaazi mihogo, mtama na wimbi. Baadhi ya wakulima hufuga mifugo wengi ambao hushindwa kustahimili kiangazi. Si ajabu kupata kwamba katika baadhi ya maeneo mizoga ya ngombe na hata ngamia imezagaa kote tanuri la kiangazi linapofanya kazi yake.

Sehemu zingine zimebarikiwa na ukwasi wa chakula. Hata hivyo baadhi ya wakazi wa sehemu hizi hawana mwao kuhusu umuhimu wa lishe bora. Wapo wanaodhani kuwa chakula ni chakula bora tumbo lipate haki. Hawa hula vyakula kama vile viazi, mahindi, na wengine nyama bila kujua wanahiyaji vyakula vyenye virutubisho muhimu, yani wanga, protini , vitamini na madini. Wapo wanaodhani kuwa protini pekee ni nyama. Hawa hula nyama mawio na machweo, matokeo yakiwa kuambulia magonjwa kama vile shinikizo la damu.

Katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa chakula, serikali kupitia wizara husika imeanzisha miradi ya kuhakikisha kuwa kuna uzalishaji wa chakula kwa kiwango cha kuridhisha. Serikali ya Ruto sasa imepunguza bei ya mbolea hadi sh 3500 ili kuwawezesha wakulima kupanda chakula kwa wingi. Visima na mabwawa ya maji pia vitachimbwa katika maeneo kame ili kunyunyuzia mashamba maji. Baadhi ya wakulima wameanza kupanda mimea ambayo inapevuka na kutoa mazao kwa haraka ipo mimea ya kuatika ambayo hutoa matunda baada ya muda mfupi, hivyo kusaidia kupunguza makali ya njaa. Wafugaji wengine wameanzisha miradi ya kufuga kuku wa kututumuliwa. Hawa hukuwa na kukomaa kwa muda mfupi na huweza kutoa nyama na mayai. Wafugaji wa kuku hawa huweza kuwauza kununua aina nyingine ya chakula.

Wakulima pia wanahimizwa kutumia njia za kisasa za kuzalisha na kuhifadhi chakula.chakula kinapohifadhiwa vyema, hata mvua isiponyesha raia huweza kujitegemea. Ikiwa maghala ya halmashauri za kuhifadhi chakula nchini hayahifadhi chakula mara nyingi hulazimika kuagiza chakula kutoka nje kiangazi kinapojiri. Aidha chakula kisipohifadhiwa vyemahuishia kuharibika na kuhasiri wanaokila ikawa msiba juu ya mwingine.

Ni muhimu kufahamu kuwajukumu la kupambana na ukosefu wa chakula ni la kila raia. Hali ya kungojea kila mara kulishwa na serikali inatufanya kuwa wategemezi Zaidi. Wadogo wadogo ambao huuza vyakula kwa bei ya chini sana mara tu wanapovitoa mashambani wanapaswa kujiasa dhidi ya mazoea haya na kujua kuwa akiba haiozi. Wanaoishi katika sehemu za vinamasi wasaidiwe kuzitunza sehemu hizi na kuzitumia kwa njia endelevu. Vijana wahimizwe wawaunge wazee mkono kushughulikia kilimo katika sehemu za mashambani badala ya kuhamia mijini kutafuta kazi za ajira ambazo ni haba.

a) Fupisha ujumbe wa aya tano za kwanza kwa maneno 100. (alama 9, 1 ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

b) Kwa kurejelea aya tatu za mwisho, eleza njia sita za kukabiliana na uhaba wa chakula. (maneno 85) **(alama 6, 1 ya mtiririko)**

Matayarisho

Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

a) Kamilisha jedwali lifuatalo kwa kuandika sauti zifaazo. **(alama 3)**

AINA	midomo	meno	ufizi	Mdomo na meno	Kaakaa gumu	Kaakaa laini	koromeo
Vipasuo						_____	
Vizuio kwamizwa					____		
vikwamizo			____				
Ving`ong`o	___						
kitambaza			____				
kimadende							
Nusu irabu					___		

b) Tofautisha sentensi zifuatazo kimaana. **(alama 2)**

i. Andai angelimnywesha babu uji kwa kikombe, babu angelishiba.

ii) Andai angalimnywesha babu uji kwa kikombe, babu angalishiba.

c) Ikanushe sentensi ifuatayo kwa wingi **(alama 2)**

Mwizi alimkata sikio na pua

d) Tunga sentensi moja itakayodhihirisha kielezi cha namna mfanano**.** **(alama 2)**

e) Ainisha mofimu katika kitenzi kilicho katika sentensi hii. **(alama 3)**

Wapenzi hao watanywiana sharubati.

f) (i) Nini maana ya kirai? **(alama 1)**

(ii) Tunga sentensi moja inayodhihirisha kirai kihusishi. **(alama 2)**

g) Eleza tofauti za kimatumizi kati ya alama zifuatazo za uakifishaji**.** **(alama 2)**

i.Koloni ……..

ii) Nusu koloni …….

h) Andika upya sentensi zifuatazo kilingana na maagizo uliyopewa.

i. Mbuzi walipopotea, mchungaji alikuwa na wasiwasi. (Anza kwa, Kupotea.... **(alama 2)**

ii. Dereva aliyesababisha ajali alihukumiwa miaka minne na kazi ngumu.

(Maliza …aliyesababisha ajali. **(alama 2)**

i) Tunga sentensi itakayodhihirisha kielelezo kifuatacho cha mstari**.** **(alama 2)**

S-RN(N+V+V)+KT(T+E)

j) Tunga sentensi moja itakayodhihirisha maana ya vitate rika na lika. **(alama 2)**

k) Bainisha vitenzi katika sentensi hii. **(alama 3)**

Ndege yu taabani, hata hivyo anajaribu kujinasua.

l) Onyesha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Bi. Kerubo alirembeshwa nyusi kwa wanja mweusi.

m) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa**.** **(alama 2)**

"Shughuli yangu itamalizika leo," mama alimwambia baba.

n) Andika visawe vya; **(alama 2)**

i) Rai ……

ii) Azimio ……..……

o) Vumisha neno zuri kwa kulitungia sentensi. **(alama 2)**

p) Ainisha vihusishi katika sentensi ifuatayo**.** **(alama 2)**

Rais alifika mapema kuliko wengine halafu akaondoka.

q) Tambua matumizi ya kiambishi -ji- katika sentensi **(alama 2)**

Jino la jitu hilo lililiwezesha kujilia chakula kingi.

r) Ikamilishe methali ifuatayo. **(alama 1)**

Cha mkufuu**……**

s) Igeuze sentensi ifuatayo iwe katika mazoea**.** **(alama 1)**

Matunda yanayoiva ndiyo yanayotundwa.

4. ISIMU JAMII (Alama 10)

Tumia kauli ifuatayo kujibu maswali

Haya ng`ara leo, nguo moto moto. Fifty hamsa fifty hamsa fifty hamsa na nyingine. Shati shilingi hamsini tu. Kuona ni bure…

a) Kando na sifa zinazojitokeza katika Makala haya taja sifa zingine tano za sajili hii. **(alama 5)**

b) Eleza juhudi tano zinazofanywa ili kukikuza Kiswahili nchini Kenya na dunia kwa jumla. **(ala** 5)

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TATU)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Jibu maswali manne pekee.*

b) *Swali la kwanza ni la lazima.*

c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya,Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*

d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

e) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU A:
FASIHI SIMULIZI

SWALI LA LAZIMA

1. SEHEMU YA A: USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Jama, Jama, Jamani
Mbona twabebeshwa mateso hivi
Mizigo mikubwa ya dhiki kama
Kwamba hatuna haki ya kusema
Kukataa ndoa za lazima
Kukataa kuozwa wazee
Kukataa kukatishwa masomo
Kukataa tohara ya lazima

Jama, Jama Jamani
Iweje tuteswe mateso haya
Na watu wasio kuwa hata na haya kama
Kwamba hatuna haki ya kulalamika
Kulalamikia kutumikishwa kama mayaya
Kulalamikia kudhalilishwa kiunyama
Kulalamikia kutolindwa na sheria

Jama, Jama, Jamani
Sasa hii ni awamu nyingine
Na macho tumeyafungua kabisa
Tumekataa kudhalilishwa kabisa
Tumekataa kuteswa kama watumwa
Tumekataa tohara ya lazima
Tumekataa kuozwa..... Tumekataa! Tumekataa
Hii awamu ya 'Haki ya mtoto wa kike'

Maswali

(a) Taja mambo **matatu** muhimu yaliyozungumziwa na mshairi kisha ueleze kila moja **.(alama 6)**
(b) Eleza muundo wa shairi hili **(alama 4)**
(c) Taja mbinu **mbili** za lugha alizotumia mshairi kisha ueleze kila moja **(alama 4)**
(d) Kwa nini mshairi huyu anasema hii ni 'awamu' nyingine? **(alama 3)**
(e) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi **(alama 3)**
(i) awamu
(ii) kudhalilishwa
(iii) Dhiki

SEHEMU YA B:

Tamhilia –Timothy M Arege:Bembea ya Maisha

Jibu swali la 2au la 3

2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:

...lakini ndio tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama... kama... kama... kama vile tambara bovu.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Eleza umuhimu wa msemaji katika kukuza ploti. **(alama 4)**

c)Tambua mbinu nne za kimtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

d)Kwa kutoa hoja nane kutoka kwa Tamthilia eleza ni vipi utamaduni ulivyothaminiwa katika jamii hii ya Bembea ya Maisha. **(alama 8)**

AU

3.Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii ya Bembea ya Maisha. **(alama 20)**

SEHEMU YA C:

Riwaya ya Nguu za Jadi-Prof Clara Momanyi

Jibu swali la 4 au la 5

4.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuta ;

Watategemewa na nani maishani? Hiki ndicho kizazi cha kesho au kizazi kilichopotea tayari?

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

b)Tambua toni katika mazungumzo haya. **alama 2)**

c)Onyesha ni vipi kizazi cha leo na cha kesho kilivyopotea. **(alama 12)**

AU

5.Fafanua ufaafu wa anwani ya ,'Nguu za Jadi'. **(alama 20)**

SEHEMU YA D:

Diwani ya Mapambazuko ya Machweo na Hadithi zingine.

Jibu swali la 6 au la 7

6.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Akainama chini kwenye tendeguu moja la kitanda cha besera.Akachukua kibatari cha kiberiti ili awashe taa.Mimi,nikiwa mle mvunguni.sasa kwa hakika nilishamjua shetani wa mzimu ule ni nani.Kumbe hakuwa shetani wala Kipwerere!

a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(alama 4)**

b)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

c)Onyesha umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(alama 4)**

d)Wanakijiji waliuogopa mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuuabudu na kutoufanyia mzaha. Thibitisha kauli hii. **(ala8)**

AU

7. Kimyakimya analikariri;
Mteule nimechoka ,kila siku kusikiya,
Vyereje nchi hakika,visanga kupindukiya,
*Tunazidi filisika ,**walaji kujijaziya***
Msiba kujitakia, kweli hauna kiliyo.

a)Huu ni ubeti wa shairi katika hadithi"Msiba wa Kujitakia'.Eleza sababu ya mwandishi kutumia mbinu hii katika usimulizi. **(alama 6)**
b)Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari katika dondoo. **(alama 8)**
c)Bainisha maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika kifungu hiki. **(alama 6)**

SEHEMU YA E:
FASIHI SIMULIZI

8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Malaika
Nakupenda malaika x2
Ningekuoa malaika...
Ningekuoa dada...
Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

Pesa, zasumbua roho yangu x2
Nami niafanyeje, kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina wee...

Ningekuoa malaika x2

(a) Ainisha wimbo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. **(alama 2)**
(b) Andika sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa na wimbo huu. **(alama 2)**
(c) Eleza mikakati **sita** ambayo mwimbaji angetumia kufanikisha uwasilishaji wa wimbo huu. **(alama 6)**
(d) Unanuia kutumia mahojiano kukusanya habari kuhusu nyimbo za aina hii.
(i) Eleza manufaa **matano** ya kutumia mbinu hii. **(alama 5)**
(ii) Eleza changamoto **tano** za kutumia mbinu hii. **(alama 5)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA NNE)

102/1

KISWAHILI

PAPER 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika insha* ***mbili****. Insha ya kwanza ni ya* ***lazima****.*

b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

c) *Kila insha isipungue maneno* ***400.***

d) *Kila insha ina alama 20.*

e) *Kila insha* ***lazima*** *iandikwe kwa lugha ya* ***Kiswahili.***

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Lazima:

Wewe ni mwakilishi wa vijana katika gatuzi lenu. Kumekuwa na tuhuma za vijana kutumia vibaya simu tamba katika jamii. Andika mahojiano yako na mwanahabari ukitetea namna simu tamba inavyowafaidi vijana.

2. Fafanua umuhimu wa kudumisha amani nchini wakati wa kampeni na uchaguzi wa kisiasa.

3. Andika insha inayooana na methali ***mchuma janga hula na wa kwao.***

4. Andika insha itakayoisha kwa maneno yafuatayo:

….nilipogutuka niliangaza macho huku na kule. Aah! Kumbe nilikuwa nikiota!

KCSE 25

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA NNE)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Jibu maswali yote katika nafasi uliyopewa.*

b) *Andika majibu yako kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

	SWALI	**UPEO**	**ALAMA**
1.	Ufahamu	15	
2.	Ufupisho	15	
3.	Matumizi ya lugha	40	
4.	Isimujamii	10	
	Jumla	80	

1. UFAHAMU(alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Athari za muda mrefu za pombe hutapakaa baina ya uwezekano wa faida za kiafya kwa watumiaji wa viwango vya chini vya pombe hadi madhara makubwa katika hali ya matumizi mabaya ya pombe kwa muda mrefu.

Viwango vya juu vya matumizi ya pombe huhusiana na ongezeko la hatari ya kuendeleza ulevi, ugonjwa wa moyo, kutofyonza vyakula, ugonjwa sugu wa kongosho, ugonjwa wa ini kutokana na pombe, na kansa. Uharibifu kwa mfumo mkuu wa neva na mfumo wa neva za pembeni unaweza kusababishwa na matumizi ya kila mara ya pombe. Matumizi ya pombe kupita kiasi kwa muda mrefu yanaweza kuharibu takribani kila kiungo na mfumo katika mwili. Ubongo unaokua wa kijana aliyebaleghe huwa hasa katika hatari kubwa ya kudhurika na sumu ya pombe.

Kihistoria, madaktari wametetea pombe kwa faida zake za kiafya na hivi karibuni kwa ajili ya uwezo wake wa kulinda watumiaji dhidi ya ugonjwa wa moyo. Kuna ushahidi wa faida kwa mishipa ya moyo inayotokana na kutumia kinywaji kimoja hadi viwili kwa siku, hata hivyo, faida za kiafya kutokana na unywaji pombe kwa wastani ni swali lenye utata. Shauku zimetolewa kuwa sawa na ilivyo katika sekta za dawa, wadau wa sekta ya pombe pia wamehusika katika kutilia chumvi faida za kiafya za pombe. Pombe inapaswa kuonekana kama dawa ya burudani yenye uwezo mkubwa wa kusababisha athari mbaya kwa afya na haipendekezwi kwa ulinzi wa moyo badala ya mbinu nyinginezo za salama na zilizothibitika za jadi kama vile lishe bora mazoezi na tiba.

Baadhi ya wataalamu wanadai kuwa faida za matumizi ya pombe ya wastani zinaweza kupitwa na ongezeko la hatari ikiwa ni pamoja na majeraha, vurugu, uharibifu wa mimba, aina fulani za saratani, ugonjwa wa kongosho na presha. Kwa vile faida bainifu za kiafya za matumizi ya pombe ya wastani ni ndogo kwa watu walio katika hatari ndogo ya kupata maradhi ya moyo, wataalamu wengine wanatahadharisha itumike kwa tahadhari kwa sababu ya uwezekano kwamba kupendekeza matumizi ya wastani ya pombe kunaweza kusababisha ongezeko la hatari ya matumizi mabaya ya pombe, hasa miongoni mwa vijana.

Madhara mabaya ya matumizi ya pombe kwa muda mrefu kupita kiasi ni sawa na yale yanaoonekana katika vitulizi-hipnoti vingine (mbali na sumu kwa viungo ambayo hutatiza zaidi katika pombe). Athari za kujiondoa katika pombe na utegemezi hukaribia sana kufanana. Pombe cha kiwango wastani ina athari chanya na hasi kwa afya. Athari hasi ni pamoja na ongezeko la hatari ya magonjwa ya ini, saratani ya orofarinji, kansa ya umio na magonjwa wa kongosho. Kinyume na hayo, unywaji wastani wa pombe unaweza kuwa na athari za faida kwa gastritis na kolelithiasi. Matumizi sugu na mabaya ya pombe huwa na athari kubwa kwa afya mwili na akili. Unywaji sugu wa pombe kupita kiasi au utegemezi pombe, unaweza kusababisha uharibufu mpana wa viungo mbalimbali vya neva za ubongo, mfumo wa neva ugonjwa wa mishipa ya moyo, maradhi ya ini, na neoplamsi isiyopona.

Matatizo ya akili ambayo huhusishwa na ulevi ni pamoja na mfadhailo mkubwa, disthimia, mania, hipomania, tatizo la hofu, tatizo la wasiwasi wa kijumla, tatizo la tabia za mtu, skizofrenia, kujinyoga, upungufu wa mfumo wa utendekazi mwilini (kwa mfano kazi za kumbukumbu, hisia,

kazi za uamuzi, uwezo wa kuona, mwendo na uwiano) na uharibufu wa ubongo, utegemezi wa pombe ni huhusishwa na shinikizo la damu, ugonjwa wa moyo na kiharusi cha iskemi, kansa ya mfumo wa upumuaji, mbali pia na saratani ya mfumo wa mlo, ini, kifua na ovari.

Unywaji kupita kiasi huhusishwa na ugonjwa wa ini, kama vile sairosi. Tafiti zimelenga wanaume na wanawake, vikundi vya umri mbalimbali na watu wa makundi mengi ya kijamii. Machapisho kwa sasa yanafikia jumla ya mamia huku tafiti zikiweza kuonyesha uwiano uliopo kati ya matumizi wastani ya pombe na afya ambayo labda yanaweza kuwa yalitokana na athari za manufaa ya maingiliano ya kijamii ambayo mara nyingi huambatana na matumizi ya pombe. Baadhi ya njia mahususi ambapo pombe huweza kuathiri afya mishipa ya moyo zimetafitiwa.

Maswali

a. Yape makala haya mada faafu. **(alama 1)**

b. Eleza madhara yanayotokana na uharibifu wa mfumo mkuu wa neva za pembeni **(alama 2)**

c. Eleza faida za matumizi ya pombe kwa mujibu wa kufungu. **(alama 3)_**

d. Mwandishi anapendekeza vipi kwa matumizi ya pombe ya kiwango cha wastani? **(alama 3)**

e. Matumizi sugu yana malipo yapi kulingana na madaktari. **(alama 3)**

f. Tafiti zilizofanywa zililenga jinsia ya kiume pekee. Thibitisha. **(alama 1)**

g. Eleza maana ya misamiati hii kulingana na taarifa **(alama 2)**

(i) wadau

(ii) aliyebaleghe

SEHEMU B

2. UFUPISHO(alama15)

Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali yafuatayo

Lugha ndio msingi wa maandishi yote. Bila lugha hakuna maandishi. Kila jambo tufanyalo kuhusiana na lugha husitawisha ufahamu wetu wa mambo tusomayo. Mazoezi katika kuandika husitawisha ufahamu katika kusoma kwa sababu katika kuandika ni lazima kuyatumia maneno vizuri kuzungumuza na kuwasikiliza wengine wakizumgumuza. Lugha tusomayo ni anina ya lugha ya masungumuzo.

Kuna ujuzi mwingi katika kuzungumuza kama vile michezo ya kuigiza, hotuba, majadiliano na mazungumuzo katika darasa. Haya yote husaidia katika uhodari wa matumizi ya lugha. Ujuzi wa kila siku utasaidika katika maendeleo ya kusoma na usitawi wa msamiati. Ikiwa mwanafunzi amemwona ndovu hasa, atakuwa amejua maana ya neno ndovu vizuri zaidi kuliko mwanafunzi ambaye hajawahi kumwona ndovu bali ameelezwa tu vile alivyo. Vilevile ujuzi wa kujionea sinema au michoro husaidia sana katika yaliyoandikwa. Ikiwa mwanafunzi ana huzuni au ana furaha, akiwa mgonjwa au amechoka an amefiwa, haya yote ni ujuzi . Wakati mwanafunzi asomapo juu ya mtu ambaye amepatikana na mambo kama hayo hana budi kufahamu zaidi.

Karibu elimu yote ulimwenguni huwa imeandikwa vitabuni. Hata hivyo, lugha zote hazina usitawi sawa kuhusu fasihi. Kwa bahati mbaya lugha nyingine hazijastawi sana na hazina vitabu vingi.

Fauka ya hayp, karibu mambo yote yanayohusiana na elimu huweza kupatikana katika vitabu kwenye lugha nyingine.

Inabidi mwanafunzi asome vitabu au majarida juu ya sayansi au siasa au historia, lakini haimbidi kusoma tu juu taaluma fulani anayojifunza. Inafaa asome juu ya michezo, mambo, ya mashairi na juu ya mahali mbalimbali ili kupata ujuzi wa mambo mengi.

a) Fupisha aya za kwanza mbili kwa kutumia maneno 65 (alama 10, 1 ya utiririko)

Matayarisho

b) Kwa kuzingatisha habari zote muhimu na bila kupoteza maana asilia, fupisha aya ya mwisho (Maneno 30) (alama 5 , 1 ya utiririko)

Matayarisho

SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA NA SARUFI (alama 40)

(A) Andika sauti yenye sifa zifuatazo

(I) Sauti mwambatano ya midomo **(alama 2)**

(II) Andika neno lenye muundo ufuatao **(alama 2)**

Konsonanti+konsonanti+nusu irabu +konsonanti+irabu

B)Bainisha vishazi katika sentensi **(alama 2)**

Mwanafunzi huyo angelisoma sana, angelifaulu katika mtihani.

C)Tunga sentensi yenye muundo huu: **(alama 2)**

Nomino ya wingi, kivumishi kiradidi, kitenzi kishirikishi kikamilifu, chagizo cha Mahali

D)Tunga sentensi ukitumia neno ‘zawadi’ kama kitenzi **(alama 2)**

E)Andika upya katika wakati ujao hali ya mazoea **(alama 2)**

F)Taja vigezo viwili vya kuanisha viambishi **(alama 2)**

G)Changanua sentensi hii kwa kielelezo cha mstari

Gazeti hilo litasomwa na mwanafunzi **(alama 2)**

H)Ainisha viambishi **(alama 2)**

Wasoila

I)Tunga sentensi yenye vijenzi **hivi** **(alama 1)**

KN(RH+ S)+KT(t+V)

J)Eleza matumizi ya ‘A’ anganifu katika sentensi **(Alama 3)**

(I) Mlango wa chuma umenunuliwa.

(II) Msumeno wa kukatia ubao ni huu.

(III) Mwimbaji wa kwanza yu jukwaani sasa.

K)Andika katika udogo

Kiti hiki cha mwanamke huyu kimevunjika **(alama 2)**

L)Eleza matumizi ya koloni na koma katika sentensi **(alama 1)**

Nyanya alinunua vitu hivi: pilipili, parachichi, pipi na papai.

M)Geuza katika hali ya wingi

Seremala aliunda kasha kwa ubao na kumpa mtume **(alama 2)**

N)Taja dhana za kimaana mbili zilizo katika sentensi **(alama 1)**

Ningekuwa na hela ningenunua shamba.

O)Tunga sentensi venye kishazi tegemezi ambacho ni**;** **(alama 2)**

(I) Kielezi cha namna

ii)Kielelezi cha Mahali

(P) Ainisha sentensi hii kwa kuzingatia dhamira **(alama 1)**

Komesha mchezo huu kuanzia leo!

(Q) Onyesha kwa kutoa mifano miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U-_Zi **(alama 2)**

(R) Ainisha yambwa katika sentensi hii

Yaya alitumia kijiko kumpatia mtoto huyo mdogo chakula kitam**u** **(alamu 3)**

(S) Andika kitenzi katika kauli ulizopewa kisha ukitungie sentensi **(alama 2)**

(i) Kauli tendata

(ii) Kauli tendama

(T) Eleza maana mbili katika utungo huu **(alama 2)**

Fundi alimkatia Makaa utepe huo.

SEHEMU D: ISIMU JAMII(alama 10)

Soma makala haya kisha ujibu maswali;

Rafiki yako amezongwa na mambo magumu na anafikiria suluhu ni kujiua umepewa jukumu la kumshauri.

(a) Utatumia Lugha ya sajili gani? **(Alama 2)**

(b) Fafanua sifa nane za kimtindo utakazomatumia ili kufanikisha mazungumuzo yako **(alama 8)**

MWISHO.

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA NNE)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

- ***a)*** *Jibu maswali manne* ***pekee****.*
- ***b)*** *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima***
- ***c)*** *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani; Riwaya Hadithi fupi,Tamthilia na Ushairi.*
- ***d)*** *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*
- ***e)*** *Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
	Jumla	

SEHEMU YA A : RIWAYA
CLARA MOMANYI: Nguu Za Jadi

LAZIMA

1. "Waite. Unadhani mapenzi yanaogopa polisi"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

(b) Fafanua sifa **sita** za msemewa **(alama 6)**

(c) Kwa kutoa mifano taja mbinu **tatu** za kimtindo katika dondoo hili (**alama 3)**

(d) Msemewa na wenzake ni adui wa wananchi wa Matuo. Fafanua ukweli kauli hii kwa kurejelea riwaya ya Nguu Za Jadi **(alama 7)**

SEHEMU YA B: TAMTHILIA ;Timothy Arege: Bembea ya Maisha

Jibu swali la 2 au la 3

2. (a) "Maradhi! Madhila yake hayasemeki. Yakimla mtu humthakilisha. Humwacha hoi,hana mbele wala nyuma."

i. Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

ii. Fafanua toni katika dondoo hili **(alama 1)**

iii. Eleza sifa nne za **msemaji** **(alama 4)**

iv. Taja na ufafanue mbinu za kimtindo katika dondoo hili **(alama 3)**

(b) Changanua mtindo **(alama 8)**

"Bunju ni mmoja wenu. Nyote ni wanangu." Hayo ni maneno ya mama. Wakati huo sikuona. Sasa naona. Wanasema mwenye macho haambiwi tazama. Kweli iliyoje! Japo hutokea wakati tukalalamika,ninafikiri Bunju ni zawadi nzuri kwetu. Leo tungekuwa wapi bila Bunju? Maji yangezidi unga. Usingepikika,usingelika.(kimya) Hebu fikiri! Umepata ajali mbaya. Inakuacha mahututi. Anapita mtu katika gari lake. Kwa imani anaguswa. Anakufanyia mpango wa Flying Doctors;ndege inafika na kukupeleka hospitali. Mwenyewe huyo analipia kila kitu!mtu huyo atakosaje kuwa zawadi kwako?

3. "Mama sijaona baba akipika hivi karibuni."

Kwa kurejelea nukuu hii fafanua usasa na utamaduni vilivyosawiriwa katika tamthilia ya Bembea ya Maisha **(Alama 20)**

SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

Rachel Wangari: Fadhila za Punda

Winnie Nyaruri Ogenche: Sabina

Jibu swali la 4 au la 5

4. ***Racheal Wangare:Fadhila za Punda***

"Rudi, nyumbani mwanamke wewe! Nitakuja jioni tuyamalize haya."

a) (i) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama 4)**

(ii) Fafanua hulka ya msemaji wa kauli hii **(alama 4)**

iii) Huku ukizingatia hadithi hii, jadili maudhui ya mabadiliko yanavyojitokeza katika hadithi **(alama 7)**

b) *Changanua mtindo katika dondoo hili* **(alama 5)**

Aligutuka kutoka kwenye usingizi wa mang'amung'amu,roho mkononi,pumzi zikimkwenda mbio. Hakujua kilichomwamsha,hivyo alitega sikio ndi! Isije akawa mwenye nyumba akaja na yeye mpangaji akachelewa kumfungulia mlango;itakuwa balaa bin beluwa. Ndio maana amelala pale juu ya kochi ili akiingia tu,hata kabla ya kubisha mlango,awe tayari kuufungua. Hilo litampa usalama,japo kwa muda tu. Baada ya kusikiliza kwa makini na kuchungulia nje,hakumwona aliyemtarajia.Asaa akaamua asifike leo.Lakini hilo halikumpunguzia wasiwasi mwenzetu,maanake kesho pia ni siku.Atakuja tu,labda ghamidha itakuwa imezidi,imefura kama hamri lililotiwa hamira.Matokeo yake aliyajua.Si bughudha hizo,nyanyaso moto mmoja.Naye yuko pale tu,subira kifuani,dua mdomoni. Walisema mvumilivu hula mbivu ila yeye hakujua stahamala yake ingempeleka wapi!

AU

5. *Winnie Nyaruri Ogenche; Sabina*

"Ninaomba wazazi wenzangu muwape watoto wa kike elimu badala ya kuwaoza mapema. Hongera, mwanangu kwa kupata alama mia nne arubaini na saba"

a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika **(alama 5)**
b) Tambua mbinu ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili **(alama 1)**
c) Fafanua jinsi mbinu yenyewe ilivyotumika ili kufanikisha utunzi wa hadithi **(alama 6)**
d) Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi **(alama 8)**

SEHEMU YA D: USHAIRI ;*Jibu swali la 6 au la 7*

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Mwanadamu mambo yake, kueleweka muhali
Ubavuni umuweke, umtowe kule mbali
Maskanini afike, umtindie fahali
Utamu anufaike, sima, bada au wali
Hatimaye ateuke, kwa viliwa vya samli
Mwanadamu simwamini, afadhali mnyama lumbwi.

Mwanadamu umjenge, awe mwenye kutajika
Mambo yake uyapange, ukawa wahangaika
Uwashe wake muwenge, uhakikishe wawaka
Nao mkono umuunge, vyake viwe vyaungika
Dhorubani umkinge, asipate kudhurika
Mara atakusahau, wema wako kafukia

Mwanadamu mpe cheo, kuwa akutumikie
Amani yako umpeo, fanaka uirajue
Kwake iwe kimbilio, wamini akukwamue
Mwisho takuwa kilio, shika sikio ujue
Ndio wake mwelekeo, yuauma avuvie
Mwanadamu mgeuze, pande zote umtizame

Mwanadamu mfadhili, kwa kila lililo jema
Pasiwe hata dalili, ya kwake kukosa wema
Viteko siwe akali, kumbizo zikaterema
Binadamu takudhili, dhili zako kazitema
Licha ya zote jamili, mwanadamu si muema
Mwanadamu ni mtu, lakini nusu mnyama

Maswali

a) Shairi hili ni la aina gani? Fafanua jibu lako. **(alama 2)**
b) Eleza usaliti unaoendelezwa na mwanadamu kwa mujibu wa shairi hili. **(alama 4)**
c) Tia shairi hili katika bahari tatu tofauti kwa kuzingatia; **(alama 3)**

i. Mpangilio wa maneno
ii. Mpangilio wa vina
iii. Mgao wa mishororo

d) Eleza muundo wa shairi hili. **(alama 4)**
e) Bainisha toni ya shairi hili. **(alama 1)**
f) Eleza mbinu mbili ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa kwanza. **(alama 2)**
g) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. **(alama 4)**

7. Nimeyaandika maneno haya
Kwa niaba ya:
Mamilioni wasio malazi
Wabebao vifurushi vilivyo wazi
Wazungukao barabarani bila mavazi
... milki yao ya maisha.
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki
Wiki baada ya wiki
leo sumu au spaki
leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
wale mayatima wa maskini
wazungukao mapipani
kila pembe mjini
kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza
walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
polepole wakijiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana watazama
wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
Kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
bila ya mtu kuona
kama kwamba sote tu vipofu,

Na kwa niaba yetu sote;
Tuliofungwa vifungoni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni, machoni
Tuliotiliwa sumu, malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini
ili 'maendeleo'
yaendelee kwenda njiani
huku yakitema machicha ya roho zetu.

Maswali

a) Hili ni shairi la aina gani? Fafanua . **(alama 2)**
b) Bainisha toni ya shairi hili . **(alama 2)**
c) Tambua aina tatu za urudiaji zinazojitokeza katika shairi. **(alama 3)**
d) Huku ukitoa mifano eleza namna mtunzi alivyotimiza arudhi za kishairi. **(alama 3)**
e) Eleza matumizi ya. **(alama 3)**

i. Mistari mishata
ii. Mistari kifu
iii. Tasfida

f) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. **(alama 2)**
g) Tambua aina za taswira katika shairi hili. **(alama 2)**
h) Mshairi anazungumza kwa niaba ya watu mbalimbali. Jadili. **(alama 4)**

SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI

(a) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Hadithi ya Jabari inasimuliwa na jamii nyingi. Jabari alizaliwa kashika mkuki mkononi. Mawio ambayo kilio chake,ambacho kwa kweli kilikuwa mngurumo,kilipasua anga,nyota kubwa ilianguka kutoka mbinguni.ulimwengu mzima ulitetemeka kwa kutwaa giza.

Hata kabla mama mtu hajampa ziwa,Jabari alikuwa amevuvumka na kuwa ghulamu wa miraba minne. Haikuchukua muda,hata vita kati ya jamii ya Sule na Suna vikaanza;kikosi cha Sule cha wapiganaji mia moja kikawajia vijana wa Suna kwa sime na nyuta. Jabari aliwakabili kwa konde moja pekee,akakirambisha dongo kita kizima.

i. Bainisha kipera cha utungo huu **(alama 1)**

ii. Toa sababu mbili kuthibitisha jibu **lako** **(alama 2)**

iii. Eleza manufaa matano ambayo jamii itapata kwa kurithisha kipera hiki kwa vizazi vijavyo **(alama 5)**

(b) Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali.

Ndimi Mwimo mdumishaji ukoo
Ndimi ndovu mtetemesha ardhi
Aliyepigana vita,ukoo kuauni
Ziliporindima zangu nyayo
Adui alinywea,mafahali na mitamba akatukabidhi
Kwenye msitu sikuwa na kifani
Paa na hata visungura
Vilijikabidhi kwangu
Kwa kuinusa tu mata
Nani aliyewahi
Ngomani kunipiku? Makoo hawakunisifu,wakalilia nikaha?
Kwenye nyanja za michuano
Nani angethubutu,ndaro kunipigia?
Sikuwabwaga chini, kwa yangu maozi,hata kabla hatujavaana?

i. Hii ni sifo gani? **(alama 1)**

ii. Bainisha shughuli **moja** ya kiuchumi na **moja** ya kijamii zinazoendelezwa na jamii inayosawiriwa na utungo huu **(alama 2)**

iii. Eleza mambo **matano** ambayo yanaweza kuzingatiwa ili kufanikisha uwasilishaji wa uungo huu **(alama 5)**

(c) Eleza faida **nne** za matumizi ya nyimbo katika uwasilishaji wa ngano (**alama 4)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TANO)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Andika jina lako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Andika insha **mbili**. Insha ya **kwanza** ni ya **lazima.***

c) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya tatu zilizobakia.*

d) *Kila insha isipungue maneno **400***

e) *Kila insha ina alama **20***

f) *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

1. LAZIMA

Wewe ni mwenyekiti wa vuguvugu la Tazama Afrika. Andika mazungumzo yako na mawaziri wawili kutoka mataifa yaliyoendelea barani kujadili matatizo yanayokumba bara la Afrika.

2. Uhuru unaopewa vijana leo katika nchi yetu una madhara zaidi kuliko faida.Jadili.

3. Maji ukiyavulia nguo, yaoge.

4. … Nilijitoa kafara na msaada wangu ukazaa natija kwa wengi.

KCSE 25

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TANO)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali* ***yote****.*

d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

e) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

1. UFAHAMU (Alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Mengi yamesemwa kuhusu utiifu. Ukweli ni kuwa,watu wengi hudhani kuwa maisha yangekuwa mazuri zaidi ikiwa kila mtu angeruhusiwa kufanya atakavyo. Kulingana na mimi, ni makosa kufikiria hivyo madhali mienendo isiyodhibitiwa na sheria ni kiini cha vurugu na ukiukaji wa sheria nchini. Hebu fikiria hali ingekuwa vipi ikiwa mwendeshaji pikipiki angeiendesha kulia na kushoto katikati ya barabara na kupuuza sheria za trafiki. Hali kama hii huweza kusababisha msongamano mkubwa wa magari mjini, hivyo kuwafanya watu wachukue muda mrefu kabla ya kufika waelekeapo. Kutengenea au shwari kwa mambo hutokana na kila mtu kufuata kanuni zote zilizowekwa.

Kila mtu hana budi kuelewa kuwa utiifu si udhaifu au woga. Ni hali ya kutambua kuwa kutii utawala wa kisheria huhakikisha kuwa kuna muumano na utangamano wa kijamii. Utiifu una maana ya kufanya yanayotarajiwa. Vilevile utiifu una maana ya kutambua na kukubali kuwa kufanya matendo mema ni bora zaidi kuliko kutekeleza jambo au matendo ya kibinafsi tu. Kwa hakika, ni vyema kutafakari kuhusu tunayoambiwa tufanye na wenzetu au hata watu wengine. Hatufai kufuata kila maagizo tunayopewa bila kuyatathmini vizuri. Mathalan; ikiwa mtu atakuambia ujihusishe na ujambazi, unafaa kuwajibika kwa kukataa kufuata amri ya aina hiyo hata kama mtu huyo ana mamlaka makubwa namna gani. Maagizo au kanuni tunazofaa kufuata au kutii ni zile zenye maana;yaani, maagizo au kanuni zenye manufaa.

Je, kwa nini watu wengi huona vigumu kuwatii walimu, wazazi au watu wenye mamlaka? Sababu kuu ni kuwa wao ni wabinafsi. Wao huchochewa na kufanya kutotii kutokana na lengo la kutenda mambo yatakayowafaidi; yale mambo yatakayowasaidia kutimiza matakwa yao ya kibinafsi. Kiini cha mioyo ya watu kama hawa kukaidi maagizo na kanuni maishani, hutokana na ukweli kuwa utiifu humlazimu mtu kupuuzilia mbali matakwa ya kibinafsi na mara nyingi hujumuisha kutekeleza anayoambiwa afanye na wengine.Hata hivyo,ikiwa watu kama hawa watazingatia manufaa ya utiifu, watatamani kupalilia utiifu kama mojawapo wa maadili maishani mwa binadamu.

Ukweli ni kuwa katika maisha ya kila siku, tunatii kanuni nyingi bila kufahamu au kujua. Hakuna mtu,kwa mfano, anayetulazimisha kuzingatia lishe bora au kufuata maagizo ya daktari. Wengi wetu huhudhuria shule au kwenda kazini kwa wakati unaofaa bila kushurutishwa. Ikiwa kwa mfano una gari unalomiliki, hakuna anayekuarifu kulipeleka kwenye gereji likatengenezwe au likarabatiwe. Hebu jiulize hapo ulipo; je, kwa nini watu hufanya mambo kama haya bila kuagizwa au kukahiriwa?Ukweli ni kuwa,tendo lolote lile la kutotii au kutotekeleza yanayohitajika litakuwa na matokeo mabaya au hata ya kuhatarisha maisha ya watu. Kwa hivyo, utiifu huleta utangamano na humfanya mtu kuishi bila mfadhaiko wowote.

Kiini cha vijana kukosa kukubali na kufuata kanuni na taratibu zilizowekwa hutokana na ukweli kuwa, wao huziona kama zilizopitwa na wakati. Ni ukweli kuwa si mambo yote wanayotuhimiza wenzetu kufanya yana mantiki. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia **matilaba** ya kuyatenda badala ya kuyapuuza. Zaidi ya hayo, tunaosema kuwa wana mawazo yaliyopitwa na wakati wanaweza

kuwa na **tajriba pevu** na umaizi au utambuzi mkubwa wa mambo kutuzidi. Vijana wengi wanaokaidi maagizo ya wazazi wao huteseka maishani. Inafaa ieleweke kuwa hata kama wazazi na walimu wanaweza kuonekana wakali na wasiozingatia kila tutakalo, daima wao hututakia mazuri na huwa na malengo mema kuhusu maisha yetu.

Baadhi ya matatizo ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa tunayopitia au kukumbana nayo hutokana na kutotii sheria. Hali ya kutotii sheria au hata kanuni zilizowekwa huwafanya baadhi ya watu hukataa kulipa ushuru, wengine kubadhiri au kuhariji mali ya umma au kujihusisha na vitendo vya kifisadi; hali ambayo huinyima nchi yetu mapato au maduhuli. Vitendo kama hivi huifanya nchi kurudi nyuma kimaendeleo. Kutotii sheria husababisha madhara mengi kwa mtu binafsi; watu wengi huharibu maisha yao kwa kupiga mtindi kupindukia, kuvuta sigara au hata kasumba na kujihusisha na mapenzi kiholela. Ukweli ni kuwa wao hujua hatari itokanayo na mienendo kama hiyo. Kabla ya kuvunja sheria au kupuuza kanuni zozote zile ni muhimu kufikiria kuhusu matokeo yake kwanza. Aidha ni vyema kugundua kuwa hakuna mtu yeyote yule anayeweza kuepuka athari za uasi.

Maswali

a) Ipe taarifa hii anwani mwafaka. **(alama 1)**

b) Je, ni kwa nini watu hawawezi kuruhusiwa kufanya watakavyo? **(alama 2)**

c) Eleza maana ya utiifu kwa mujibu wa taarifa hii**.** **(alama 2)**

d) Eleza sababu inayowafanya watu kuasi. **(alama 1)**

e) Kwa nini tunafaa kusikiliza wanayotuambia wazazi na walimu wetu hata kama hatukubaliani nayo **(alama 2)**

f) Eleza manufaa matatu ya utiifu. **(alama 3)**

g) Fafanua matokeo mawili ya uasi kulingana na taarifa hii**.** **(alama 2)**

h) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika taarifa: **(alama 2)**

(i) matilaba

(ii) Tajriba pevu

2. UFUPISHO (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali uliyoulizwa.

Suala la uzito wa mwili ni mojawapo wa masuala ambayo yamewashughulisha wataalamu katika miaka ya karibuni.Tatizo hasa sio uzito wa mwili wenyewe bali ni uto ambao aghalabu unaenda sambamba na uzito huo. Uzito wa mwili ni kipimo cha mwili mzima ukihusishwa na misuli ya mwili. Zipo njia mbali mbali zinazoweza kuchangia uzito wa mwili.Kimsingi, hutokana na kalori za ziada ambazo mwili huo huwa nazo. Kalori hizi hutokana na hamirojo , mafuta au hata proteini.Kalori hizi huhifadhiwa na mwili katika seli maalum (tishu za mafuta). Asilimia 50 ya jumla ya mafuta au uto wa mwili huhifadhiwa chini ya ngozi ya mwili. Ile nyingine huzunguka viungo mbalimbali vya mwili kama vile moyo.

Uto una faida kadha mwilini.Kwanza,ni msingi muhimu na mkuu wa nishati za mwili. Uto unapochomwa na mwili huvyaza oksijeni ya ziada ambayo husambazwa kwenye seli za mwilini.Oksijeni hii inapoungana na atomu za kaboni na haidrojeni huwa chanzo cha joto mwilini.Uto pia hukinga mifupa na viungo vya mwili,huhifadhi au kuukinga mwili hasa dhidi ya baridi na huwa nyenzo muhimu hasa kwa mwenye matendo ambayo yanahitaji matumizi ya nguvu.Licha ya faida zake hizi,uto huwa na matatizo.Kimsingi, uto mwingi unaweza kuwa chanzo cha unene au utipwatipwa wa mwili ambao unaweza kuwa chanzo cha fedheha kutokana na unene.Uto pia unahusishwa na hali kadha za kimatibabu kama kufupisha uwezekano wa maisha kuwa marefu.Yapo maradhi ambayo yanahusishwa kwa kiasi kikubwa
na unene wa mwili,unaotokana na uto ,kama maradhi ya moyo,bolisukari,ugonjwa wa ini na matatizo ya figo.

Vyanzo vya tatizo la uto hutofautiana.Wataalamu wanaamini zipo chembechembe zinazorithiwa ambazo huweza kuwa chanzo cha ulaji unaopiku ambao unaweza kusababisha unene. Hata hivyo, ingawa msimbojeni unaweza kuwa chanzo hiki,ulaji usiozingatia hatari kama hizi huchangia pakubwa. Vipo baadhi ya vyakula ambavyo vina mchango mkubwa katika kulivyaza tatizo la unene.Vyakula hivi ni vile vinavyojulikana kama vyakula chapwa vikiwemo kaukau na viazi vya kutafuna.Aidha, vinywaji huweza kuwa vyanzo vya kalori ambazo huishia kuwa chanzo cha uto mwingi mwilini.Ili kupambana na tatizo la unene, pana haja ya kuhakikisha kuwa tunapunguza ulaji wa baadhi ya vyakula.Hivi ni vyakula vyenye mafuta mengi.Kwa mfano,mtu wa wastani anaweza kukung'uta kalori 300 kwa saa afanyapo mazoezi.Mazoezi haya husaidia viungo vingine vya mwili kama vile moyo kwa kiasi kikubwa.

Hizi ni njia nyepesi ambazo zinaweza kutumika kupunguzia uzito kuliko matumizi ya madawa au njia nyingine za kihazigi ambazo huweza kuwa na matokeo hasi kwa mwili.

Maswali

a) Fupisha ujumbe wa aya ya kwanza kwa maneno 50 (Alama 5;1 ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

b) Eleza masuala ambayo mwandishi ameibua katika aya ya pili kwa maneno 50.

(Alama 7;1 ya mtiririko)

Matayarisho

Jibu

c) Fupisha ujumbe wa aya ya tatu kwa maneno 40 **(Alama 3)**

Matayarisho

Jibu

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Andika sauti zenye sifa zifuatazo: **(alama2)**

(i) kipasuo **sighuna/hafifu** cha ufizi

(ii) irabu ya mbele juu

(b) Neno 'kwapa ' liko katika **ngel**i gani? **(alama 1)**

(c) Tofauitisha sentensi zifuatazo **kimaana** **(alama 2)**

(i) yote yameliwa .

(ii) yoyote yameliwa.

(d) Andika neno moja lenye **mofimu** zifuatazo: **(alama 3)**

Nafsi ya pili wingi , hali timilifu ,yambwa,mzizi, kauli tendea, kiishio

e) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya **ukubwa wingi** **(alama 2)**

Ng'ombe huyo alinunuliwa mbali na mji ule mkuu.

(f) Ka imetumika kuleta maana gani katika sentensi zifuatazo : **(alama 2)**

(i) Rais kazuru mbuga za wanyama

(ii) Mgeni kaingia humu ndani kupumzika.

(g)i) Kirai ni nini? **(alama 1)**

(ii) Bainisha **aina** za virai vilivyopigiwa mstari**.** **(alama2)**

Yule mzembe alipigwa na mwanawe.

(h) Tofautisha maana ya **jozi** ifuatayo ya maneno**.** **(alama 2)**

i.ridhi ……

ii.rithi…….....

(i) Eleza matumizi yoyote mawili ya alama ya **kistari kirefu** katika sarufi ya Kiswahili.**(Alama 2**

(j) Ainisha **vihusishi** katika sentensi: (Alama 2)

i) Hawa watatumia pesa nyingi kushinda wale.

ii) Darasa nzima litatuzwa na mwalimu wao.

(k) Sahihisha sentensi zifuatazo . (alama 2)

i) Kile kitabu kilipasuka ni changu .

ii) Mtu mwenye ameanguka ni ndugu yangu.

(l) Nyambua vitenzi hivi katika kauli ya **kutendesha**, kisha uvitungie sentensi . **(alama 2)**

i) oa…….

ii) la……

(m) Mkunga ni mtu mwenye maarifa ya kushugulikia wanawake wajawazito wakati wa kujifungua . Tunga sentensi mbili zitakazodhihirisha maana nyingine mbili za neno hili.

(alama 2)

(n) Kwa kutungia sentensi, dhihirisha matumizi ya '**kwa**' ili kuonyesha : **(alama 2)**

i) sababu / nia

ii) Jinsi ya kutenda/kitendo kilivyofanywa

o) Changanua sentensi hii kwa kielelezo cha **matawi.** **(alama 4)**

Muumini atakayeshtaki ni msaliti mkubwa sana.

(p) Bainisha shamirisho kitondo katika sentensi :

Lola alimpasulia nyanya kuni**.** **(alama 1)**

(q) Tumia viashiria vya **kutilia mkazo** katika sentensi zifuatazo: **(alama 2)**

c) Wema----------ulisababisha atuzwe.

ii) Polisi waliwafuata ---------- walikoenda.

(r) Andika **kitenzi** kinachotokana na neno **:** **(alama 1)**

mfuasi

(s) Eleza **tofauti** baina ya sentensi hizi**:** **(alama 2)**

i) Ningekuwa na pesa ningenunua pikipiki.

ii) Ningelikuwa na pesa ningelinunua pikipiki.

(t) Andika **methali** inayoafiki maelezo yafuatayo**:** **(alama 1)**

Mwanadamu hakosi ila. Aliyekamilika ni Mungu pekee.

4 ISIMUJAMII **(Alama 10)**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Jumamosi ,Disemba 26,2020

Ananyoa kwa shoka

Na Wangu kanuvi

Julius Mwangi, 24, ni kinyozi ambaye amevuma kwa kunyoa wateja wake. Kinyozi huyu aliamua kuanza kutumia shoka miezi mitatu iliyopita baada ya kutambua kuwa ipo haja ya kuwa na njia ya pekee ya kuwanyoa watu.

"Nimebobea katika kutumia mashine lakini nilitaka njia mbadala na ya kipekee ya kuwanyoa watu…"

Wateja wake hujaa kibao katika kibanda chake kilicho katika mtaa wa Tayari, kaunti ya kiambu…

a) Bainisha sajili ya makala haya**.** **(Alama 2)**

(b) Eleza sifa zozote **sita** za sajili hii kwa kurejelea makala haya**.** **(alama 6)**

(c) Fafanua sifa nyingine **mbili** za sajili hii ambazo zingejitokeza katika makala haya. **(alama2)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TANO)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

(a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
(c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*
(d) *Swali la kwanza ni la* ***lazima.***
(e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki;yaani:Riwaya, Tamthilia,,Hadithi Fupi na Ushairi.*
(f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka sehemu moja.*

Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	

SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI

SWALI LA LAZIMA

1. *Soma kifungu kilicho hapo juu kisha ujibu maswali yafuatayo.*

Ndimi kisoi, dume la ukoo mtukufu wa kifalme.
Ukoo wa kipekee, utukukao kwao ubingwa
Ubingwa wa kucheza ngoma
Uhodari wa kusakata rumba
Hakuna abishanaye name, uwanjani
Mabinti wang'ang'ania kusakata name
Bingwa kisoi aingia nyanjani

a) Tambulisha kipera cha maghani kinachojitokeza katika kifungu hiki. **(alama 2)**

b) Kipera ulichotaja katika (a) ni cha utanzu upi? **(alama 1)**

c) Fafanua sifa tano za kipera hiki. **(alama 5)**

d) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. **(alama 2)**

e) Ngomezi ni nini? **(alama 2)**

f) i) Fafanua dhima tano za ngomezi. **(alama 5)**

ii) Taja mifano yoyote mitatu ya ngomezi za kisasa. **(alama 3)**

SEHEMU YA B: TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA

Jibu swali la 2 au 3

2. "Sisi tuna bahati ya mtende mtoto kutusikiliza na kutupiga jeki."

a) Tambua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Kwa kutoa mifano minne, eleza vipi mrejelewa amewapiga jeki. **(alama 4)**

c) Taja na ufafanue mbinu iliyojitokeza katika dondoo. **(alama)**

d) Fafanua sifa sita za mnenewa. **(alama 6)**

e) Tambua na ufafanue maudhui yoyote mawili yanayojitokeza katika dondoo. **(alama 4)**

3. a) Kwa kurejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha, eleza namna mwanamke alivyosawiriwa. **(alama 10)**

b) Angazia kwa mifano mwafaka namna ambavyo maudhui ya utu yanavyojitokeza katika tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama 10)**

SEHEMU YA C: RIWAYA YA NGUU ZA JADI

Jibu swali la 4 au 5

4. a) Riwaya ya Nguu Za Jadi ni kioo cha nchi za Afrika. Fafanua. **(alama 20)**

5. …….. alifanya kazi yake kwa moyo wa kujituma. Hakunung'unika pale kazi zilipomzidi bali alitabasamu na kuchapa kazi. Matatizo ya nyumbani yalipomzonga, hakukosa kufika kazini. Alidunduiza vijisenti vichache ambavyo alikuwa akipokea kama ujira wake akaweza kuwasomesha wanawe.

a) Tambua muktadha wa dondoo. **(alama 4)**
b) Fafanua sifa nne za msemewa. **(alama 4)**
c) Jadili changamoto za kikazi zinazojitokeza katika riwaya ya Nguu Za Jadi. **(alama 12.**

SEHEMU YA D: HADIDHI FUPI: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

Jibu swali la 6 au 7

Harubu ya maisha na Paul Ng'ang'a Mutua

6. Muda si mrefu, chakula kilikuwa tayari. Nilimlisha Mercy. Akalala. Akaniachia mzigo wa kupambana na njaa yangu mwenyewe. Lakini mtu anawezaje kula chakula mkewe akiwa njaa, tena hapo hapo katika chumba kimoja? Na kuongeza msumari wa moto kwenye kidonda kibichi, chakula kina harufu na muonjo wa mafuta taa! Hii kweli ndiyo maana ya kila msiba kuandamana na mwenziwe! Nilishindwa kula kabisa. Niliangalia mahali anakoweka sukari Mama Mercy. Mkebe ulikuwa shinda. Nilihisi machozi yanayotunga kwenye ncha za macho lakini nikajikaza kiume.

a) Tambua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**
b) Tambua mbinu zozote zinazojitokeza katika dondoo. **(alama 6)**
c) Tambua maudhui yanayojitokeza katika dondoo. **(alama 2)**
d) Eleza sifa na umuhimu wa msimulizi. **(alama 6)**
e) Kwa kurejelea dondoo eleza maana ya kauli "msiba kuandamana na mwenziwe." **(alama 2)**

(Mzimu wa kipwere na Yussuf Shoka Hamad.)

7. …….. mara nilisikia sauti ya mtu ikiimba ule wimbo wa mzimu ikiashiria kuomba ruhusa ya kuingia, kusikia vile, nikajua sasa nitafumaniwa na wahusika na bila shaka nitakabiliana na hukumu ambayo sitasahau milele iwapo nitatiwa nguvuni. Kwa kuhofia kupatwa na mnadhaa au idhara, nikaizima tochi yangu, tap! Kisha bila ya kupepesa macho mara mbili, nikajivurumisha uvunguni mwa kile kitanda chenye matendegu marefu kama miguu ya punda kirongwe nikakaa kimya na kutulia kama ninyolewaye! Wale watu wawili waliimba wimbo wao wa kawaida. Mara tu walipomaliza na kutambuana, wote waliingia mle ndani ya mzimu. Siku hii kama kawaida, walioingia mle mmoja alikuwa mwanamke na mwingine mwanaume. Bila ya kupoteza muda, Yule mwanaume alianza kwa kusema kwa sauti ambayo niliitambua kuwa ya Salihina. Hapo masikio yangu yalivuka kichwa kwa kumwogopa bwana yule aliyetisha sana, yakawa kama masikio ya sungura anayeiba mazao shambani.

a) Mwandishi katika kifungu hiki ametumia mbinu ya ulinganisho kwa mapana. Tambua mbinu hii na utaje mifano yoyote mitatu. **(alama 3)**
b) Tambua mbinu nyinginezo za lugha zinazojitokeza katika kifungu. **(alama 4)**
c) Fafanua sifa zozote tano za Salihina kama zinavyojitokeza katika hadithi ya Mzimu wa Kipwerere**.** **(alama 5)**
d) Fafanua umuhimu wa msimulizi. **(alama 2)**
e) Eleza umuhimu wa mandhari ya Mzimu wa Kipwerere. **(alama 6)**

SEHEMU YA E: USHAIRI

8. Soma shairi kisha ujibu maswali yafuatayo.

Wanafunzi sikilizeni, niwape wangu wasia
Mkiwa mtihanini, muweze kuzingatia,
Nataka mtambueni, msije mkajutia
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Kufanikiwa kitaka, watii nao walimu
Sielekeze dhihaka, kwao wao ni muhimu,
Kwauliza mwahitajika, maswali yalo magumu,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mrauke na mapema, msome kwa tumaini,
Msije nyie kukwama, kwenye wenu mtihani,
Muweze rudia vyema, mlofunzwa awalini,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu,

Umoja ni nguvuni, mwafaa mfahamuni,
Jiunge na makundi, masomo mujadilini,
Na lile lilo gizani, takuja kulionani,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Ilopita mitihani, kwa chudi irudieni,
mpate na taswirani, ya ule ulo mwishoni,
Ya ziada kazini, ifanye sizembeeni,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mwelewe sana vyema, yaliyo mtaalani,
Msije mkandama, cha mtihani chumbani
Mgongeni ndipo vyema, sije mkapoteani,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Mkiwa madarasani, kelele muepukeni,
Sije mkapotezani, muda wenu masomoni
Neneni na vitabuni, vitakuja walipani,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Michezo sipuuzeni, kwayo nyie burudika,
Nishati mtapatani, kifurahia michezo,
Mazoezi eleweni, ni muhimu kwa ubongo,
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

Nimefika kaditama, kuwelekeza moyoni,
Yafwateni hayo mema, mfaulu mtihani,
Ni upuzi msiseme, muda wangu potezeni
Kwa bidii durusuni, mtihani mfaulu

a) Eleza mawaidha yanayotolewa kwa wanafunzi kuhusu namna ya kujitayarisha vyema kwa mtihani. **(alama 5)**
b) Eleza umbo la shairi hili. **(alama 4)**
c) Eleza mbinu tatu zilizotumiwa katika shairi ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi. **(alama 3)**
d) Taja mifano ya tamathali mbili zilizotumiwa katika shairi hili. **(alama 4)**
e) Eleza toni ya shairi. **(alama 1)**
f) Andika ubeti wa pili kwa lugha tutumbi/ nathari. **(alama 3)**

KCSE 25

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA SITA)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

- *Andika insha mbili.*
- *Swali la kwanza ni la lazima.*
- *Kila insha isipungue maneno 400.*
- *Chagua insha nyingine moja kutoka kwa hizo tatu zilizosalia .*
- *Kila insha ina alama 20.*
- *Kila insha iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	ALAMA
1	
JUMLA	

Ukihitaji majibu, wasiliana na Bw. Isaboke - 0746 222 000 / 0742 999 000

1. <u>LAZIMA</u>

Umekuwa msaidizi wa mbunge wa eneobunge la Mfanisi. Ungependa mbunge huyu apate nafasi ya kuwa mbunge wa eneobunge hili tena. Andika wasifu utakaochapishiwa wanaeneobunge ukieleza mchango wake katika sekta mbalimbali za eneobunge hilo.

2. Eleza namna wananchi wanavyoonyesha uzalendo kwa nchi yao.

3. Andika kisa kitakachoafiki maana ya methali: Mwota mchana hukosa mali na wana.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo.

Mahakama ilikuwa imejaa furifuri. Jamaa na marafiki walikuwepo. Nilisimama kizimbani. Mashahidi walikuwa wamekamilisha kutoa ushahidi wao. Jaji aliinua uso wake akaniangalia kwa ukali kisha**...**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA SITA)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2 ½

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo ya Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

(a) *Andika jina na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

(b) *Jibu maswali yote.*

(c) *Majibu yaandikwe katika nafasiulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

(d) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MITAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Ukihitaji majibu, wasiliana na Bw. Isaboke - 0746 222 000 / 0742 999 000

1. SEHEMU YA A: HAMU YA HAMO

Hamo alirauka majogoo kuanza maandalizi ya mapema. Hakutaka kukosa sherehe ya sikukuuu ya Jamhuri kama alivyokuwa amekosa ile ya mashujaa. Siku hiyo alipofika kwenye langa kuu la uga ambako sherehe zilitendeka, askari mmoja mwenye kofia nyekundu, miwani myeusi na bunduki kifuani alimnyoshea kidole na kumwambia, “Kwenda nyumbani kijana . Unafika hapa baada ya rais kuingia kwani wewe ni rais wa Marekani?” swali hilo lilimsumbua kwa siku kadhaa, akawachukia maafisaa wa usalama, na likamtwanga kwa nguvu sana asubuhi ya Jamuhuri. Alimaliza maandalizi na kupiga milundi uwanjani.

“Una kitambulisho?” Hamo aliona ajibu kwa kukitoa na wakati huu afisaa wa usalama alimruhusu aingie bila maswali zaidi. “Huyu amechoka sana. Hata sare yake ya bluu imechujuka jamani!” Hamo alijiambia akiingia uwanjani. Uwanja ulikula watu bila kushiba, kwani kulikuwa na mapengo ya hapa na pale kama kinywa kilichong’oka meno. Bw. Hamo alitafuta nafasi karibu na jukwaa lakini katika sehemu iliyotengwa “wananchi wa kawaida.” Hayo maneno matatu yalikuwa yamemsumbua Hamo akijiuliza mbona wale wengine walijiona wasiokuwa wa kawaida. Hata, hivyo, hakutaka fikra hizo ziboronge hamu yake ya siku.

Basi, bendi ya wanajeshi ilisikika na kiongozi wao akawa na fimbo fulani aliyoizungusha mkononi hapa na pale na wakati mwingine kuirusha juu, akakimbi kuidaka kabla ya kugusa ardhini. Vikosi vitatu vya wanajeshi waliovalia sare za rangi tatu tofauti: nyekundu, bluu na nyeupe viliingia kwa kupendeza. Kila mwanajeshi alikuwa ameishika bunduki yake kwa mkono wa kulia, na kuurusha mkono wa kushoto mbele na nyuma kana kwamba hawakupendezwa na mikono yao, ila mikono hiyo ilirushwa kwa pamoja na kuunda safu nzuri, ungedhani mikono hiyo iliunganishwa na kufungwa. Kiongozi mmoja aliyekuwa na kitara mkononi alisimama katikati na kupaaza sauti kubwa ilyosikika kanakwamba alikuwa na kipaza sauti. Kwa pamoja wanajeshi waliichapa miguu yao chini kwa nguvu kana kwamba wakimuua nyoka na kutulia tuli! Haya yalimshangaza Hamo kwani alisikia ni kama kiongozi alilia “Hooooo ho!

Muda ulizidi kuyoyoma na punde si punde rais aliingia kwenye gari lililompa uwezo wa kuwasalimu wananchi. Bw. Hamo alipiga kelele kama wananchi wengine na rais alipopita karibu naye, Bw. Hamo alimwambia “Nakupenda rais!” Rais alitabasamu na kuangalia upande huo huku akiweka viganja vyake pamoja na kuinua juu, ishara ya kwamba, “tu pamoja” , jambo lililomfurahisha Hamo aliyetabasamu nusura aonyeshe magego yake. Burudani iliendelea pale na wanajeshi wakapendeza kwa vioja na viroja vyao; mara waangalie mbele, mara wapinduke ghafla kama walioumwa na siafu, mara wasukumane mikono na kujipanga vizuri zaidi, mara wawe wawili wawili, waunde ruwaza za kupendeza; haya yote baada ya kilio cha yule kiongozi ambacho Hamo hakusikia kikibadilika pahubwa, kwani kilicheza “Hoooho” na maneno mengine ambayo Hamo aliamini kuwa hayakuwa kwa mojawapo ya lugha alizozielewa.

Kilele cha siku kilikuwa hotuba ndefu ya rais ya Kiingereza na japo Hamo hakung’amua chochote, alihisi kuwa ilikuwa siku iliyofana, na kwa kuwa rais alimjibu salamu zake kwa heshima kubwa, alijiona kuwa shujaa. Muhimu zaidi alikula yamini kuwa mwanajesi, ambaye ama awe Yule wa “hooooho!” au Yule wa kurusha na kudaka fimbo kabla ifike ardhini.

MASWALI

a) Mbona Hamo aliamka wakati wa majogoo **(alama 2)**
b) Tofautisha maafisa wawili waliotajwa kwenye kifungu kihulka. **(alama 4)**
c) Eleza sifa tatu za rais kulingana na taarifa. **(alama 3)**
d) Mbona Homa alikuwa yamini kuwa mwanajesi. **(alama 1)**
e) Thibitisha suala la utabaka kwa kurejelea kifungo. **(alama 1)**
f) Toa mfano mmoja wa matumizi ya mbinu ya mbinu ya uhuishaji kutoka kwenye kifungo.**(ala 1)**
g) Eleza maana ya maneno haya kulingana na taarifa: **(alama 3)**
i) uga
ii) boronga
iii) kula yamini

2. UFUPISHO

Soma kifungo kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Mirundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji wake ni tisho kubwa kwa siha ya umma pamoja na mazingira . Hii ni kwa kuwa taka huwa ni makaazi ya wadudu na wanyama waharibifu kama nzi, mbu, kombamwiko na panya ambao hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye dhamani. Maji taka nayo, pamoja na mifuko ya sandarusi huwa mastakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa mbalimbali.

Mifuko ya sandarusi ina madhara kwa kuwa huziba mitaro ya maji na kuzuia upitaji wa maji. Madhara hutokeza wakati wa mvua za ngarika. Maji haya husababisha mafuriko ambayo huleta hasara ya mali na wakati mwingine ya uhai. Fauka ya haya, mifuko hii huwasakama tumboni wanyama sio wa nyumbani tu, bali wa porini na majini.

Kwa sababu ya hatari zitokanazo na taka, pana haja kutafuta njia na teknolojia ya kwanza kukabiliana na tatizo hili ili kuyatunza mazingira na siha ya umma. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na raslimali ili kupunguza uzalishaji wa taka. Matumizi ya bidhaa kwa njia ya ubadhirifu huwa chanzo cha uzalishaji wa taka kwa wingi. Kwa mfano, maji ni raslimali ambayo imeendelea kutumiwa kwa ubadhirifu na hiyo uzalishaji maji taka kwa wingi. Raslimali hii inaweza ikatumiwa kwa njia endelevu. Kwa mfano, badala ya kutumia bafu ya nyumbani kuoga mtu anaweza kutumia maji ya karai.

Watu wengi huchukulia taka kuwa kitu kisicho na manufaa yoyote. Hawajui kuwa kwa kutumia teknolojia endelezi, taka nyingi zinaweza zikageuzwa na kuwa na manufaa mengi. Vijana wadogo sehemu za mashambani wanahitaji pongezi kwa kuwa na utambuzi huu. Wengi, kwa kukosa hela za kununulia mipira ya viwandani, hutumia teknolojia endelezi ambapo taka hugeuzwa na kuwa na manufaa.

Baadhi ya wananchi wenye ubunifu nao wameanzisha miradi ya kuzoa takataka kutoka majumbani mwa watu kwa ada kisha huzipeleka taka hizi kule zitakakobadilishwa ili ziwe na manufaa. Mifuko na mabaki ya sandarusi hupelekwa katika viwanda vinavyotengeneza bidhaa za plastiki kama matangi, mitungi, sapatu na champali. Taka hizi huwa malighafi ya kutengeneza bidhaa nungine.

Taka za chupa na chuma nazo huuzwa katika viwanda vinavyozigeuza kuwa na manufaa tena. Taka za karatasi hutumiwa kutengeneza bidhaa kama vitabu, katoni, shashi za chooni na magazeti.

Taka zinaweza pia kugeuzwa kuwa zenye faida kwa kuzitumia kufanyia mboji. Ni muhimu kutambua kuwa si kila aina ya taka inaweza kutumiwa hapa. Taka zinazoweza kufanyiwa mboji ni zile ambazo

huoza kwa haraka, kama vile: mabaki ya vyakula mboga na matunda. Kwa sadfa, hizi ndizo taka zinazozalishwa zaidi siku na hasa sehemu za mjini katika maeneo ya biashara kama mikahawa na hospitali. Mtu akiwa na nafasi anaweza kuchimba shimo ambalo atafukia taka ili kutengeneza mbolea. Hii ni njia isiyodhuru mazingira na yenye manufaa kemkem. Kwanza, kugeuza taka ambayo inaweza kuwa hatari na kuifanya iwe yenye manufaa. Kwa hivyo hutatua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokana na mirundiko ya taka. Mchanga nao hufaidika kupata virutubishi. Mbolea kama hii inaweza ikatumika kukuzia mboga au maua katia bustani.

Maji taka, hasa yanayotumika kuosha vyombo, nayo yanaweza kutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani za maua. Maji taka haya yanahitaji kutayarishwa njia mahususi ya kuyaelekeza katika mashamba haya baada ya kutumiwa.

Anglalabu watu wengi wana mazoea ya kuchoma taka. Ni kawaida kupata matanuri ya kuchomea taka katika baadhi ya mitaa, shule na hospitali. Badala ya kupoteza moto huu bure bilashi, inawezekana pakawekwa birika kubwa au tangi la chuma ambalo litatuma moto huo kuchemsha maji. Maji haya yanaweza yakatumiwa katika shughuli za nyumbani.

Hata hivyo ni muhimu kukumbuka kuwa kuna baadhi ya taka ambazo ni hatari na huenda zisigeuzwe ili kutumika kwa njia yenye faida. Taka hizi ni kama vile mikebe au vifaa vingine vyenye kubeba sumu au dawa hatari. Ni bora kuvitupa vifaa hivi katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo.

Kwa vyovyote vile, si jambo muhali kwa watu popote wanapoishi kulinda siha yao pamoja na kutunza mazingira. Ulinzi na utunzaji huo huhitaji uangalifu mkubwa katika utupaji taka.

a) Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 100. (alama 8, 1 utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

b) Kwa kurejelea aya ya tano hadi ya tisa, onyesha manufaa ya taka (maneno 80)
(alama 7, 1 utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Unda maneno yenye muundo wa sauti zifuatazo: **(alama 2)**

i) King'ong'o cha kaakaa laini, irabu ya nyuma wastani, irabu ya chini kati.

ii) Kikwamizo hafifu cha koromeo, irabu ya nyuma juu , kiyeyusho cha kaakaa gumu, irabu ya nyuma kati

b) Andika neno moja lenye silabi za muundo ufuatao. **(alama 1)**
irabu, konsonantii +konsonanti, irabu+konsonanti, irabu

c) Bainisha matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo: **(alama 2)**
Akiendelea kukichezea, kichuma chake ki motoni.

d) Unda vitenzi kutokana na nomino zifuatazo **(alama 2)**

i) hasidi-

ii) tafakuri-

e) Tunga sentensi yenye mpangilio wa maneno ufuatao: **(alama 2)**
nomino katika ngeli ya U-zi wingi.

Kivumishi cha pekee
Kitenzi halisi
Kielezi cha kiasi

f) Ainisha viambishi: **(alama 2)**
haujiki

g) Tumia mzizi –ny- kukamiliisha sentensi hii **(alama 1)**
Miti ya msitu huo ime ……. mvua katika jimbo hili

h) Tumia mzizi '-ema' katika sentensi kama: **(alama 3)**
i) kivumishi
ii) kielezi
iii) nomino

i) Mchezaji alipoona kiyu* aliya gugumia maji
Kando na matumizi haya ya kinyota, taja matumizi mengine mawili ya kiakifishi hiki. **(alama 2)**

j)Tunga sentensi ya swali ukitumia kiwakilishi nafsi ambata nafsi ya pili wingi **(alama2)**

k) Andika sentensi hii iwe katika usemi wa taarifa
"Nyinyi nyote mkipita nitawanunulia mikate miwili kesho jioni, mwalimu alituambia**. (alama 2)**

l) Andika kinyume cha sentensi hii:
Tajiri wengi walikashifiwa baada ya kuhamia msituni **(alama 2)**

m)Ainisha shamirisho na chajizo: **(alama 4)**
Mwanamke mzee alipikiwa chai tamu kwa sufuria kubwa leo asubuhi na mjukuu wake.

n) **Tunga** sentensi yenye muundo ufuatao: **(alama 2)**
$\boldsymbol{KN(\overline{S}) + KT\left(t + KN_2\,(N + V)\right)}$

o) Mohamed alifuzu mtihani huo vizuri kwa sababu alisoma kwa bidii (maliza kwa mtihani huo vizuri) **(alama 1)**

p) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielezo cha matawi.
Lilikuwa limelimwa na wakulima hodari sana. **(alama 4)**

q) **Andika** ukubwa wingi wa sentensi hii
Mtoto alimuua nyoka mdogo kwa kumpiga kichwani **(alama 1)**

r) Ainisha virai vinne katika sentensi hii:
Vipya kabisa vilivyoagizwa jana sokoni vitanunuliwa na mtoto wa Juma **(alama 2)**

s) Tunga sentensi moja kionyesha maana mbili za neno 'funza' **(alama 2)**

t) Mkungu ni kwa ndizi, koja ni kwa **…….** na**…….** ni kwa mboga . **(alama 1)**

4 <u>ISIMUJAMII (ALAMA 10)</u>

a) Terry: Liandikwalo ndilo liwalo. "Since when has man ever changed his destiny?"
i) Tambua mtindo wa lugha uliotumiwa na mzungumzaji wa maneno haya. **(alama 1)**
ii) Eleza sababu nne zinazopelekea wazungumzaji kutumia mtindo huu. **(alama 4)**

b) Wewe ni mfanyikazi katika kiwanda cha kutengeneza mavazi. Eleza sifa tano za lugha utayotumia unapowasiliana na wafanyakazi wenzako. **(alama 5)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA SITA)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*

d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima.***

e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Hadithi Fupi.*

f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	80	

SEHEMU YA A: RIWAYA (NGUU ZA JADI)

1. <u>Swali la lazima</u>

Alishangaa barua hiyo iliingia vipi mle ndani. Kwa nini ……. aweke barua yake ndani ya mkoba wake bila kuisoma? Au alisahau alipokwenda zake uhamishoni? Na ilitoka wapi hasa? …… aliamua kuifungua bahasha, liwe liwalo. Potelea mbali hata kama haikuwa yake …….. mwenyewe alikuwa kesha mtema kama masuo. Barua ile ina maana gani kwake sasa hata akiisoma? Alijaribu kuitatanua ili gundi iachilie ule upeto wa juu wa bahasha lakini wapi. Gundi ilikazana kumsumbua hadi akaamua kuirarua raru raru bahasha ili mradi aifikie ile barua. Alikuwa mwangalifu asiirarue hata hivyo barua aliyotamani sana kuisoma. Aliichomoa akaona ilikunjwa peto tatu. Aliikunjua huku mikono ikitetemeka. Vidole vilijaa jasho kwa shauku ya kutaka kujua yaliyoandikwa. Iliandikwa kwa wino mweusi uliokoza.

a) Tambua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Changanua mtindo katika kifungu hiki. **(alama 10)**

c) Fafanua sifa za wahusika wanaorejelewa. **(alama 6)**

<u>SEHEMU YA B: TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA</u>

Jibu swali la 2 au 3

2. Matatizo anuwai yanakabili jamii ya Bembea ya Maisha. Eleza kwa kutoa mifano mwafaka. **(alama 2)**

3. "Tena mtu asiyekujua wala hajapata kukutia jicho! Mpita njia na shughuli zake si ni malaika huyo? Kana kwamba umalaika una ngazi ……."

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Eleza 'umalaika' wa mrejelewa. **(alama 8)**

c) Tambua mbinu yoyote ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili. **(alama 4)**

d) Fafanua sifa za msemaji. **(alama 4)**

<u>SEHEMU YA C: HADITHI FUPI:</u>

<u>MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE</u>

Jibu swali la 4 au 5.

4. ' Pombe ina madhara chungu nzima' Thibitisha ukweli wa kauli hii ukirejelea hadithi ya kila mchezea wembe. **(alama 20)**

5. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo.

"Akili za masomo huna ……..zinachangamkia barua na mambo ya wanaume tu. Mamako alikuwa vivyo hivyo na unajua kilichomfika. Kweli mtoto wa nyoka ni nyoka!" Yunuke alimfokea. Alikizima kibatari kile na giza kuu likaivaa nyumba. Mwezi mmoja baada ya mtihani kukamilika, Ombati alifika kijijini kwa ajili ya likizo ya mwezi wa Disemba. Alifika nyumbani kufanya maandalizi ya kupeleka Mike katika shule ya upili kwani alikuwa na imani kuwa angepita mtihani. Ombati alikuwa na jingine. Sabina aliwasikia binamu zake waliokuwa katika shule ya upili wakizungumza kuhusu mpango wa baba yao wa kumwoza kwa kijana mmoja mwendesha pikipiki ili apate mahari ambayo dadake Nyaboke hakumpa.

a) Tambua mbinu zozote za lugha ambazo zinajitokeza katika kifungu hiki. **(alama 4)**

b) Fafanua maudhui yoyote matano yanayojitokeza katika dondoo hili. **(alama 10)**

c) Hakika mwishowe machweo yalifika. Huku ukirejelea hadithi ya Mapambazuko ya Machweo, tetea kauli hii.

SEHEMU YA D: FASIHI SIMULIZI

Jibu swali la 6 au 7.

6. a) Fafanua maana ya miviga. **(alama 2)**

b) Eleza sifa saba za miviga. **(alama 7)**

c) Tambua hawara nne za Miviga. **(alama 8)**

d) Taja mifano yoyote mitatu ya miviga. **(alama 3)**

7. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.

Hadithi ya Jabali inasimuliwa na jamii nyingi. Jabari alizaliwa kashika mkuki mkononi. Mawio ambayo kilio chake, ambacho kwa kweli kulikuwa mgurumo, kilipasua anga, nyota kubwa ilianguka kutoka mbinguni. Ulimwengu mzima ulitetemeka na kutwaa giza.

Hata kabla mama mtu hajampa ziwa, Jabali alikuwa amevuvumka na kuwa ghulamu wa miraba mine. Haikuchukua muda, hata vita kati ya jamii ya Sule na Suna vikaanza; kikosi cha Sule cha wapiganaji mia moja kikawajia vijana wa Suna kwa sime na nyuta. Jabari aliwakabili kwa konde pekee akakirambisha dongo kita kizima.

a) Bainisha kipera cha utungo huu. **(alama 1)**

b) Toa sababu nne kutoka kwa kifungu kuthibitisha jibu lako la (a). **(alama 4)**

c) Eleza munufaa matano ambayo jamii itapata kutokana na kipera hiki. **(alama 5)**

c) Eleza changamoto nne ambazo mkusanyaji wa data kuhusu kipera hiki angekumbana nazo. **(alama 10)**

SEHEMU YA E: USHAIRI

8. Soma shairi kisha ujibu maswali yanayofuata.

Niokoa muokozi, uniondolee mashaka
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
Nimekitiri simanzi, ni katika kuudhika
Mja wako nasumbuka, nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka, nataka kwao afua
Nirehemu kwa haraka, nami nipate pumua
Naomba hisikitika, na mikono hiinua
Mtenda ndiwe moliwa, nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe moliwa, we ndiwe Mola wa anga
Mazito kuyaondoa, pamoja kuyatenga
Ukauepusha ukiwa, ya pingu zilonifunga
Nikundulia muwanga, nipate nitakayo

Nikundulia muwanga, nipate toka kizani
Na huzuni n'ondolea, itoke kwangu moyoni
Mambo mema niegheshea, maovu nisitamani
Nitendea wa manani, nipate niyatakayo

Igeuze yangu nia, dhaifu unipe mema
Nili katika dunia, kwa afia na uzima
Moliwa nitimizia, yatimize yawe mema
Nifurahike mtima, nipate niyatakayo

a) Taja aina ya shairi. **(alama 2)**
b) Fafanua dhamira ya mshairi. **(alama 2)**
c) Tambua na ueleze bahari zozote tatu za shairi. **(alama 3)**
d) Eleza muundo wa shairi hili. **(alama 4)**
e) Msahiri ametumia uhuru wake wa utunzi. Eleza kwa mifano mine. **(alama 4)**
f) Eleza toni ya shairi. **(alama1)**
g) Andika ubeti wa pili katika lugha ya nathali. **(alama 4)**

KCSE 25

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA SABA)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)

MAAGIZO KWA MTAHINIWA:

a) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima**.*

b) *Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*

c) *Kila insha isipungue maneno **400.***

d) *Kila insha ina alama 20.*

e) *Kila insha **lazima** iandikwe kwa lugha ya **Kiswahili.***

f) *Insha zote **sharti** ziandikwe katika nafasi ulizoachiwa kwenye kijitabu hiki cha maswali.*

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	20	
2	20	
3	20	
4	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Wewe ni mhariri mkuu wa Gazeti la Mwangaza, andika tahariri kuhusu namna tatizo la ukosefu wa nafasi za ajira miongoni mwa vijana linavyoweza kukabiliwa.

2. Serikali za ugatuzi zina faida nyingi kuliko hasara . Jadili

3. Andika insha inayooana na methali **kutangulia si kufika**

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno haya:

Milipuko mikubwa ilisikika pu! Pu! Puu! Kisha niliwaona watu wakikimbia kuelekea pande zote**…**

KCSE 25

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA SABA)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)

Maagizo

(a)Andika jina na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.

(b)Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani

(c) Jibu maswali yote.

Kwa matumizi ya mtahini pekee

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
4	40	
4	10	

1. UFAHAMU (alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano yenyewe. Yapo mahusiano bainaya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huuhautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetuwa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu,unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili,mahusiano ya kipindi cha wastani,kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi,washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekanakudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya,hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii waoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri,uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe,kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano katiya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani. Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasahuweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujirikatika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada,kwenye kituo cha mafuta,kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekanowa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na‘uhusiano wa chembe chembe.’ Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea,nguo anazokufulia,ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzakekwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula,amefutwa kazi,amefiliwa,ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusianavipi na jamaa zetu, marafiki zetuna majirani zetu? Je, uhusianowetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. **(alama 1)**

(b) Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. **(alama 1)**

(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. **(alama 2)**

(d) Eleza sababu nne kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo**.** **(alama 2)**

(e) Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. **(alama2)**

(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? **(alama2)**

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. **(alama 3)**

(i) inasigana**.....**

(ii)yameghoshi**……**

(iii)vighairi**……**

2 UFUPISHO (alama 15)

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema ‘maarifa ni nguvu.’

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: ‘Elimu ni mali.’ Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile.

Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', ' mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a) Fupisha aya ya pilina tatu (maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.

(maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)

Matayarisho

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA (alama 40)

(a) Taja sauti mbili zinazotamkwa mdomoni. **(alama 2)**

(b) Andika visawe vya maneno yafuatayo; **(alama 2)**

i)doa……

ii)omba……

(c) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi **(alama 2)**

Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo .

(d) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo;

Hawa ni watoto wa marehemu Bwana Ndovu na Bi.Makombo **(alama 2)**

(e) Eleza matumizi ya alama ya ritifaa kwa neno lifuatalo;

N'shamchukua **(alama 2)**

(f) Eleza mofimu katika neno lifuatalo **(alama 3)**

Walichokilalia

(g) Bainisha vitenzi vilivyo katika sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

Kalamu aliyokuwa nayo mwalimu ni ya mwanafunzi.

(h) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale **(alama 4)**

Chakula kitamu kimeandaliwa.

(i) Huku ukitoa mifano mwafaka onyesha matumizi matatu ya kinyota katika sentensi. **(alama 3)**

(j)Tunga sentensi moja ukitumia kielezi cha wakati na kielezi cha mahali**.** **(alama2)**

(k) Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. **(alama 1)**

IK+KI+KI+KI

(l) Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo. **(alama 2)**

(i) kibainishi

(ii)parandesi

(m) Tumia neno –baya kama**:** **(alama 2)**

(i) kiwakilishi

(ii)kielezi

(n) Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi 'la' katika kauli ya tendewa. **(alama 2)**

(o) Unganisha sentensi zifuatazo ukitumia neno japo;

i)Selina alijitahidi sana.

ii)Selina hakushinda mbio hizo.

(p) Kwa kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo: (**alama2)**

Tinga amewafanya ng'ombe wake wanywe maji.

(Anza kwa : Mifugo wangu ……..usitumie 'amewafanya')

(q)Tunga sentensi moja yenye nomino dhahania na kivumishi kimilikishi. **(alama 2)**

(r) Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii. **(alama 2)**

Umu alimwandikisha mkewe.

(s)Onyesha dhamira ya sentensi hii; **(alama 1)**

Huenda mvua ikanyesha leo

4.ISIMU JAMII **(Alama 10)**

Kumekuwa na mijadala mingi kuhusu athari ya chanjo dhidi ya ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Kovid-19.Wewe ni Afisa wa afya katika eneo lenu umealikwa kutoa hotuba kuhusu usalama wa chanjo hii .Eleza sifa kumi za lugha utakayotumia.

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA SABA)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Masomo ya Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali* ***manne*** *pekee.*

d) *Swali la* ***kwanza*** *ni la* ***lazima.***

e) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Hadithi Fupi.*

f) *Usijibu maswali* ***mawili*** *kutoka* ***sehemu moja****.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	80	

1. LAZIMA: NGUU ZA JADI- Prof Clara Momanyi ALAMA 20

Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuta ;

Watategemewa na nani maishani? Hiki ndicho kizazi cha kesho au kizazi kilichopotea tayari?

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

b)Tambua toni katika mazungumzo haya. **(alama 2)**

c)Onyesha ni vipi kizazi cha leo na cha kesho kilivyopotea. **(alama 12)**

2. TAMTHILIA: BEMBEA YA MAISHA – Timothy Arege ALAMA 20

Jibu swali la i au ii

i) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:

...lakini ndio tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama... kama... kama... kama vile tambara bovu.

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b) Eleza umuhimu wa msemewa katika kukuza maudhui. **(alama 4)**

c)Tambua mbinu nne za kimtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

d)Kwa kutoa hoja nne kutoka kwa Tamthilia eleza ni vipi utamaduni ulivyothaminiwa katika jamii hii ya Bembea ya Maisha. **(alama 4)**

e) Onyesha jinsi faraja ilivyoalika katika maisha ya msemewa kwa kurejelea tamthilia ya: Bembea ya Maisha. **(alama 4)**

AU

(a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. **(alama 10)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (*Kimya*). Siku hazigandiwala jana hairudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (*Kimya*). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (*Kimya*). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! *(kama anayeisemea pombe).* Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. *(anapunga mkono.)* Kwaheri pombe. Buriani.

b) Bainisha toni ya dondoo hili. **(alama 2)**

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima.**(alama 8)**

3. USHAIRI ALAMA 20

i) Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

Nilikuomba chakula, nawe kweli kaninyima
Sikuwa hata na hela, kakimbila kwenye **dhima**
Megunduwa ewe Shilla, hunijalingi daima.

Sisahau kisogoni, mnobe ulipokuwa
Makabadhi linombeni, nani kwa wema litowa
Na libasi za mwilini, samani za mtakawa.

Shilla ya shule **sifutu**, lokufanyia hisani
Dafutari na madutu, sare pia likupeni
Linisumbua kuntu, na mie kavumileni

Kozi na nilikupeni, kulipa karo chuoni
Ulinisapa kamani, mnobe nikabakini
Asante punda yani, ni mateke wajamani

Bada ya kazi mwanangu, siku 'tupa abadani.
Nilisaka msenangu, lodi rafiki moyoni
Ka'pa kazi wanguwangu, hela nyingi kushikeni

Babayo alifariki, ukiwa bado kiini
Kiacha bila rafiki, hapo hapo pa nyumbani
Nami amiyo kacheki, na nikakuchukueni

Waringa kama tausi, wewe Shilla ni kinyonga
Daraja usilitusi, lokuvusha engaenga
Unapofika ofisini, kumbuka kutojitenga

Maswali

(a) Lipe shairi hili anwani inayofaa. **(alama 1)**

(b) Bainisha hisani **tatu** alizofanyiwa nafsi nenewa. **(alama 3)**

(c) Tambua nafsi neni katika shairi hili. **(alama 1)**

(d) Andika ubeti wa **pili** katika lugha nathari. **(alama 3)**

(e) Taja na ueleze mbinu **tatu** alizotumia malenga ili kutosheleza mahitaji yake ya kiarudhi. **(alama 3)**

(f) Eleza toni za shairi hili. **(alama 1)**

(g) Fafanua sura ya shairi hili. **(alama 3)**

(h) Ainisha shairi hili ukizingatia vigezo vifuatavyo: **(alama 3)**

(i) Mishororo
(ii) Migao/ vipande
(iii) Vina

(i) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. **(alama 2)**

(a) Dhima

(b) sifutu

AU

ii) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Moyo haukongi:
Haidhuru uwe wa mwanadamu
Au wanyamamwitu.

Japo maji yamyumbishe
Kando ni mwabahari
Kizee utamwona
Kwa nguvu za uchawi wa moyo
Mawimbini akisukwasukwa
Mithili ya jahazi lililochoka
Kwa urefu wa safari:
Ingawa atabamizwa matumbwaweni
Na yake seruni maji kuitwaa
Atang'ang'ana kuidaka japo kwa shida
Na majini kuelea
Kama anayeyatisha kuwa
Bado si haya misuli ipo.

Basi ajabu usione
Paka maziwa kunywa
Katika uzima wake
Au bi kizee kichwa akiyumbisha
Kwa mliowaala
Ama nyama kupania kula
Japo jino la mwisho
Liling'oka juzi.

Moyo haukongi kwa msukumo wa wakati:
Ni misuli inokonga.
Moyo, simba wa wakati.

a) Hili ni shairi la aina gani? **(Alama 2)**

b) Eleza muundo wa shairi hili. **(Alama 4)**

c) Kwa nini mshairi anaeleza kuwa moyo haukongi? (**Alama 4)**

d) Tambua mishororo baki kwenye shairi hili. **(Alama 2)**

e) Eleza mbinu mbili za idhini ya mshairi kwa kurejelea shairi hili. **(Alama 2)**

f) Eleza toni ya shairi hili. **(Alama 2)**

g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. **(Alama 4)**

4. HADITHI FUPI: Mapambazuko ya Machweo Na Hadithi Nyingine na D.W. Lutoma na Phibbian MuthamALAMA 20

Jibu swali moja

i) Mzimu wa Kipwerere!-Yussuf Shoka Hamad

Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuata.

"…Akainama chini kwenye tendeguu moja la kitanda cha besera.Akachukua kibatari cha kiberiti ili awashe taa.Mimi,nikiwa mle mvunguni.sasa kwa hakika nilishamjua shetani wa mzimu ule ni nani.Kumbe hakuwa shetani wala Kipwerere!"

a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(alama 4)**

b)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. **(alama 4)**

c)Onyesha umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(alama 4)**

d)Wanakijiji waliuogopa mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuuabudu na kutoufanyia mzaha. Thibitisha kauli hii **(alama 8)**

AU

ii) ***Msiba wa Kujitakia*** **- D.W .Lutomia**

"Wetu ni wetu ,hata akiwa mbaya …ni wetu.hatuna budi kuchagua yeye .lisilobudi hubidi."

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4)**

(b)Fafanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hii. (**alama 4**)

(c)Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai.jadili.(**alama 12**)

5. FASIHI SIMULIZI ALAMA 20

Chagua swali moja kati ya haya

1.**Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Heri ujue mapema
Nasaba yetu haina woga
Woga haumei kwetu, humea kwa kina mamako.
Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah! Kisu cha ngariba ni kikali ajabu.
Iwapo utatikisa kichwacho.
Uhamie kwa wasiotahiri,
Ama tukwite njeku.

Mpwangu kumbuka hili,
Wanaume wa mlango wetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali
Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia
Sema unachotaka
Usije kunitia aibu

Maswali;

(a) Taja na uthibitishe shughuli zozote za kiuchumi za jamii ya wimbo huu **(alama 4)**
(b) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? **(alama 2)**
(c) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha **(alama 2)**
(d) Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume. Thibitisha kauli hii. **(alama 2)**
(e) Eleza kwa hoja sita wajibu wa nyimbo katika jamii **(alama 6)**
(f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii kwa hoja nne. **(alama 4)**

AU

2. Soma yafuatayo kisha ujibu maswali

…Niaje wazungu wanaweza kutunza vitu vikajaa kwenye friji? Kwani tamaa yao huwa wapi? Yaani nimeweka soda mbili tu kwenye friji lakini akili haitulii hadi nizinywe.Siwezi kulala chumba kimoja na chakula.. Niko sebuleni nazunguka tu kama koo atafutaye pa kutagia yai. Najaribu kuwaza vitu vingine lakini wapi! Akili inaniambia tu, "My friend, kunywa soda!"

a) Bainisha kipera cha utungo huu **(alama2)**
b) Utanzu wa kipera hiki huweza kuchukua nafasi muhimu katika fasihi simulizi. Thibitisha kwa kurejelea hoja zozote sita **(alama6)**
c) Ufanisi wa uwasilishaji wa utanzu huu unategemea fanani. Tetea kauli hii. **(alama6)**
d) Ni changamoto zipi zinaweza kumkabili mwanafasihi mtafiti nyanjani? **(alama6)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA NANE)

KISWAHILI

102/1

KARATASI YA 1 (INSHA)

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

(a) Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.

(b) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobaki.

(c) Kila insha isipungue maneno 400.

(d) Kila insha ina alama 20.

(e) Kila insha lazima iandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
	40	

1. Lazima

Wewe ni Mwenyekiti wa Tume ya kupigana na ufisadi nchini. Umealikwa kuhutubia magavana kuhusu athari za ufisadi huku ukipendekeza hatua za kukabiliana na jinamizi hili. Andika hotuba utakayoiwasilisha.

2. Mitandao ya kijamii ina madhara mengi kuliko faida. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Achezeaye tope humrukia.

4. Andika insha itakayoanza kwa maneno yafuatayo:

Mara nilisikia ukemi mkali kutoka nje. Majibwa yalibweka kwa mfululizo kana kwamba yanasemezana**…**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA NANE)

KISWAHILI

102/2

KARATASI YA 2 (LUGHA)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO

a) *Jibu maswali* ***yote*** .

b) *Majibu yote yaandikwe katika* ***nafasi*** *ulizoachiwa katika kitabu hiki cha maswali.*

c) *Majibu yote ni* ***lazima*** *yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1. UFAHAMU ` **(alama 15)**

Unafiki katika dini pia unadhihirika kupitia injili ya ufanisi ambayo siku hizi inaenezwa kama moto kichakani ikilinganishwa na walivyosisitiza mitume kuwa, watu watubu na kuishi maisha ya utakatifu. Si ajabu kumsikia mchungaji akiitisha shilingi elfu moja ili kupata thibitisho la iwapo jina lako linapatikana katika kitabu cha uzima wa milele. Huu ni unafiki kwa sababu maandiko matakatifu hayakubaliani na hilo. Waumini hujikuta wakinunua miujiza. Viongozi wanafiki huwaambia watoe kiasi fulani cha pesa ili kupona kutokana na magonjwa sugu kama vile ukimwi,saratani, kupinda kwa midomo na kadhalika.

Nyadhifa katika dini pia huwavutia watu wengi.Utawapata baadhi ya viongozi wa dini wakitumia kila njia kubaki uongozini. Wao huwezah ata kuwanunua wafuasi ili wawapigie kura ama kuwaunga mkono

katika kinyang'anyiro cha cheo fulani. Uongozi hutoka kwa Mungu. Hata hivyo, baadhi ya viongozi wanaohubiri neno hilo la Mungu, utawapata wakiwa na mikutano ya siri ili kuwashawishi waumini kuhakikisha kuwa wamebaki uongozini.

Haina haja ya kusaza waumini. Baadhi yao pia ni wanafiki. Utawapata wakishiriki kikamilifu katika masuala ya dini, ilhali nia yao ni tofauti. Vijana waliopatikana katika msikiti huko Mombasa wakipewa 'mafunzo

va kidini ilhali bunduki na risasi pia zinapatikana mumo humo msikitini, ni mfano wa **ulaghai** na unafiki katika dini, (iwapo taarifa hizo ni za kweli). Wahubiri waliokuwa wakiendesha mafunzo hayo, ni wanafiki

kwa sababu nia yao katika nyumba ya Mungu ilikuwa mbaya ndiposa makabiliano kati yao na polisi ilichukua muda wa saa saba hivi.

Unafiki pia hujitokeza wakati ambapo baadhi ya viongozi wa dini hutumia dini kama daraja ya kuingia katika ulingo wa siasa. Wao hutumia madhabahu kufanyia kampeni ili kujitosheleza kisiasa. Kupinga maovu ya kisiasa kupitia dini ni sawa. Hata hivyo, kutumia dini kujipatia umaarufu ni kosa la kinafiki.

Ni ombi langu kuwa dini itatumiwa kulisha kondoo wala si **kuwapunja.** Maandiko matakatifu yanapigia debe utakatifu katika dini wala si ulaghai na unafiki. Lazima kila muumini atoe zaka na sadaka kama ilivyo katika

neno la Mungu. Hata hivyo nafasi hii isitumiwe na viongozi wenye ulafi kuwanyonya waumini wao. Mahali patakatifu ni lazima paheshimiwe wala pasitumiwe kama nyumba ya kupanga mashambulizi na maovu kwa wanadamu wasiokuwa na hatia.

a) Kipe kifungu hiki anwani mwafaka. **(alama 1)**

b) Onyesha msambao wa unafiki katika dini. **(alama 4)**

c) Kwa nini waumini wanaonekana kuchanganyikiwa? **(alama 2)**

d) Kwa nini injili ya ufanisi imeshamiri kuliko ile ya toba? **(alama 2)**

e) Viongozi wengi wa kidini hawataki kung'atuka uongozini. Toa sababu moja. **(alama 2)**

f) Waumini wanalaumiwa kwa nini? **(alama 2)**

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyo tumika katika kifungu. **(alama 2)**

i) ulaghai

ii) kuwapunja

2. MUHTASARI

Kila niwazapo kisa hiki, machozi hunitoka si haba. Hali ya huzuni ikanikumbatia kusadifu kusononeka. Nikawa sina sinani majibu kwa maswali kochokocho. Ama kweli “majuto ni mjukuu huja kinyume”.

Katika kijiji chetu cha Kazamwendo, tuliishi pamoja kwa umoja na udugu ukazagaa kotekote. Wanakijiji walisaidiana kwa lolote lile, shida ya mmoja ikawa shida ya wote. Ungewakuta wavyele waliobugia chumvi nyingi wakiwapa nasaha vijana kwa hekima isiyo na kifani. Tabia ya ufuska ikakemewa na maadili ya utu wema yakafunzwa kwa wote. Utovu wa nidhamu ukakashifiwa pasi na maficho wala tasfida.

Kukaja siku moja akatokea barobaro kutoka mjini. Asili yake ikawa kizungumkuti na hata jina lake halisi halikufahamika. Kila mmoja alimwita jina la utani “Mpanzi”. Ni wazi alikuwa na fedha na alivalia nadhifu. Fauka ya hayo, alipenda anasa sana. Vijana wengi kijijini walimfuata ili angalau wajinasibishe kwake. Miongoni mwa waathiriwa waliovutiwa na Mpanzi alikuwa Maria, mkoi wangu tuliyeishi pamoja tangu utotoni, tukicheza pamoja na hata kusoma shule moja.

Ushirika wa Maria na Mpanzi ulielekeza mabadiliko makubwa katika tabia yake. Dharau ikachukua nafasi ya heshima, kiburi kikachukua nafasi ya unyenyekevu na aibu akaipa kisogo. Akakataa katakata kutangamana na wanakijiji wenzake akiwaita “washamba”. Kila mtu alistaajabishwa na yale mabadiliko ya kighafla yaliyompata Maria kwa kuwa hapo awali, licha ya kurembeka mithili ya tausi alikuwa na nidhamu ya hali ya juu akiwaheshimu wote na kijiheshimu pia.

Maji yalizidi unga binti ya watu alipoanza kukwepa nyumbani akienda densini au ukipenda kwenye disko. Huko akatangamanana watu asiowajua walomwingiza katika uraibu wa ulevi na mapenzi haramu. Akabadilisha wanaume kama nguo ili apate fedha za kustarehe kutimiza raha na buraha. Mavazi yakawa minisketi au tumboketi. Akatembea nusu-uchi na wakati mwingine mavazi yakimbana huku akizua ashiki za kifisi mioyoni mwa wanaume. Akafaulu azimo lake na akafuatwa na wengi.

Waviele walipoona hivyo, wakajaribu kwa juhudi na adili kumnasihi lakini akawa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Wakamwachia ulimwengu. Muda hakuisha mwingi Maria akaanza kuugua. Ikaanza kana kwamba ni kikohozi cha kawaida, kisha upele mwilini, afya ikadhoofika kiasi cha nyama kuganda kwenye mifupa.ungemtazama ungefikiri ni kiwiliwili cha mtu. Uchunguzi wa daktari ulibainisha wazi kuwa alikuwa ameambukizwa ugonjwa wa ukimwi. Mtoto wa tatu akalia kwa uchungu na majuto mengi. Akaomba kuwaona wanakijiji wote. Walipoitikia mwito wake aliwaomba msamaha kwa majozi huku akidondoa orodha ndfu ya majina ya watu aliofanya nao mahaba. Kwa sauti hafifu alisema “Taf-taf-adh-ali m-m-mnisamehe, nilidanganywa na mpanzi, nikasusia ushauri wa wazazi wangu. Nikaasi mema niliyopewa. Nawaomba muichukulie hali yangu kama funzo. Msife moyo kwa yote, siku hizi madktari husema ugonjwa huu hauna tiba lakini una kinga. Heri muende mpimwe mjue hali zenye za afya. Msiugue kama mimi ilhali kuna dawa zinazoweza kupunguza makali ya viini vya ugonjwa huu.” Mara pu! Akaanguka chini na kukata roho.

Hali ya simamzi na majonzi ikakithiri maana ilikuwa dhahiri shairi watu wengi wengi walikuwa wameathirika. Fikira za kufa kwa wazazi na kuwaacha mayatima wachanga katika kijiji ziliwazuga. Siku ya mazishi ukumbi ulijaa hadi pomoni. Jamaa na marafaiki walliwasihi kumpa buriani. Muhubiri aliposimama kuhutubia waombolezaji alitamka “Maandiko yanasema kuna njia panda-

njema kwa macho ya mwanadamu yenye hatima ya mauti na njema kwa mtazamo wa Mungu yenye mwisho mzuri. Kila mtu aepukane na uozo na msishiriki ngono kiholela. Waliooa wawe waaminifu ;waache "mipango ya kando." Sote tuishi kwa kumcha Mungu ili tupone. Wote walisikiza wasia huo kwa umakini na utulivu. Maria alipozikwa, watu walirejea kwao huku wakiungama kuwa "Majuto ni mjukuu huja baadaye".

a) Fupisha ujumbe wa aya ya **pili, tatu** na **nne** kwa maneno 50. **(Alama 7,** mtiririko 1)

Matayarisho

Jibu

(b)Eleza kwa maneno 60 masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya **mbili** za mwisho.

(Alama 8, mtiririko 1)

Matayarisho

Jibu

3) MATUMIZI YA LUGHA **(alama40)**

(a) Linganisha na ulinganue sauti **ny** na **ng'.** **(alama 2)**

(b) Onyesha **shadda** katika maneno yafuatayo. **(alama1)**

(i)chekesha**……**

(ii)embe**……**

(c) Kamilisha majina ya **makundi** yafuatayo. **(alama 2)**

(i)……. cha nyanya

(ii)…….. cha funguo

(d) Andika sentensi upya ukitumia aina za **viwakilishi** vilivyo katika mabano. **(alama 2)**

(i) Baadaye…… walitoa ushahidi .(nafsi)

(ii)Bilauri hii ina maji .**Bilauri** iliyowekwa pale ina maziwa.(Kiwakilishi cha pekee badala ya neno lililokolezwa wino)

(e) Andika katika **usemi** halisi. **(alama3)**

Daktari alitaka kujua matatizo aliyokuwa nayo.

(f) Eleza matumizi ya **na** katika sentensi ifuatayo: **(alama2)**

Walimu na wanafunzi wana nafasi nzuri ya kuwashauri wanafunzi wanaopotoshwa na wenzao.

(g) Andika **wingi** wa sentensi : **(alama 2)**

Wembe ule ni mkali sana.

(h) Bainisha aina za **shamirisho** na **chagizo** katika sentensi ifuatayo: **(alama 3)**

Seremala alimtengenezea mwalimu mkuu madawati ishirini juzi.

(i) Tunga sentensi ukitumia neno **mpaka** kama : **(alama 4)**

(i)nomino……

(ii)kitenzi……

(iii)kielezi……

(iv)kihusishi……

(j)Ainisha viambishi katika neno: **(alama 2)**

Tutaonana

(k)Akifisha sentensi ifuatayo. **(alama 3)**

mody alitusomea aya mbili kutoka kitabu maisha ya kisiwa cha hazina.

(l)Ainisha **virai** vilivyopigiwa mstari. **(alama 2)**

Mawingu <u>mazito ajabu</u> yalijitandaza <u>kwenye anga</u> .

(m)Tunga sentensi yenye **muundo** ufuatao : **(alama 3)**

KN(N+RV) + KT(T+RE)

(n) Tumia vishazi vifuatavyo kuunda sentensi kulingana na maagizo. **(alama 2)**

Wanasayansi walifanya majaribio .

Wanasayansi walipata tiba ya ugonjwa huo.(Tumia **ka** ya kuonyesha tukio moja ni matokeo ya tukio lingine)

(O)Nyambua vitenzi vifuatavyo katika hali uliyopewa kisha uvitungie sentensi: **(alama 2)**

(i)la (kutendeshana)

(ii) panga (kutendeshewa)

(p)Kamilisha sentensi ifuatayo kwa kutumia **kinyume** cha kitenzi kilichopigiwa mstari. **(alama 1)**

(ii)Mafundi <u>wataezeka</u>……. paa la mabati.

(q) Eleza matumizi ya **ki** katika sentensi ifuatayo: **(alama 4)**

Kijakazi na kitoto wamekuwa wakila wakiimba kikasuku.

<u>4. ISIMU JAMII (Alama 10)</u>

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Msemaji 1:Wale wanaounga mkono mswada huu wa Finance waseme ndiyo!

Sauti:Ndiyooooooo!

Msemaji 1:Wale wanaopinga mswada waseme laa!

Sauti: Laaaa!

Msemaji 1: Waliounga mkono mjadala wameshinda.

Msemaji 2:Hoja ya nidhamu please!

Msemaji 1: Mheshimiwa,sheria nambari 200 , kifungu cha 6, yazuia mjadala zaidi.

Naomba kuvunja baraza.

a)Bainisha sajili ya mazungumzo haya. ` **(alama 2)**

b)Eleza sifa zozote nne zinazojitokeza katika sajili uliyobainisha katika (a). **(alama 4)**

c) Eleza jinsi mazingira hudhibiti mazungumzo: **(alama 4)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA NANE)

KISWAHILI

102/3

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Andika jina lako na nambari yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

b) *Tia sahihi kisha uandike tarehe*

c) *Jibu maswali **manne** pekee*

d) *Swali la kwanza ni la lazima*

e) *Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Tamthilia, Riwaya, Ushairi na Hadithi Fupi*

f) *Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja*

g) *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU YA A: USHAIRI **(ALAMA 20)**

LAZIMA

Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,
Ufyeke, upime na uweke nguzo,
Kisha paa uweke na ukandike,
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,
Nje na ndani ya nyumba watazunguka,
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,
Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,
Ukae nje nzima siku usubiri,
Wazima wamelala ukirudi usiku,
Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,
Na kisha wengine usiku mchana uwasake.
Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

Maswali

(i) Hili ni shairi la aina gani? **(alama 1)**

(ii) Eleza **muundo** wa shairi hili **(alama 3)**

iii) Eleza jinsi mshairi alivyoutumia **uhuru** wake katika utunzi wa shairi hili. **(alama 4)**

iv)Taja mbinu **mbili za lugha** alizotumia mshairi na uzitolee mifano. **(alama 4)**

v)Andika **ubeti wa tatu** kwa lugha nathari. **(alama 4)**

vi)Eleza **ujumbe** wa mshairi. **(alama 2)**

vii)Toa mfano mmoja wa mshororo **mshata**. **(alama 1)**

viii)Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? **(alama 1)**

SEHEMU YA B:TAMTHILIA

BEMBEA YA MAISHA (TIMOTHY M. AREGE)

Jibu swali la 2 au 3

2.‘’ Lakini ndiyo tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama...kama…kama vile tambara bovu.’’

a. i)Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. **(Alama 4)**

ii)Tambua mbinu **mbili** za kimtindo katika dondoo. **(Alama 2)**

b) Fafanua **umuhimu wa msemaji** katika kujenga ploti. **(Alama 4)**

c) **Utamanduni** huthaminiwa sana na jamii ya tamthilia ya Bembea ya Maisha. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutoa mifano **kumi** mwafaka tamthiliani. **(alama 10)**

3.Beni:Afadhali hao.Mjukuu wangu hatofautishi kondoo,mbuzi na mbwa.Wote hao kwake yeye ni mbwa!(*wanacheka wote)*

Yona: Inachekesha.

Swali

Mazungumzo haya kati ya Beni na Yona yanabainisha tofauti iliopo kati ya suala la *usasa na ukale*. Kwa kutoa mifano **kumi** inayoonyesha usasa na **kumi** inayoonyesha ukale,linganua masuala haya. **(alama 20)**

SEHEMU YA C: RIWAYA

NGUU ZA JADI:*CLARA MOMANYI*

Jibu swali la 4 au 5

4.“Naweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake.”

(a)Weka dondoo hili katika **muktadha** wake. **(alama 4)**

(b)Tambua **maudhui** katika dondoo hili. **(alama 4)**

(c)Kwa kutoa mifano **kumi na miwili** mwafaka kutoka riwayani,onyesha jinsi maudhui uliyotambua hapo juu(4b) yalivyoshughulikiwa na mwandishi**.** **(alama 12)**

5. Tamaa na ubinafsi ni baadhi ya masuala makuu yaliyoshughulikiwa kwa mapana na marefu na *Clara Momanyi* katika riwaya yake ya *Nguu za Jadi*. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani thibitisha ukweli wa kauli hii. **(alama 20)**

SEHEMU YA D :HADITHI FUPI

MAPAMBAZUKO YA MACHWEONA HADITHI NYINGINE

Jibu swali la 6 au 7

WINNIE NYARURI OGENCHE:SABINA

6.Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.

a)Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. **(alama 6)**

b)Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. **(alama 4)**

c)Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. **(alama 10)**

YUSSUF SHOKA HAMAD: ***Mzimu wa Kipwerere***

7.“…Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama.”

(a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(Alama 4)**

(b)Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(Alama 4)**

(c)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. **(Alama 2)**

(d)Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. **(alama 10)**

SEHEMU YA E: FASI HI SIMULIZI

Swali la nane

8. a) Ulumbi ni nini**?** **(alama 2)**

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii**?. (alama 6)**

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi**. (alama 6)**

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. **(alama 6)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TISA)

KISWAHILI

102/1

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
c) *Andika insha **mbili**. Insha ya kwanza ni ya **lazima** kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobakia.*
d) *Kila insha isipungue maneno 400.*
e) *Kila insha ina alama 20.*

Matumizi ya Mtahini Pekee

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
Jumla	40	

MASWALI

1. Suala la umoja wa kitaifa wakati huu wa kampeni za uchaguzi limekuwa katika vinywa vya wananchi wengi. Andika tahariri katika gazeti la MWANANCHI, kuhusu namna ya kustawisha umoja wa kitaifa.

2. Magonjwa mengi yanasababishwa na mitindo ya kisasa ya maisha. Jadili.

3. Andika insha inayoafiki methali; Asiyejua faida ya mwangaza aingie gizani.

4. Andika insha itakayomalizika kwa; **...** nilipojitazama, nilijidharau kwa aibu niliyopata. Niliapa kutorudia kitendo hicho maishani mwangu.

KCSE 25

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TISA)

KISWAHILI

102/2

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

i.*Andika jina lako na Nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

ii.*Weka sahihi yako kisha tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa*

iii.*Jibu maswali yote.*

iv.*Majibu yaandikwe katika nafasi zilizoachwa wazi katika kijitabu hiki cha maswali*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	**80**	

1. UFAHAMU: (Alama 15)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

KUKITHIRI kwa visa vya utoaji wa hongo kwa wapiga kura walioshiriki chaguzi ndogo zilizofanyika Jumatatu katika eneobunge la Malindi na Kaunti ya Kericho ni ithibati tosha kuwa ufisadi ume-kita mizizi nchini.Kadhalika,visa hivyo vilidhihirisha kuwa demokrasia imedidimia na taasisi za kupambana na visa vya ufisadi zimefifia.mwezi uliopita, Wakenya kupitia mitandao ya kijamii walishtumu Rais wa Uganda Yoweri Museveni kutokana na kile walichotaja kuwa matumizi ya mabavu' kuhifadhi kiti chake baada ya kuwatishia wapinzani wake.

Watumiaji wa mitandao ya kijamii pia walimkosoa Rais Uhuru Kenyatta kumpongeza wenzake wa Uganda huku wakisema aliunga mkono ukandamizaji wa demokrasia,Lakini, visa vya uhongaji wa wapiga kura vilivyoshuhudiwa katika maeneo ya Malindi na Kericho vikitekelezwa na viongozi wa kisiasa hata Wengine wakiwa wa muungano tawala wa Jubilee, ni dhihirisho tosha kuwa Wakenya hawakuwa na sababu ya kushutumu Rais Museveni.

Utumiaji wa mabavu au kununua wapiga kura ili kushinda uchaguzi ni hujuma kwa demokrasia. Baadhi ya wanasiasa pia wameripotiwa wa kuwa Wanatumia fedha zao kusafirisha watu kutoka eneo moja hadi jingine ili wajiandikishe kuwa wapiga kura na wawachague katika uchaguzi ujao. Huu pia ni ukiukaji wa misingi ya demokrasia.

Ununuaji wa wapiga kura unamanisha mabwanyenye ambao wamehusishwa na sakata mbalimbali za ufisadi ndio nyadhifa mbalimbali za uongozi kwa kuwa wao ndio wana mabunda ya fedha za kuhonga wapiga kura.Viongozi wanaochaguliwa baada ya kuwahonga wapiga kura huwatafanya maendeleo yoyote na badala yake, watakuwa wakihusika na wizi wa rasilimali za umma ili kupata fedha za kuwahonga watu katika uchaguzi unaofuatia. Mabwanyenye hawa wanafanya kila wawezalo kuhakikisha wapiga kura wanaendelea kuzama katika lindi la maskini ili waweze kununuliwa kwa urahisi. Sawa na Esau katika Bibilia tuliyeelezwa kwamba aliuza urithi wake wa kuzaliwa kwa Yakobo kwa kubadilishana na chakula,maskini pia wako tayari kuuza haki yao ya kuchagua kiongozi bora kwa Shilingi mia moja.

Viongozi wanaotoa hongo kwa wapiga kura kwa lengo la kushinda uchaguzi ni ishara kwamba hawana maono wala sera za maendeleo. Badala yake wanang'ang'ania mamlaka ili kujilimbikizia utajiri wala si kusaidia mpiga kura kujiinua kimaisha. **(Taifa leo. Machi 10,2016)**

MASWALI

(a). Kwa kurejelea kifungu,visa vya kutoa rushwa kwa wapiga kura vinadhihirisha nini? **Alama 3)**

(b). Bainisha jinsi nne ambazo viongozi wa kisiasa wanatumia kuendeleza ukiukaji wa misingi ya demokrasia. **(Alama 4)**

c). Fafanua athari za uozo unaorejelewa katika taarifa kwa

(i). Viongozi. **(alama 2)**

(ii). Raia **(Alama 2)**

(d). Thibitisha kuwa nyani haoni ngokoye katika muktadha wa Makala haya. **(Alama.2).**

(e).Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa **(Alama 2)**

(i). Mitandao ya kijami

(ii). Mabwanyeye

2. UFUPISHO (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa . Inakera mno kwa vitendo vya kigaidi. Inagadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuwawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kwamba magaidi hawa wameelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani, damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini, vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na Imani ya kumwua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi,manaji,unajisi,ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki ya kikatiba ya Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao. Lakini cha kusikitisha ni kuwa,mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kuhusu kinachoendelea,inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha kwennye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako imeishia kunasa raia wengi wasio na makosa. Wanaponaswa,hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadhaa na hata kama wanaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika,mbinu hii yanaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani,magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati,polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka Zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

<u>Maswali</u>

(a). Ni nini maoni wa mwandishi kuhusu suala la ugaidi. **(alama 7 1 utiririko)** maneno 60-70)

Nakala chafu

Nakala safi

(b). Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fupisha aya mbili za mwisho. **(Alama 6, 1 utiririko)**

Nakala safi

Nakala safi

3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)

a. Andika sifa zozote mbili za sauti zifuatazo. **(alama 2)**

(i). /u/

(ii). /ch/

b). Tenga silabi katika maneno yafuatayo kisha uandike muundo wake. **(Alama 2)**

i) igwa

ii) Oa

c). Andika upya sentensi kwa kutumia ‘O’ rejeshi tamati. (**alama 2)**

Gari lililoanguka si lile unalolizungumzia

d). Unda nomino kutokana na kivumishi kifuatacho; **(Alama 1)**

Tepetevu

(e). Badilisha katika usemi halisi **(alama 3)**

Afisa wa usalama alisema kuwa wangemsaidia ikiwa angeshirikiana nao

f). Pambanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha Vishale. **(Alama 4)**

Letu lililopaliliwa limetuletea mazao mengi.

g). Ainisha virai vyovyote vitatu **(Alama 3)**

Mwanafunzi yule mtoro hupenda kutembea katikati ya barabara kila wakati.

(h) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate vifuatavyo: **(Alama 2)**

i) Chaka

ii). Shaka

j). Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao,hali timilifu **(alama.2)**

Mwanafunzi aliandika insha nzuri

k). Andika sentensi hii katika udogo wingi. **(alama.2)**

Mtoto amefunga mlango wa nyumba yao

l). Onyesha matumizi matatu ya alama ya vifungo katika sentensi. **(alama.3)**

m). Eleza maana ya kishazi. **(Alama 2)**

n). Nyambua vitenzi vifuatavyo kama ulivyoelekezwa **(Alama 2)**

i). Suka (kauli ya kutendata)

ii). Pa (kauli ya kutendeka)

o). Onyesha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo.

Babu alijengewa nyumba kwa mawe na Juma. **(Alama 2)**

(p) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kufuata maagizo uliyopewa

Mzazi alishangilia matokeo ya mwana. **(alama 2)**

(Anza Mwana…)

q). Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo.

Mama alinileta Kanga. **(alama.2)**

r). Yakinisha.

Usiponiita sitaandamana nawe **(alama.2)**

s). Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo.

Mgeni alikuwa amewasili jana. **(alama 1)**

ISIMU JAMII **(Alama 10)**

(a). Wewe ni mfanyabiashara katika soko la Chapakazi,eleza sifa tano za lugha utakayotumia kuwasiliana na wateja pamoja na washiriki wengine siku ya soko. **(Alama 10)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA TISA)

KISWAHILI

102/3

KARATASI YA 3 (FASIHI)

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Andika jina lako na nambari yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu*

b) *Tia sahihi kisha uandike tarehe*

c) *Jibu maswali **manne** pekee*

d) *Swali la kwanza ni la lazima*

e) *Maswali hayo mengine **matatu** yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani Tamthilia, Riwaya, Ushairi na Hadithi Fupi*

f) *Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja*

g) *Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU YA A: USHAIRI
SWALI LA LAZIMA
MBELE YA SAFARI

1. Ilipoanza safari , ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

2. Njaa ikawa dhabiti ,na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti ,dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

3. Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari,utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari , juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

4. Ile ilikuwa ndoto , mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto,sahala ‘mekuwa dhiki
Wagombanio kipato,utashi haukatiki
Nakutabakari

5. Msafara ukasita , kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita , mlima haupandiki
Basi sote ‘kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

6. Tukiwa migongo wazi ,tukainama kwa shaki
Tukawa’chia ukwezi , kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi ,Kuteremsha miliki
Wakaitapia

7. Wakafikia makazi,ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

8. Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema , kwa umati halaiki
Imezima nia yote ,kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

a) Eleza safari inayolejelewa katika shairi hili. **(al 2)**
b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. **(al 6)**
c) Taja na ueleze bahari mbili za shairi ukizingatia : **(al 4)**
i. Mizani
ii. Vina
d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari**.** **(al 4)**
e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita **(al 4)**
f) Eleza umbo/ muundo wa shairi hili. **(ala 2)**

SEHEMU YA B: TAMTHILIA
Timothy Arege
BEMBEA YA MAISHA
Jibu swali la 2 au la 3
2.(a.) Soma dondoo lifuatalo kasha ujibu maswali.

Sara : Mimi ninashukuru kwa hawa alionipa mungu. Nikitaka zaidi nitakuwa mchache wa shukrani.(kimya) Dina nimesemwa sanana kutukanwa kwa sababu ya hawa wasichana wangu. Wewe unajua yote yaliyosemwa, hadharani na faraghani. Si makanisani, si magengeni. Leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao, ninaridhika moyoni. Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika. (Anatokwa na machozi)

Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha.
i.) Changanua maudhui katika dondoo hili **(ala 3)**
ii.) Bainisha toni katika dondoo hili **(ala 2)**
iii.) Tambua mbinu tatu za lugha ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. **(ala 3)**
(b.) Jadili jinsi suala la utu linavyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea Ya Maisha**(ala 12).**

AU.

3. Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(ala 20)**

SEHEMU YA C: RIWAYA
C. MOMANYI: **NGUU ZA JADI**
Jibu swali la 4 au la 5
4. "Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."
(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**
(b) Anayesema maneno haya ni jasiri. Thibitisha kwa hoja tano. **(alama 5)**
(c) Tathmini kwa hoja kumi na moja nafasi ya wenye pesa katika kuendeleza tamaa na ubinafsi katika nchi ya Matuo. **(alama 11)**

AU

5. "Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu?" alijiskia kusema. Alishusha pumzi kwa

nguvu akajiuliza kimoyomoyo kwa nini Mungu aliruhusu moto kumtia kwenye shimo la maangamizi na wanawe. Hata hivyo, aliamini kuwa wakati mwingine Mungu huruhusu mabaya kutokea ili kuwafunza waja. Waaidha, alijua kuwa mashaka yanapomkumba mja, huwa ni funzo pia. Humtayarisha kuyahimili machungu zaidi ulimwenguni ama kumuasa dhidi ya kuabudu maovu. Maovu yanapotendwa na wachache, hata wale wasio na hatia pia hujikuta wamo humo uovuni. Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.

(a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 5)**

(b) Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisani aliko Mangwasha katika kukuza Riwaya ya Nguu za Jadi **(alama 5)**

(c) Nchi ya matuo imeshinikizwa na Nguu Za Jadi zinazorudisha nyuma usawa katika jamii. Tathmini kauli hii kwa hoja kumi. **(alama 10)**

SEHEMU YA D :HADITHI FUPI

MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

Jibu swali la 6 au 7

WINNIE NYARURI OGENCHE: ''SABINA''

6. ''Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.''

a) Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. **(alama 6)**

b) Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. **(alama 4)**

c) Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. **(alama 10)**

YUSSUF SHOKA HAMAD: ''*Mzimu wa Kipwerere*''

7."…Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama."

(a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. **(Alama 4)**

(b) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(Alama 4)**

(c) Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. **(Alama 2)**

(d) Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. **(alama 10)**

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

Swali la nane

8. a) Ulumbi ni nini? **(alama 2)**

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii?. **(alama 6)**

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. **(alama 6)**

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. **(alama 6)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA KUMI)

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MUDA: SAA 1¾

JINA……

SHULE…… **SAHIHI**……

NAMBARI YA USAJILI…… **MKONDO**……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

- *Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya **lazima**.*
- *Kisha chagua insha **moja** nyingine kutoka hizo **tatu** zilizobaki.*
- *Kila insha isipungue Maneno **400**.*
- *Kila insha ina alama **20**.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

Swali	Upeo	Alama
1	20	
	20	
Jumla	40	

1. **Lazima**

   Wewe ni Kiranja Mkuu Shuleni Juhudi. Umetembelewa na waandishi wa habari kutoka '**Redio Nipashe'** na '**NTV**'. Wangependa kujua changamoto zilizowakumba wanafunzi wa shule za upili nchini baada ya janga la Korona. Andika mahojiano yenu.

2. " Uvumbuzi wa rununu umeleta madhara mengi kuliko manufaa kwa vijana." Jadili.

3. Maji ukiyavulia nguo huna budi kuyaoga.

4. Andika Insha itakayoishia kwa maneno haya … Nilikuwa nimepanda shari nikavuna laana. Nilijuta kwa nini sikumtunza marehemu nyanya yangu.

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA KUMI)

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

Maagizo

a) *Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

b) *Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*

c) *Jibu maswali **yote**.*

d) *Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

e) *Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
Jumla	80	

1. <u>UFAHAMU: (ALAMA 15)</u>

<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali</u>:

Takwimu zilizothibitishwa zaonyesha kuwa kila sekunde nane mtu mmoja hufa duniani kutokana na utumiaji wa tumbako. Kwa siku basi, watu 10,800 hufa. Wengi wa wavuta sigara huanza katika umri kati ya miaka kumi na mitatu hadi kumi na tisa. Takwimu zaonyesha kuwa mtu akivuta sigara kwa zaidi ya miaka ishirini huupunguza umri wake kwa kati ya miaka 20 hadi 25 zaidi ya ambaye hajawahi kuvuta. Hii ni kwa kuwa tumbako ina zaidi ya kemikali 4,000 zinazodhuru afya.

Mojawapo ya madhara makuu zaidi yanayosababishwa na sigara ni saratani. Kunayo saratani ya ngozi – vidonda visivyopona huchubuka ngozini na baada ya muda hugeuka na kuwa kansa. Iri ya mapafu hutokea vifuko vya hewa vinapopasuka na hivyo kutatiza uvutaji wa oksijeni na utoaji wa kabondayoksaidi. Moshi pia husababisha madhara kwa njia ya kupitisha hewa, yaani umio, ambapo njia hii yaweza hata kuzibika hivyo kulazimu tundu kutobolewa kooni ili mgonjwa aweze kupumua. Kabla ya kufika kooni na mapafuni, moshi hupitia mdomoni. Saratani ya mdomo na ulimi basi hupatikana zaidi miongoni mwa wavuta sigara. Pia kidonda chochote, kwa mfano baada ya kung'olewa jino, huwa vigumu kupona kwa mvutaji sigara.

Kwa wanawake, kuna hatari ya kupatwa na iri ya fuko la uzazi. Madhara kwenye njia nzima ya uzazi huifanya iwe vigumu kwa wanawake wavuta sigara kuhimili. Ni rahisi pia kuzaa njiti. Mtoto wa mvutaji huzaliwa akiwa mwepesi zaidi ya kawaida. Hii husababishwa na kabonimonoksaidi kutoka kwa sigara inayomdhuru mtoto tumboni. Saratani hii husababisha hata kifo cha mtoto aliye tumboni. Wengine wazaliwapo huwa na hatari ya kupatwa na saratani zaidi ya waliozaliwa na akina mama wasiovuta sigara.

Aina zaidi za saratani zinazowakumba wavuta sigara ni kama vile saratani ya pua, ya tumbo, ya figo, ya kibofu cha mkojo, ya kongosho, ya njia ya kinyesi na hata saratani ya matiti inayowaathiri zaidi wanawake.

Shida za sigara sio saratani pekee; sigara husababisha shida za macho na masikio kwa kiasi kikubwa. Mboni ya jicho yaweza kufunikwa na utando, hali inayoweza kusababisha hata upofu. Macho yaweza kuwashwa na moshi mkali wa sigara au mishipa ya macho iathirike na kemikali zinazofika kwayo kupitia kwa mishipa mapafu yanapoathirika. Masikio nayo huathiriwa na uchafu wa tumbako unaoganda kwenye mishipa hadi sehemu za ndani za masikio. Damu hupunguza mwendo ufaao masikioni hivyo yanaugua. Moshi na kemikali za tumbako pia hujeruhi sehemu za ndani na athari hii yaweza kuenea hadi ubongoni na kusababisha utando unaofunika ubongo. Hali hizi zaweza kusababisha uziwi.

Mifupa na meno huathirika pia. Mifupa huwa myepesi, hukosa nguvu na kuwa rahisi kuvunjika. Mvuta sigara akivunjika mfupa huchukua muda wa asilimia themanini (80%) kupona zaidi ya mtu asiyevuta. Meno nayo hutatizika katika ukuaji wake kutokana na kugandwa na moshi wenye kemikali. Hali hii husababisha harufu mbaya, uchafu pamoja na kuoza kwa meno.

Ngozi ya mvuta sigara hukaushwa na kemikali kwa sahabu uwezo wake wa kujirekebisha na kujilainisha hupunguzwa pakubwa. Hali hii husababisha ukavu unaoonekana pamoja na makunyanzi yanayomfanya mvuta sigara aonekane mzee zaidi ya umri wake. Vidole navyo vilevile hugandwa na kutu ya sigara, nazo kucha na vidole hugeuka rangi vikawa vya manjano, hudhurungi au maji ya kunde. Vidole pia hukaushwa na moto na kemikali ya sigara. Nywele za mvuta sigara

pia huathirika kwa kuwa kemikali huipunguza kinga ya mwili hivyo mizizi ya nywele kukosa nguvu. Nywele za mvuta sigara zaweza kung'oka mapema.

Sigara husababisha magonjwa ya moyo na vidonda vya tumbo. Kwa moyo, sigara husababisha shinikizo la damu na hatimaye mshtuko wa moyo waweza kutokea na kusababisha hata kifo. Kwa tumbo, sigara hupunguza uwezo wa kinga zake wa kuikinga dhidi ya asidi zinazosaga chakula. Pia hupunguza uwezo wa mwili wa kujikinga dhidi ya vidonda vya tumboni. Vidonda vya tumbo vya mvuta sigara huwa vigumu kupona na, ni rahisi kutokea tena baada ya kupona.

Kwa mwanamume, mpigo wa damu kwenye sehemu za uzazi huathiriwa. Hali hii ikizidi husababisha hata upungufu wa nguvu ya mbegu kwenye shahawa. Hata ugumba waweza kutokea. Pia watoto wa mwanamke mvuta sigara waweza kuzaliwa wakiwa na kasoro. Mimba zingine zilizotungwa na wanawake wavuta sigara pia hutunguka. Na si hayo tu; madhara ya sigara ni mengi zaidi.

Maswali

a) Yape makala haya kichwa. **(alama 2)**

b) Mbali na athari kwa uzazi kwa wanawake na wanaume na sura/umbo la binadamu, taja madhara mengine ya uvutaji sigara kwa binadamu. **(alama3)**

c) Kwa kurejelea kifungu onyesha kwamba sigara kwa wanawake hasa ni hatari mno. **(alama 4)**

(d) Je, ni kweli kuwa vifo vingi hutokea kwa sababu ya uvutaji sigara? Toa sababu. **(alama 2)**

(e) **Eleza** namna ambavyo uvutaji sigara huathiri sura ya mhusika. **(alama 3)**

(f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kwenye taarifa. **(alama 1)**

Gandwa ___

2. UFUPISHO:(ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali:

Biashara ya kimataifa ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ile. Nchi mbalimbali zimekuwa zikitegemeana kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, nchi ya Kenya imekuwa ikiuza maua na mboga katika nchi za ng'ambo na kupata fedha za kigeni ambazo hutumiwa humu nchini kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Biashara ya kimataifa huziwezesha nchi ambazo hazizalishi bidhaa na hata huduma mbalimbali kupata bidhaa hizo kutoka nchi nyingine zinazohusiana nayo katika biashara. Mathalan, Kenya ni nchi ambayo imekuwa ikitegemea kilimo lakini haijaendelea katika sekta ya viwanda. Kenya huagiza bidhaa kama vile vipuri vya magari na hata magari yenyewe kutoka nchi kama vile Japan. Nayo Kenya huuza mazao ya shambani kama vile pareto, chai na kahawa ng'ambo.

Kupitia kwa biashara ya kimataifa, nchi hupata masoko kwa bidhaa zake. Kwa vile biashara ya kimataifa huziwezesha nchi husika kuzalisha bidhaa mahususi ambazo hazitaigharimu nchi pesa nyingi kuzalisha, nchi hizo aghalabu huzalisha kiasi kikubwa cha bidhaa kuliko mahitaji yake ya nyumbani. Nchi basi hulazimika kutafuta masoko nje ya mipaka yake. Kwa njia hii uchumi wa nchi huendelea kuimarika.

Aidha, biashara ya kimataifa huwezesha nchi kupata huduma za kitaaluma ambazo hazipatikini katika nchi husika. Kuna nyanja za kiuchumi ambazo huhitaji wataalamu mahususi. Kwa mfano, katika sekta ya matibabu nchini humu tumepata kwamba kuna baadhi ya magonjwa ambayo yanahitaji matibabu maalumu. Wanaougua magonjwa haya huagiziwa madaktari kutoka ng'ambo au hata kupelekwa ng'ambo kwa uchunguzi na matibabu zaidi.

Biashara ya kimataifa hukuza ushirikiano wa kimataifa. Nyakati za majanga ya kimaumbile na hata mengine yanayosababishwa na kutowajibika kwa binadamu, nchi hupata usaidizi kutoka nchi za ng'ambo. Kwa mfano wakati wa mkasa wa bomu wa 1998, Kenya ilipata msaada wa kukabiliana na janga hili kutoka Israeli, Marekani na hata Ujerumani ambako baadhi ya waathiriwa wa mkasa huo walipelekwa kwa matibabu zaidi. Ushirikiano huu wa kimataifa huwezesha wananchi kutoka nchi fulani kwenda kusomea na hata kufanya kazi katika nchi nyingine. Katika miaka ya hivi karibuni Wakenya wengi wamekuwa wakienda kusomea vyuo vikuu vya ng'ambo. Wengine wamediriki kupata kazi katika mashirika ya kimataifa katika nchi mbalimbali kama vile Afrika Kusini, Rwanda, Msumbiji na kadhalika.

Biashara ya kimataifa husaidia kukuza ushindani kati ya nchi husika. Ushindani huu ni hakikisho la uzalishaji wa bidhaa za thamani bora. Kila nchi itafanya juu chini kuzalisha bidhaa ambazo zinaweza kukubalika katika soko la kimataifa. Pia wananchi wa nchi husika hupata aina tofauti za bidhaa badala ya kutegemea aina moja tu ya bidhaa zinazozalishwa nchini mwao.

Biashara ya kimataifa huleta ushirikiano wa kisiasa na uelewano zaidi kati ya madola mbalimbali. Mathalan muungano wa nchi za Afrika Mashariki – Kenya, Uganda na Tanzania, hauchangii tu kuleta manufaa ya kiuchumi bali huleta ushirikiano zaidi wa kisiasa.

Ingawa biashara ya kimataifa ina natija, biashara hii huandamana na hasara mbalimbali. Biashara hii imesababisha kuwapo kwa masoko huru ambayo yameleta ushindani mkubwa kwa wafanyibiashara wadogo wa humu nchini. Baadhi ya wafanyibiashara wamelazimika kufunga biashara zao baada ya kufilisika. Ushuru mkubwa unaotozwa baadhi ya bidhaa nchini huwafanya wananchi wengi kutofaidika kwa bidhaa na huduma kutoka nje. Aidha, kuna ucheleweshaji wa bidhaa zilizoagizwa. Bidhaa hizi mara nyingi huchukua muda kabla ya kutoka nchini, kwa hivyo wafanyibiashara wengi hulazimika kungojea kupata bidhaa hizi na kuwauzia wateja wao.

Vilevile, kutokana na biashara ya kimataifa, bidhaa duni huweza kupenyezwa katika mataifa yanayoendelea. Pia baadhi ya wafanyibiashara wa kimataifa huchukua fursa hii kulangua dawa mbalimbali za kulevya ambazo huwaathiri vijana wa nchi husika. Wengine huhusika katika vitendo vya kigaidi kama vile uchomaji wa majengo mbalimbali kwa bomu na mauaji ya ananchi wasio na hatia.

Ni kweli kuwa biashara ya kimataifa ina hasara zake. Hata hivyo mhimili mkubwa wa uchumi wa mataifa machanga.

(a) Kwa maneno yasiyozidi **themanini**, eleza umuhimu wa biashara ya kimataifa**.(alama 7)**

Matayarisho

Nakala safi

(b) Kwa maneno yasiyozidi **40**, eleza ujumbe wa aya tatu za mwisho. **(alama 6)**

Matayarisho

Nakala safi

3.MATUMIZI YA LUGHA

(a) Sahihisha sentensi: **(alama 2)**

(i) Mitume hiyo siyo ambayo tunaijua.

(ii) Wasikilizaji sasa wanaburudika na muziki kutoka idhaa la taifa hii.

(b) Ikanushe sentensi hii katika umoja. **(alama 2)**

Wasingecheza kiustadi wasingeshinda katika michezo ile.

(c)Tambulisha nyakati na hali katika sentensi: **(alama 2)**

(i) Wachezaji walikuwa wanafanya mazoezi.

(ii) Nkirote alipoingia alitukemea.

(d) Eleza maana za sentensi. **(alama 2)**

(i) Kwa nini wasililie hapa?

(ii) Kwa nini wasilie hapa?

(e)Toa mifano miwili miwili ya sauti zinazotamkiwa katika : **(alama 2)**

(i) ufizi ……

(ii) meno ……

(f) Andika udogo na ukubwa wa neno ‘kidole’. **(alama 2)**

(i)……(ii)……

(g) Tunga sentensi mbili tofauti kubainisha matumizi ya KWA. **(alama 2)**

(h) Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi ifuatayo. **(alama 2)**

Msichana alimkaririra mgeni shairi.

(i) Tumia vitenzi hivi katika sentensi mojamoja katika jinsi ya kufanyiwa. **(alama 2)**

(i) nywa

(ii) pa

(j) Kistari kifupi (-) aghalabu hutumika kuendeleza sauti hasa katika vihisishi. Onyesha matumizi mengine matatu ya alama hii akifishi. **(alama 3)**

(k)Tunga sentensi kubainisha tofauti kimaana kati ya vitawe: **(alama 2)**

(i)juha……

(ii)jua……

(l) Ziandike upya sentensi hizi kwa mujibu wa maagizo uliyopewa. **(alama 2)**

(i) Kiyondi aliukomelea mlango alipovisikia vishindo.

(Anza kwa :Mlango……..)

(ii) Mvua ilinyesha sana alasiri hiyo. Wachezaji walicheza mpira vizuri tu.

(Tumia 'japo')

(m) Tunga sentensi sahihi kubainisha matumizi ya KI kuonyesha: (alama 4)

(i) masharti

(ii) ngeli

(iii) kufanyika vitenzi viwili au zaidi wakati mmoja

(iv)kielezi namna

(n)Tambua hali na matumizi ya kisarufi ya neno lililopigwa mstari katika sentensi: (alama 1)

Mtu mzee anapaswa kuheshimiwa

(o) Andika katika usemi halisi. (alama 2)

Mwalimu aliwaagiza wanafunzi warudi darasani, warejelee madaftari yao ya kumbukumbu na kuikosoa kazi hiyo.

(P)Andika katika umoja. **(alama 2)**

Tembe ambazo tulizimeza zilikuwa chungu.

(q)Eleza maana za semi au nahau: **(alama 2)**

(i) kwenda mbweu

(ii) shika sikio

(r) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha jedwali **(alama 4)**

Kiatu kilichonunuliwa juzi kimerejeshwa dukani.

4. ISIMU - JAMII

(a) Eleza ukionyesha bayana tofauti baina ya lahaja na lafudhi. **(alama 4)**

(b)Taja sifa tatu tambulizi za lugha ya misimu **(alama 3)**

(c) Orodhesha sifa kuu za sajili ya siasa. **(alama 3)**

UTABIRI WA MWISHO WA KCSE 2025

(JARIBIO LA KUMI)

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MUDA: SAA 2½

JINA……

SHULE…… SAHIHI……

NAMBARI YA USAJILI…… MKONDO……

Cheti cha Kuhitimu Kisomo cha Sekondari (KCSE)

MAAGIZO:

a) *Jibu maswali manne pekee.*

b) *Swali la kwanza ni la lazima.*

c) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya,Ushairi, Hadithi Fupi na Fasihi Simulizi.*

d) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*

e) *Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.

SWALI	UPEO	ALAMA
1	20	
	20	
	20	
	20	
Jumla	**80**	

SEHEMU YA A. USHAIRI

1. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Jiulize ni kwa nini, uanzapo kuongea
Sana sana makundini, watu
hukuondokea Ndugu ujitathmini,
hakika umepotea
Sisi twakuombea, mwenye damu ya kunguni!

Mwenye damu ya kunguni, nayo lugha ya
ajuza Wengi hawamtamani, maneno yake
yaliza Yeye ana walakini, dosari kuliko
pweza
Kama wewe umefunza, sote hutuona duni!

Sote hutuona duni, na hilo tumezowea
Kazi zetu zote guni, yeye tu amebobea
Umewachokoza mbuni, mateke
anapokea Sisi twakuombea, upae hadi
hewani!

Upae hadi hewani, ujione kama bingwa
Mewashinda gazetini, wandishi kwako
wapingwa Yeye kwetu mpinzani, metia mipaka
tingwa Twakuombea mtafiti, hesabu hadi
mizani!

Hesabu hadi mizani, utunge kwa kukosoa
U hodari hesabuni, nasi tushakuzoea
We nduli kwa majirani, na waja mekutegea
Kurekebisha hujui, ywatanika peupeni!

Ywatanika peupeni, ywajisifu mjuaji
Amezidi zetu mboni, na amevijunjia mji
Twamwachia waamuzi, kesi wasome
majaji Sisi twakuombea, sirekebike
kidogo!

a) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili**(alama 6)**

b) Tambua miundo wa shairi hili**(alama 4)**

c) Tambua bahari ya shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa maneno.**(alama 2)**

d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari**(alama 4)**

e) Tambua aina tatu za takriri zinazojitokeza**(alama 3)**

f) Onyesha toni ya shairi hili**(alama 1)**

SEHEMU YA B.

TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA NA TIMOTHY AREGE

2. "…haikuwa mara moja mnavyofikiria. Ilianza pale chuoni. Wenzangu walinipa mvinyo kunirai kuonja ulevi."

a) Eleza maudhui manne yanayojidokeza katika dondoo hili.**(alama 4)**

b) Eleza athari za mhusika anayerejelewa kujitosa katika suala linalooredheshwa kwenye dondoo. **(alama 6)**

c Kwa kurejelewa mifano mitano katika tamthilia ya Bembea ya maisha, eleza tofauti iliyopo katika maisha ya ndoa ya zamani na sasa
(alama 10)

AU

3. " Maskini mke wangu ! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo . Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imemsimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. Siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mfuriko msimu wa masika…Sasa nimekata shauri …Pombe! Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu . Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa"

a) Changanua mbinu **sita** za kimtindo zilizotumika katika kifungu hiki. **(alama 6)**

b) Taja na ueleze maudhui **manne** yanayojitokeza katika dondoo. **(alama 4)**

Jadili sababu kumi zilizompeleka mwandishi T. Arege kuandika Tamthilia hii. **(alama 10)**

SEHEMU YA C . RIWAYA YA NGUU ZA JADI

4."Nikupe ushauri dada.Kaa mbali naye kwani Yule ni moto wa kuotewa mbali.Ukimfuatafuata,anaweza kukutendea mambo mabaya"

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 4)**

b)Tambua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. **(alama 4)**

c)Andika sifa nne za "dada" anayetajwa na msemaji katika dondoo hili. **(alama 4)**

d)Jadili ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari. **(alama10)**

AU

5.

a)Chambua mtindo. **(al 8)**

Walitembea kuelekea mahali hapo kwa muda wa nusu saa.Mwishowe,waliona korongo kubwa.Ndanimwe,mlikuwa na walevi waliolala fofofo.Walikuwa wakipokezana mikoromo mizigo mizito iliyowashtua kina mama wale.Walijua lazima Mrima angekuwa hapo.Walipitapita huku wakiwakaguanyuso.Hakuna uso uliofanana na ule wa Mrima.Mangwasha akazidi kufadhaika.Alikuwa na uhakika kama mchana kwamba angemkuta mumewe mahali hapo.Wakaamua kwenda katika upande wa pili wa korongo hilo.Hapa pia palikuwa na walevi waliolewa chakari.Baadhi yao walikuwa wanavuta sigara.Wengine waliendelea kubugia pombe kutoka katika chupa walizobeba.Wengine tayari walikuwa wametekwa na usingizi.Walilala

vinywa wazi bila kujali nzi waliong'ong'a nyuso zao.Lonare ndiye aliyemtambua Mrima.Alikuwa amelala kifudifudi,kaegemeza kichwa kwenye gogo.Lonare alimsukasuka ili aamke lakini wapi.

Mrima alikuwa akitabaradi kwenye ndoto zake,hana habari wala taarifa.Mkewe aliamua kumwita kwa nguvu huku akimfinya sikio.Mrima alihisi maumivu,akafungua jicho moja na kusema,"Nikilaala…shida i..iko wapi?Kwendeeni huko…ma…loofa nyie."Waliamua kumwinua.Walimbeba hobelahobela hadi kwenye gari.Alikuwa hatazamiki.Uchafu wa siku nyingi ulimfanya kunuka kama kisonzo.Nywele zilizosokotana.Maneno yalipiga manjano kutokana na ugaga uliokolea.Alivaa nguo bwaga mtwae tu.Nguo hizo zilicheua harufu mbaya mithili ya kicheche.Mangwasha chozi la huzuni lilimdondoka.Mrima alilalama huku akitoa matusi lakini hakuna aliyemsikiza.Lonare aliamua kumpeleka hospitali moja kwa moja.Hali yake ilihitaji matibabu ya dharura.Matibabu ya mwili na akili.

b)Jadili umuhimu wa mandhari ambamo kifungu hiki kimenukuliwa. **(al 12)**

SEHEMU D: HADITHI FUPI

D.W. Lutomia na Phibbian Muthama (wah.): *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

Jibu swali la 6 au 7

Msibu wa Kujitakia - D. W. Lutomia

6. … kesho hoja zitakuwa msingi wa kupimia ubora wa wawaniaji uongozi.

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama 4)**

b) Fafanua mbinu **nane** ambazo viongozi katika jamii hii wanatumia kupata uongozi. **(alama 8)**

c) Ukirejelea hadithi hii jadili jinsi wahusika mbalimbali wanavyojutia maamuzi yao. **(alama 8)**

7. a.Eleza nafasi ya vijana na wazee katika hadithi ya Mapambazuko ya machweo. **(alama 10)**

Nafasi ya vijana

b. Kwa hoja tatu, eleza umuhimu wa msimulizi katika kuendeleza hadithi ya mzimu wa kipwerere **(alama 10)**

SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8.Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali yanayofuata.

Msichana wa sura mzuri
Kitu gani kinakufanya usiolewe
Elimu unayo ya kutosha
Hata ngambo ukaenda ukarudi

Msichana wa urembo kama wewe
Uonyeshe mapenzi kwa vijana
Ukionyesha majivuno kwa vijana
Utazeeka ukiwa nyumbani kwenu

Ooh baby miaka yaenda mbio sana…

a) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha. **(alama 2)**

b) Taja shughuli mbili za kijamii katika utungo huu. **(alama 2)**

c) Eleza toni ya utungo huu. **(alama 1)**

d) Wewe kama mwasilishaji wa fasihi simulizi, ni mbinu zipi ungetumia ili kufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. **(alama 5)**

e) Maandishi ni mojawapo ya vifaa vya kukusanya na kuhifadhi fasihi simulizi. Tathmini udhaifu wa kutumia mbinu hii. **(alama 5)**

f) Eleza changamoto zozote nne zinazoweza kumkumba mtu ambaye angependa kuusanya data kuhusu kiperahiki.

KCSE 25

Kupata nakala za majibu, Tafathali wasiliana na;

0746 222 000
0742 999 000

kcsepredictions@gmail.com

Inayoendeshwa na Bw. Isaboke

MAFANIKIO!

DEAR KCSE 2025 CANDIDATES,

In case part/all of these questions reflect in Final KCSE 2025 exam, calm down & be easy.Exercise Extreme caution.

Don't panic!

KCSE 25